# KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA

*FOR FORM 2, 3, 4 NOTES, SMS OR WHATSAPP:* 0723981225

# INSHA

- ☝ Utungo unaoundwa kwa mfululizo wa sentensi zinazozungumzia jambo, tukio au kitu fulani

**Aina**

**1. INSHA ZA KAWAIDA**

**a) Insha ya Picha**

- ☝ Ambapo mwanafunzi amepewa picha kadha na kutakiwa kutunga kisa na kueleza yote yanayotokea kwenye picha hizo. Chunguza vizuri ujue kinachotokea katika hizo picha.
- ✔ Kichwa kiafikiane na picha ulizopewa. Kila picha ipangwe na kuwa na aya moja.

**b) Insha ya Methali**

- ☝ Insha inayosimulia kisa kinachoonyesha ukweli au uongo wa methali Fulani.
- ✔ Wazia methali nyingine za kutilia mkazo methali uliyopewa.

**Muundo**

Kichwa
methali yenyewe
Utangulizi

i. Maana ya juu/wazi
i. Maana ya ndani/batini

Mwili
kisa kinachofungamana na methali cha kweli au cha kubuni
Hitimisho
funzo/maadili

**c) Insha ya Maelezo**

Inayohusu kutoa ufafanuzi kuhusu mahali, kitu au jambo fulani kama vile ugonjwa wa ukimwi, umuhimu wa maji, n.k.

**d)** **Insha ya Masimulizi**

Ambapo unatakiwa kusimulia hadithi, kisa au tukio kuhusu jinsi mambo fulani yalivyotokea. Huweza kuanzia kwa 'Ilikuwa…'

**e)** **Insha ya Mdokezo**

Ambapo umepewa mdokezo wa kuanzia (xxx…) au kumalizia (…xxx) k.m. '…tangu siku hiyo alikula yamini kutopuuza ushauri wa wazazi wake tena'

**f)** **Insha ya Mjadala**

Ambapo unatakiwa kujadili suala fulani k.m. 'Shule za mabweni zina manufaa' au 'Kujiajiri ni bora kuliko kuajiriwa' Jadili.

Unapaswa:

Kuunga
Kupinga
Kutoa uamuzi kutegemea upande ulio na hoja nyingi au nzito.

**g)** **Insha ya Mawazo**

Inayohusu mambo ya kuwaza kuhusu jambo fulani k.m. 'MIMI NYUKI'

✔ Ni nani asiyenifahamu mimi nyuki.

**a)** **Insha ya Mazungumzo**

✔ Maongeo ya kawaida ambayo huandikwa kama tamthilia
✔ MAZUNGUMZO BAINA YA…

**Muundo**

✔ Kichwa
✔ Jina la msemaji kwa herufi kubwa likifuatwa na koloni
✔ Maneno ya msemaji
✔ maelezo ya mandhari na vitendo vya msemaji kwenye mabano
✔ Wazungumzaji wasikike kama watu wa kawaida
✔ Pawepo na sentensi ndefu na fupi
✔ Matumizi ya vihisishi
✔ Ukatizaji wa maneno…

**2.** **TUNGO ZA KIUAMILIFU**

☝ Ambazo hutekeleza kazi maalum na huwa na muundo maalum.

**Dayalojia**

☝ Mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi kuhusu jambo au mada fulani
DAYALOJIA BAINA YA…
Huwa na utangulizi, mwili na hitimisho

**Mahojiano**

- Mazungumzo yanayoendeshwa kwa muundo wa maswali na majibu (MAHOJIANO BAINA YA…)

**Barua ya Kirafiki**

- Inayoandikwa kwa ndugu, jamaa na marafiki.

**Muundo**

Anwani ya mwandishi (wima au mshazari. Jina lisiwekwe!)
Tarehe ya kuandikwa barua (22 Februari, 2011)
Mwanzo wa barua (kwa … mpendwa/kwenu…
utangulizi (salamu, kumjuliana hali)
mwili/yaliyomo (ujumbe)
Hitimisho (Kwa leo sina mengi. Wasalimie jamaa wote. Ni mimi wako/wenu, Jina (wima au mshazari)

**Barua Rasmi/Kwa Mhariri**

Barua ambazo huandikwa na kutumwa ofisini kwa kutaka kuomba kazi, kuomba msaada, malalamiko, kutoa maoni gazetini, n.k.

**Muundo**

- ✔ Anwani ya mwandishi (wima au mshazari)
- ✔ Tarehe ya kuandikwa (usiweke jina).
- ✔ Marejeleo k.m. REJ: SUD/MSS/054/009 (nambari ya kumbukumbu, faili au nambari ya barua)
- ✔ Cheo na anwani ya mwandikiwa k.m. Mkurugenzi, Kiwanda cha majani chai cha Kangaita, S.L.P, 12000, Kerugoya au Mhariri wa Gazeti la 'Nation', S.L.P 89000, Nairobi au KWA ANAYEHUSIKA
- ✔ Kupitia kwa: MWALIMU MKUU, anwani
- ✔ Mtajo k.m. Kwa Bwana/Bibi/Profesa/Daktari/Mhubiri
- ✔ Kichwa cha barua k.m. MINT: OMBI LA KAZI YA UALIMU/MAPENDEKEZO KUHUSU JUMA MRISHO/ MWALIKO WA KUHUDHURIA KONGAMANO LA KISWAHILI
- ✔ Utangulizi **(**Mintaarafu ya tangazo mlilochapisha…naandika kuomba…jinsia…ahadi kufanya kazi kwa bidii)
- ✔ Mwili (matatizo, madhara, mapendekezo (naomba, paswa, stahili, naonelea ni bora)
- ✔ Hitimisho (Natumai, Nitashukuru…Wako mwaminifu/mtiifu, sahihi, jina /cheo, Chama cha Kiswahili. Nakala kwa: (i), (ii) (wima au mshazari)

**Barua ya Gazetini Iliyohaririwa**

- ✔ Kichwa (kwa herufi ndogo na usemi halisi)
- ✔ mtajo (Mhariri,)
- ✔ Utangulizi (Naandika kueleza…)
- ✔ Mwili (malalamiko, maoni, maombi, mapendekezo)
- ✔ Hitimisho (Natumai…) jina na anwani ya mwandishi)

**Tahariri**

Maelezo mafupi ya mhariri wa gazeti kutoa mawazo, maoni au msimamo wa chombo cha habari anachowakilisha kuhusu suala maalum na muhimu.

**Muundo**

**GAZETI LA MZALENDO**

**Februari 24, 2011**

**HATIMA YA WATAHINIWA**

**Yaliyomo**

**Imeandikwa na…**

**Hotuba**

- ☝ Maelezo yanayotolewa mbele ya watu.
- ✔ Hutolewa kwa usemi halisi na huanzia na kuishia kwa alama za usemi.

**Muundo**

- ✔ Anwani (HOTUBA KUHUSU…)
- ✔ Utangulizi (kutaja hadhira kuanzia walio mashuhuri, kuwasalimu, kujitambulisha na kuwakaribisha na kutambulisha kiini cha hotuba)
- ✔ Yaliyomo (kutaja na kufafanua hoja)
- ✔ Hitimisho (shukrani na kuwatakia mema katika shughuli zao za kila siku)

**Ratiba**

- ☝ Mpangilio wa jinsi shughuli fulani inavyofanyika kulingana na wakati fulani uliotengwa k.m. sherehe ya arusi, mazishi, siku ya michezo, kutoa zawadi n.k.

**Muundo**

- ✔ Kichwa (Ratiba ya shughuli gani, ya nani, mahali na tarehe, mgeni wa heshima: …Wageni mashuhuri: 1….2….3….)

| SAA | TUKIO | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Asubuhi/adhuhuri** | **Ku…/watu…** | |

- ✔ Makaribisho
- ✔ Maombi
- ✔ Kutoa tuzo
- ✔ Kutoa shukrani
- ✔ Kufungwa kwa maombi
- ✔ Kuondoka/kufumkana

**Shajara**

Daftari ambayo huhifadhiwa matukio yanayofanyika kila siku. Yaweza kuwa ya siku moja, wiki au mwezi mmoja.

**Aina**

a) **Ya kibinafsi**

JUMANNE 30/8/10

Leo tulizuru…

b) **Rasmi (hutumiwa katika ofisi)**

SHAJARA

JUMANNE MEI 7, 2008

| asubuhi | Ku… |
|---|---|
| | |

**Onyo**

Makatazo.

**Tahadhari**

Julisho kuhusu jambo la hatari.

| |
|---|
| **ONYO!**<br>**USISIMAMISHE WALA KUEGESHA GARI KWENYE ENEO HILI!** |

| |
|---|
| **TAHADHARI!**<br>**DARAJA HILI LINA KASORO**<br>**TAFADHALI USILITUMIE** |

**Ilani**

Julisho, tangazo au notisi.

| |
|---|
| **ILANI**<br>**TAFADHALI USITUMIE SIMU**<br>**YA MKONO NDANI YA BENKI** |

**ILANI YA SERIKALI KUHUSU KUZUKA KWA UGONJWA WA KIPINDUPINDU**

Serikali imetoa ilani kwa wananchi kuhusu kuzuka kwa ugonjwa wa kipindupindu. Kila mwananchi anatakikana kuzingatia mambo yafuatayo ili kudhibiti maambukizi.

a) Mtu asinywe maji kabla kuyachemsha
b) Kupika chakula hadi kiive vizuri
c) Kutoenda haja nje bali kutumia vyoo vya mashimo
d) Mtu anawe mikono yake kwa sabuni baada ya kutoka msalani
e) Mtu asile matunda au mboga za majani bila kuziosha kwanza
f) Anayeonyesha dalili ya ugonjwa wa kipindupindu apelekwe katika kituo cha afya mara moja.
g) Uchuuzi wa vyakula umepigwa marufuku
h) Ufuliaji nguo motoni pia umepigwa marufuku

Watakaokaidi maagizo katika (g) na (h) watachukuliwa hatua kali za kisheria ya kutozwa faini ya shilingi elfu tano au kifungo cha miezi miwili gerezani.

**Matangazo**

Majulisho kuhusu jambo fulani.

**a) Arifa**

SHULE YA UPILI YA GATWE

Anwani, tarehe

USAJILI WA …

Sahihi

Jina

Cheo

**b) Kibiashara**
**Sifa**

- ✔ Lugha kwa kifupi
- ✔ Chuku
- ✔ Takriri
- ✔ Alama ya (!) na (?)
- ✔ Michoro
- ✔ Maonyo
- ✔ Maelezo kukihusu
- ✔ Kinavyotumika
- ✔ Ubora wake
- ✔ Watengenezaji

| **JINUNULIE UNGA WA MAHINDI WA** |
| --- |
| **JAMBO SIKU YA LEO. UNGA WA JAMBO UMEONGEZEWA VITAMINI NA MADINI MUHIMU. BEI IMEPUNGUZWA KUTOKA SHILINGI 120 HADI SHILINGI 90. JIPAPIE PAKITI YAKO LEO KABLA BEI HII KUACHA KUTUMIKA** |

**C)Kifo**

TANGAZO LA KIFO

Tunasikitika kutangaza kifo cha …Alikuwa…

Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi

**c) kazi**
SHULE YA UPILI YA GATWE

Anwani, tarehe

NAFASI YA KAZI YA UHASIBU

SIFA ZA MWOMBA KAZI

**JINSIA**

Awe wa jinsia ya kike.

**UMRI**

Awe na umri wa miaka isiyopungua25 na isiyozidi 40.

**ELIMU**

i. Awe na shahada ya uhasibu kutoka chuo kikuu au awe na shahada ya diploma ya juu ya uhasibu
ii. Awe amepata alama ya c katika kingereza

**KAZI**

i. Kuidhinisha hati za malipo za shirika
ii. Kusimamia shughuli za uhasibu katika idara inayohusika

**UZOEVU/TAJRIBA**

Awe na uzoevu wa kazi usiopungua miaka 5 kwenye shirika au taasisi kubwa.

**DINI**

Awe muumini wa dini ya kikristu na awe ameokoka.

**MUDA WA KAZI**

Kuanzia saa mbili hadi saa kumi na moja jioni na masaa mengine ikibidi.

**MSHAHARA**

Mshahara utategemea elimu ya anayehusika lakini utakuwa baina ya ksh 24,000 na ksh 45000.

**MAELEZO YA ZIADA**

i. Maombi yote yawe yamewasilishwa kabla ya tarehe 30 mei 2010.
ii. Maombi yatumwe kwa:

**Katibu,**

**Halmashauri ya shule ya upili ya Gatwe,**

**Anwani**

iii. Maombi yatakayopelekwa baada ya muda wa mwisho hayatajibiwa.
iv. Maombi yaandamane na hundi ya shilingi elfu moja ambazo hazitarejeshwa.

**Maagizo/Maelekezo**

✔ Maelezo kuhusu namna ya kufika mahali kutoka kituo fulani au maelezo kuhusu njia ya kutumia kitu au huduma fulani.

**Sifa**

a) Maelezo wazi
b) Michoro au ramani
c) Dira
d) Huhusika maonyo
e) Tarakimu k.m. 1×3
f) Matumizi ya herufi nzito.

**Mifano**

a) Maagizo ya daktari kwa mgonjwa wa kisukari.
b) Maelekezo ya kutoka nyumbani hadi shuleni mwenu.
c) Jinsi ya kutumia dawa za wadudu

**Kujaza Fomu**

☝ Karatasi ambayo ina nafasi ya kuandika maelezo ambayo yanatakiwa.
a) Soma fomu kwa makini kabla ya kujaza chochote.
b) Andika maelezo kwa muhtasari.
c) Usijaze kama huna hakika kwenye sehemu Fulani.
d) Usifutafute.
e) Itumie alama inayostahili wakati wa kujaza fomu.

**MAELEZO YA KIBINAFSI**

**TAREHE**……………………………………………………

**JINA**…………………………………………………………

**JINSIA**………………………………………………………

**UMRI**…………………………………………………

**TAREHE YA KUZALIWA**……………………………………

**URAIA**…………………………………………

**NAMBARI YA KITAMBULISHO**…………………………

**KAZI**………………………………………………

**MKOA………………………………………………………………**

**WILAYA…………………………………………………………**

**SIMU……………………………………………………………**

**SAHIHI…………………………………………………**

**TAREHE…………………………………………………..**

**Hojaji**

☝ Maswali ambayo hutumiwa kama msingi wa kufanyia utafiti na huelekezwa kwa mhojiwa.

**Aina**

**a) Hojaji Wazi**

☝ Hojaji yenye maswali ambayo mhojiwa anaruhusiwa kuyajibu kwa maneno yake mwenyewe.

**UCHAGUZI NA VIONGOZI**

1. Una maoni gani kuhusu uchaguzi wa kila baada ya miaka mitatu? ……………………………………………………………………… ……………………………………………………………………… ……
2. Kwa nini una maoni hayo? ……………………………………………………………………… ……………………………………………………………………… ……
3. Wewe ungependelea utaratibu gani wa uchaguzi? ……………………………………………………………………… ……………………………………………………………………… ……
4. Je ni kweli viongozi hung'ang'ania mamlaka? ............................................................................................................ ............................................................................................................ ......
5. Je viongozi hung'ang'ania uongozi kwa sababu zipi?

a) ………………………………………………………...……………………
…

b) ……………………………………………………………………………
…
c) ……………………………………………………………………………
….

**b) Hojaji Funge**
Hojaji ambapo mhojiwa anapewa majibu kadha ambayo anatakiwa kuchagua mojawapo bila kuwa na uhuru wa kuandika atakayo.
**MATATIZO YA KIJAMII**

Tia alama kwenye jibu unaloafiki

a) Jamii yetu inawakandamiza wanawake?
Ndiyo (    )   La (    )

b) Tatizo kubwa la jamii yetu kwa sasa ni umaskini na ugonjwa.
Kweli (     )  Si kweli (     )

**Mialiko**

☝ Barua ambayo hupeleka taarifa kwa mtu kumuomba ahudhurie sherehe fulani.

**a) Rasmi (kadi au barua rasmi)**
**Muundo**

✔ Jina la mwalikaji/waalikaji (Bwana/mabwana/bibi/kasisi/daktari
✔ Jina la mwalikwa
✔ Sherehe (ndoa, mchango wa pesa, Kuna aina mbili za mialiko.
✔ Kusherehekea/kuadhimisha…)
✔ Kuhusu nani
✔ Mahali pa kukutanika
✔ Tarehe
✔ Wakati
✔ Anwani na nambari ya simu ya mwalikaji ambapo jibu litapelekwa kushoto chini (Majibu kwa…wima)

**b) Kirafiki (barua ya kirafiki)**
Sehemu ya mwili itoe habari zote muhimu katika mwaliko.
**Risala**

Taarifa inayotoka kwa mtu au watu inayoeleza haja fulani k.m. risaala ya rambirambi, risala ya heri njema, ya waajiriwa kwa mwajiri au kinyume.

**RISALA YA RAMBIRAMBI/HERI NJEMA KWA…KUFUATIA**

Mimi wako…

**Resipe**

Jumla ya hatua na kanuni ambazo hufuatiwa na mtu anayenuia kupika au kuandaa kitu fulani.

**UPISHI WA PILAU**

**Walengwa/walaji**

Mipakuo mine (kwa watu wanne)

**Viambata**

a) Vikombe viwili vya mchele
b) Gramu 25 za mafuta ya majimaji
c) Vijiko viwili vidogo vya pilau masala
d) Nusu kilo ya nyama
e) Vitunguu vinne vya ukubwa wa wastani
f) Vikombe vinne vwa maji

**Hatua za Upishi**

a) Kaanga vitunguu katika mafuta hadi rangi yake ikaribie rangi ya udhurungi
b) Chemsha nyama pekee hadi ilainike
c) Ongeza nyama kwenye sufuria yenye vitunguu na upike kwa dakika tano
d) Ongeza mchele na uchanganye kwa mwiko
e) Ongeza maji na uache mchanganyiko utokote kwa dakika kumi na tano
f) Pakua pilau ikiwa tayari

**Orodha Ya Mambo**

Mlolongo wa vitu vilivyoandikwa.

**MAHITAJI MUHIMU YA KURUDI SHULENI TAREHE 5/1/2010**

a) Sukari kilo mbili
b) Dawa ya meno ya gramu hamsini
c) Koko gramu 500
d) Sabuni sita za kipande
e) Kalamu nne za rangi

f) Penseli moja
g) Rangi ya viatu ya gramu 40

**Tahakiki**

Maandishi ya kuchambua maandishi ya fasihi.

**USASA WAKUTANA NA UKALE**

Anwani: Kitumbua Kimeingia Mchanga

Mwandishi: Said A. Mohamed

Mchapishaji: Oxford University Press

Mhakiki: Amina Fuzo

Maudhui

**Meme**

Barua ambazo huhusisha matumizi ya ya vifaa vya umeme kama talakilishi, kiepesi/nukulishi/faksi au simu ya mkonono/tamba/rukono.

**Barua za Mdahilisi/Pepe**

Ambazo hutumwa kwa tarakilishi kwa njia ya mtandao.

**Ijumaa Machi 30, 2007 saa 08:09:19**

**Kutoka: aisha@yahoo.com**

**Kwa: ahmed@african online.ke**

**Nakala kwa: amina @ mwananchi.com**

**MINT/KUH:**

**Barua ya kawaida**

**Hitimisho: Aisha Kizito Makwere**

**Memo**

Taarifa fupi ambayo huandikwa ofisini kuhusu mambo ya ndani kutoa maelekezo, maelezo au kukumbusha kuhusu jambo fulani. Ujumbe huwa mfupi na huhusu suala moja tu.

**SHULE YA UPILI YA GATWE**

**Anwani**

**MEMO**

**REJ: km/01/06**

**KUTOKA: Mwalimu Mkuu**

**KWA: wafanyakazi wote**

**MADA: likizo fupi**

**TAREHE: 28/2/2011**

**Ujumbe**

**Sahihi**

**Jina**

**Cheo (mwalimu mkuu)**

**Taarifa**

Kuarifu kuhusu habari mpya
**UCHOCHEZI**

**Hitimisho**

**Mariga Mununga**

**Mwanahabari**

**Wasifu**

Maelezo ya mtu kuhusu mtu mwingine tangu kuzaliwa mpaka alipo au kufa kwake.
**WASUFU WA NDUGU YANGU JUMA**

**Tawasifu**

Maelezo ya mtu kujihusu
**TAWASIFU YANGU**

**Vidokezo**

- ✔ Jina lake/lako
- ✔ Jinsia
- ✔ Anakotoka
- ✔ Umri

- ✔ Kuzaliwa
- ✔ Maumbile
- ✔ Elimu
- ✔ Kazi
- ✔ Hadhi ya ndoa
- ✔ Lugha
- ✔ Lakabu na sababu
- ✔ Umaarufu
- ✔ Uraibu

**Wasifutaala/Wasifu Kazi**

☝ Maelezo rasmi kuhusu mtu binafsi ambayo huambatanishwa na barua ya kuomba kazi.

**WASIFUTAALA WANGU**

**MAELEZO BINAFSI**

**Jina** **:** Farida Almasi Juma

**Tarehe ya Kuzaliwa** **:** 7-6-1980

**Umri** **:** miaka 22

**Mahali pa kuzaliwa** **:** Voi

**Jinsia** **:** mwanamke

**Hadhi ya ndoa : Nimeolewa/kapera**

**Nambari ya kitambulisho : 12345678**

**Uraia : Mkenya**

**Lugha : Kiswahili, Kingereza, Kikuyu**

**Anwani ya kudumu : S.L.P. 1600, Voi**

**Barua pepe : Farial@yahoo.com**

**Simu tamba : 9876543210**

**ELIMU**

**Chuo Kikuu cha Maseno (Shahada ya Uhasibu)**
**Shule ya upili ya Shimoni (Shahada ya KCSE)**

**1978-1987** **Shule ya Msingi ya Umazi (shahada ya KCPE)**

**TAJRIBA**

**Mpaka sasa** **Mhasibu katika shule chekechea ya Mtakatifu Yohana**

**HABARI ZA ZIADA**

**URAIBU**

a) **Kusoma vitabu vya sarufi na fasihi**
b) **Kutembelea wajane, mayatima na wagonjwa**
c) **Kuandika mashairi**

**AZIMIO LANGU**

a) **Kupaa kitaaluma kwa kuendeleza masomo yangu hadi kiwango cha uzamifu**
b) **Kuwa mhasibu bora zaidi nchini kwa matendo na kuwapa wananchi huduma za kufaa**

**WAREJELEWA**

1. **Profesa Hassan Muoso,**
   **Chuo Kikuu Kenyatta,**

   **S.L.P.43844,**

   **Nairobi.**

2. **Maimuna Njavu Mukota,**
   **Shule ya Upili ya Alliance,**

   **S.L.P. 1 234,**

   **Nairobi.**

**Kumbukumbu**

- Maelezo kuhusu yaliyojadiliwa na kuafikiwa katika mkutano.

**Muundo**

- Kichwa (kumbukumbu za mkutano wa kamati/jopo gani, uliofanyika wapi, tarehe gani, saa ngapi hadi gani na majira)
- Waliohudhuria (mwenyekiti, katibu, mweka hazina, wanakamati)
- Waliotuma udhuru kwa kutohudhuria
- Waliokosa kutuma udhuru wa kutohudhuria
- waalikwa

- Ajenda

a) Kufunguliwa kwa mkutano (KUMB 3/2OO9)

✔ Kufunguliwa kwa mkutano, mwenyekiti kuwakaribisha na kuwashukuru waliohudhuruia na kumwomba … aongoze kwa maombi.

b) Kusoma na kudhibitisha kumbukumbu za mkutano uliotangulia

✔ Kusomwa na katibu, aliyependekeza na aliyedhibitisha.

c) Masuala yaliyotokana na kumbukumbu hizo

✔ (a) KUMB 8/2008 ununuzi wa miti

d) Shughuli nyinginezo

e) Kufunga mkutano (KUMB 7/2009)

✔ Mkutano uliisha saa ngapi, maombi yaliongozwa na nani, na mwingine ukapangwa kuwa wa siku gani.

- Maneo kama walikubaliana, waliafikiana, alipendekezwa, ilisemekana, waliambiwa, ilionelewa ni bora, walishauriwa, ilidaiwa, aliomba, n.k.

**THIBITISHO**

KATIBU TAREHE…………… SAHIHI ……………

MWENYEKITI TAREHE ………..…. SAHIHI ……………

**Ripoti**

☝ Maelezo kuhusu mtu, kitu au tukio

**a) Ripoti ya Kawaida**

Swali huanzia kwa 'Wewe kama katibu wa chama…'

**Muundo**

- Kichwa (ripoti ya kamati/jopo gani)
- Utangulizi (maelezo mafupi ya jumla kuhusu chama)
- Shughuli za chama (i, ii, iii)
- Hitimisho (matumaini, mwito kwa wengine wajiunge, wajitahidi)
- Ripoti imeandikwa na (jina, cheo/katibu, sahihi, tarehe)

**b) Ripoti Maalum**

- Kichwa (ripoti ya jopo la kutathmini usalama barabarani)
- Utangulizi/Hadidu za rejea (ripoti ilihitajika na kamati gani, uchunguzi ulifanywa kubainisha nini, matokeo kuelezewa chini pamoja na mapendekezo kutolewa)
- Jopo (majina na vyeo vya wanajopo waliohusika)

- Utaratibu/ hatua za utafiti (wanakamati walifanya nini (kamati iliwahoji…ilifanya ukaguzi wa magari, iliwapa baadhi ya wasafiri hojaji wakajaza, ilipiga picha za video, mashauriano)
- Matokeo (kamati iligundua kuwa: (a)
- Mapendekezo (suluhisho la shida)
- Hitimisho (ripoti imeandikwa na, sahihi, jina, cheo/katibu, tarehe 21 Machi 2011.

**3. UTUNGAJI WA/INSHA ZA KISANII**

a) michezo ya kuigiza
b) hadithi fupi
c) mashairi
d) mafumbo
e) vitanza ndimi

# USHAIRI

**Istilahi za Kishairi**

1. arudhi
☝ sheria za jadi zzinazofuatwa na watunzi wa mashairi:
a) kugawa shairi katika beti
b) beti kugawika katika mishororo inayolingana kiidadi
c) mishororo kugawika katika vipande
d) mishororo kuwa na mizani zinazolingana kiidadi (urari wa mizani)
e) kuwa na vina vya kati na vya mwisho vinavyotamkika kwa namna sawa (urari wa vina)
f) mtoshelezo wa beti au beti kutoa wazo kamili
2. bahari
☝ aina tofauti tofauti za mashairi k.m. ukara
3. ubeti/beti
kifungu katika shairi kinachojitosheleza kimaaa
4. mshororo
☝ mstari katika ubeti
5. mwanzo
☝ mshororo katika ubeti
6. mloto
☝ mshororo wa pili katika ubeti

7. mleo
- mshororo wa tatu katika ubeti
8. kimalizio
- mshororo wa mwisho ambao haurudiwi katika kila ubeti
9. kibwagizo/mkarara/kipokeo/kiitikio
- mshororo wa mwisho ambao hurudiwarudiwa katika kila ubeti na hubeba maudhui au kiini cha shairi.
10. kipande/mgao
- sehemu katika mshororo ambayo huonyeshwa na koma na huwa na kina
11. ukwapi
- kipande cha kwanza katika mshororo
12. utao
- kipande cha pili katika mshororo
13. mwandamizi
- kipande cha tatu katika mshororo
14. mizani
- silabi zinazotamkika katika mishororo
15. urari wa mizani
- kuwepo kwa idadi sawa ya mizani katika mishororo
16. kina/vina
- silabi zinazotamkika kwa namna sawa zinazopatikana katikati na mwishoni mwa sentensi.
17. urari wa vina/vue
- kuwepo kwa silabi zinazotamkika kwa namna sawa

**Aina za Mashairi**

a) mashairi la arudhi/ushairi wa kijadi
   Ambayo huzingatia sheria za jadi za utunzi wa mashairi.
b) mashairi huru
- Ambayo hayazingatii sheria za jadi za utunzi wa mashairi.

**Mashairi ya Arudhi**

**a) Aina**

i. tathmina (mshororo mmoja katika kila ubeti)
ii. tathnia (miwili)
iii. tathlitha (mitatu)
iv. tarbia (minne)
v. takhmisa (mitano)

vi. tasdisa (sita)
vii. ushuri (kumi)

**b) Bahari**

viii. mtiririko (mfanano wa vina vya kati na vya mwisho katika shairi zima)
ix. ukara (vina vya mwisho kufanana na vya kati kutofautiana)
x. ukaraguni (vina vya kati na vya mwisho kutofautiana katika shairi zima)
xi. kikwamba (mishororo kuanza kwa neno fulani katika shairi zima)
xii. pindu (neno au maneno mawili ya mwisho ya kila mshororo kutumiwa kuanzia mshororo unaofuata) k.m. kicha changu wachezea. Wachezea kichwa changu.
xiii. Tenzi/tendi (mgao mmoja, kina kimoja)
xiv. Mathnawi (migao miwili, vina viwili)
xv. Ukawafi (migao mitatu, tumbuizo 8,8,8)
xvi. Ngonjera (majibizano)
xvii. Malumbano (kujinaki/kuonyesha ugwiji akimdunisha mshairi mpinzani ili kutaniana)
xviii. Msuko (mshororo wa mwisho mfupi kuliko inayotangulia)
xix. Sakarani (mchanganyiko wa bahari)
xx. Dura mandhuma (kauli/swali katika ukwapi na mjalizo/jibu katika utao k.m. shida zikishinda, hazishindiki. Unalolipenda, halipendeki. Unapopaenda, hapaendeki)
xxi. Gungu (mizani 12, kina kimoja cha mwisho)
xxii. Upeo (mishororo inayozidiana ki mizani)
xxiii. Kikai (mizani 12, 4:8 au 8:4, hakuna ulinganifu wa mizani katika ukwapi na utao)
xxiv. Zivindo (hutoa maana tofauti za neno k.m.
xxv. Sumbila (kila ubeti una kimalizio tofauti na beti nyingine)

**c) Muundo/Umbo/Sura ya Nje**

xxvi. Kutaja idadi ya beti
xxvii. Mishororo mingapi katika kila ubeti
xxviii. Vipande vingapi katika kila mshororo-aina
xxix. Mpangilio wa mizani na jumla k.m. ukwapi 8, utao 8, jumla 16.

8 8

8 8

8 8

8 8

xxx. Mpangilio wa vina au kufanana, kutofanana katika shairi zima au vina vya mwisho kufanana na vya kati kutofautiana-bahari

na ma

na ma

na ma

ka ba

**Vina na Mizani**

8a 8b

8a 8b

8a 8b

8c 8b

xxxi. Kibwagizo(linacho au halina. Kinakili kama kipo)
xxxii. Majibizano (ngonjera)
xxxiii. Malumbano (majinaki)

**d) Uhuru/Idhini za Kishairi**

kibali mshairi alichonacho kukiuka sheria fulani.

i) Inkisari (kufupisha ili kuwe na urari wa mizani na vina. Aghalabu huonyeshwa kwa matumizi ya ritifaa k.m. 'sikate-usikate)
xxxiv. Mazda/mazida (kurefusha neno ili kuwa na urari wa mizani na vina)
xxxv. Tabdila (kubadilisha tahajia ya neno bila kuzidisha au kupunguza mizani k.m. siachi-siati)
xxxvi. Utohozi
xxxvii. Kuboronga/kufinyanga sarufi (kubadili mpangilio wa maneno katika sentensi k.m. upesi jielimishe)
xxxviii. Kiswahili cha kikale/ujadi (mtima, ngeu, insi, mja)
xxxix. Lahaja k.m. ficha-fita
xl. Matumizi ya ritifaa

**e) Lugha ya Nathari**

☝ lugha ya kawaida na kimtiririko
✔ Kutotumia koma au vipande
✔ Kutumia maumbo ya kawaida ya maneno

✔ Ubeti kutengewa aya moja
✔ Kuondoa uhuru na kusanifisha lahaja na kikale
f) matumizi ya lugha/fani
g) matumizi ya maneno (kama yalivyotumiwa)
h) ujumbe
i) maudhui
j) dhamira
☝ kusimanga, kusuta, kudharau, kusifu, kufunza, n.k.

**Mashairi Huru**

**Sifa/Mbinu**

a) urudiaji
i) wa neno (takriri neno)
ii) wa kifungu (usambamba)

**Umuhimu**

kusisitiza ujumbe
kutia ridhimu/mapigo fulani katika usomaji

b) mishata
mishtari ambayo haikamiliki. Mistari toshelezi ni mistari iliyokamilika.
c) sehemu za beti kuingizwa ndani

**Umuhimu**

✔ ili kusisitiza
✔ kuzifanya zionekane wazi

**Ulinganishaji wa Shairi la Arudhi na Shairi Huru**

**Kufananisha**

a) yote mawili ni sanaa ya ushairi
b) mishororo kupangwa katika beti
c) yametumia mbinu za lugha za namna moja
d) alama za kuakifisha zinazofanana
e) kufanana kimuundo
f) uhuru wa kishairi

**Kutofautisha**

a) moja ni la arudhi jingine ni huru
b) mishata
c) sehemu za beti kuingizwa ndani

d) kuwa au kutokuwa na urari wa mizani
e) kuwa au kutokuwa na urari wa vina
f) tofauti kimaudhui
g) idadi ya beti
h) idadi ya mishororo katika beti
i) vipande
j) kutumia alama za uakifishi tofauti
k) uhuru wa kishairi

**MASUALA IBUKA**

**Magonjwa**

**Aina**

d) malaria
e) mafua
f) macho
g) ngozi
h) meno
i) kifua kikuu
j) homa ya mapafu
k) kifaduro
l) zinaa (kaswede/syphilis)
m) kipindupindu
n) homa ya matumbo
o) homa ya mapafu
p) shinikizo la damu
q) ugonjwa wa moyo
r) matumbwitumbwi/machapwi
s) saratani
t) utapia mlo
u) ukambi/surua
v) tetewanga
w) homa
x) malale

**Jinsi ya Kujikinga na Magonjwa**

✔ Kula chakula chenye virutubisho vyote na madini
✔ Kutotumia chumvi, sukari au mafuta mengi

- ✔ Kufanya mazoezi
- ✔ Kupimwa mara kwa mara
- ✔ Kupika vyakula vizuri
- ✔ Kunawa mikono na macho
- ✔ Kuchemsha maji au kuyatia dawa kabla ya kuyanywa
- ✔ Kutozini au kutumia kinga
- ✔ Chanjo kwa watoto
- ✔ Kutochangia vifaa kama vitana na nyembe na mavazi ili kujikinga na magonjwa ya ngozi.
- ✔ Kulala ndani ya neti iliyotiwa dawa
- ✔ Kufyeka nyasi karibu na nyumba na kutupa mikebe iliyo na maji
- ✔ Kuweka dawa kwenye vidimbwi ili kuua mbu
- ✔ Kutotumia vileo kama vile pombe na sigara
- ✔ Kuzuia kunyeshewa na mvua na kuvaa mavazi mazito wakati wa baridi au usiku
- ✔ Kukohoa au kupiga chafya mtu akiwa ameziba pua na midomo na kutotema kikohozi ovyo
- ✔ Kutubu dhambi, kujua Mungu na kuomba kwa afya ya kiroho

**Ukimwi**

- ☝ Ugonjwa unaosababishwa na virusi vya HIV unaofanya mwili kupungukiwa na kinga dhidi magonjwa.

**Njia za Maambukizi**

a) Uzinzi, ubakaji au ulawiti
b) Tohara ambapo ngariga anatumia kisu kimoja kwa watahiriwa wote
c) Kuchangia vifaa vyenye ncha kali k.v. nyembe, vinyoleo n.k.
d) Utumiaji wa sindano moja na vifaa vya upasuati ambavyo havijatiwa dawa au kutokoswa ili kuua viini
e) Wanawake kuambukiza watoto wakijifungua
f) Kuongezewa damu ambayo haijapimwa au haijapimwa vizuri.
g) Utumiaji wa dawa za kulevya kwa kujidunga kwa sindano moja
h) Ulevi kumfanya mtu kupotewa na utambuzi kisha kufanya ngono na mtu aliyeambukizwa.
i) Kubusu mtu aliye na virusi ukiwa na vidonda kinywani
j) Wakati wa ajali watu walio na viini wanapojeruhiwa na kutokwa na damu na inafikia majeraha katika miili ya wasio na hivyo viini

**Dalili**

- ✔ Kukohoa kwa muda mrefu
- ✔ Kuendesha kwa muda mrefu
- ✔ Kupoteza hamu ya kula
- ✔ Kukonda au kupoteza uzani wa zaidi ya kilo 10 kwa muda mfupi
- ✔ Mwili kudhoofika/unyonge
- ✔ Kunyonyoka nywele
- ✔ Jipu lmwilini
- ✔ Mwasho mkali katika ngozi
- ✔ Vidonda kinywani na kooni
- ✔ Homa na kutokwa na jasho jingi usiku
- ✔ Magonjwa ya kifua kikuu na homa ya mapafu
- ✔ Saratani ya ngozi
- ✔ Kuvimba shingoni
- ✔ Utaahira wa akili k.v. kusahau na kutokumbuka mambo

**Madhara**

- ✔ Jamaa kuathirika kisaikolojia wakiona mtu wao akiteseka na ugonjwa
- ✔ Vifo kwa kuzidiwa na ugonjwa
- ✔ Huzuni baada ya mgonjwa kuaga dunia
- ✔ Watoto kuachwa wakiwa mayatima baada ya wazazi kufa
- ✔ Gharama kubwa ya kugharamia matibabu
- ✔ Unyanyapaa/kutengwa/kubaguliwa
- ✔ Ndoa kuvunjika kutokana na lawama
- ✔ Ubakaji wa watoto wa kike ili kujitakasa
- ✔ Kuathiri uchumi wa nchi pesa nyingi zinapotumiwa kununulia dawa za kupunguza makali hata za kifua kikuu
- ✔ Serikali kupoteza wataalamu iliyogharamia elimu yao kulazimika kuajiri wataalamu kutoka nje kwa gharama ya juu sana

**Jinsi ya Kujikinga**

- ✔ Kutofanya zinaa kabla na nje ya ndoa
- ✔ Walioambukizwa kutumia dawa za kupunguza makali (A.R.Vs)
- ✔ Aliyebakwa kupewa dawa za A.R.V kabla ya saa 72
- ✔ Kuwapa mama waja mzito wenye virusi dawa kabla ya kujifungua kukinga mtoto
- ✔ Ngariba kutotumia kisu kimoja kwa watahiriwa wote
- ✔ Kutumia sindano mpya hospitalini na matumizi ya dawa za kulevya
- ✔ Kupima damu vizuri kabla ya kuwaongezea wagonjwa

- ✔ Kupimwa kabla ya ndoa na mara kwa mara ili kujua hali ili kujikinga dhidi ya maambukizi au kujitunza kama mtu ameambukizwa
- ✔ Kutumia mipira
- ✔ Walioambukizwa kutofanya mapenzi bila kinga ili wasipate virusi aina tofauti na sugu au magonjwa mengine ya zinaa
- ✔ Kula chakula vinavyofaa na kufanya mazoezi
- ✔ Kupata matibabu wakati ufaao mtu anapougua magonjwa mengine
- ✔ Kumjua Mungu ili kumwamini na kumtumainia ili kuondoa uoga na mahangaiko na hivyo kumwezeha mtu kuishi siku zaidi

**Unyanyasaji/Udunishaji wa Wanawake na Utamaduni/Taasubi ya Kiume**

- ✔ Kutorithi mali
- ✔ Wanawake wajane kunyang'anywa mali na kufukuzwa
- ✔ Ndoa za wake wengi (uke wenza)
- ✔ Kupata watoto wengi
- ✔ Kurithi wanawake
- ✔ Kupashwa tohara
- ✔ Kutawishwa au kunyimwa uhuru wa kutoka
- ✔ Kutoelimishwa eti kwa akiolewa hatafaidi familia, atapanda wanaume vichwa au atakuwa malaya
- ✔ Ndoa za mapema/lazima zinazosababisha kukatiza elimu yake (mahari haiwezi kurudishwa)
- ✔ Kulazimishwa kuolewa na mtu asiyempenda
- ✔ Kunyimwa haki ya kusema
- ✔ Kupigwa na kutusiwa
- ✔ kubakwa
- ✔ Kutalikiwa
- ✔ Wanaume kutokuwa waminifu kwao hata kuwanyima mahitaji na kuwapa mahawara zao
- ✔ Wanaume kupuuza majukumu ya kukimu familia
- ✔ Ubadhirifu wa wanaume na hali wake zao ndio walifanya kazi za kupatia hizo pesa
- ✔ Kubughudhiwa
- ✔ Kulaumiwa mtoto akikosekana hata mke mwingine kuolewa
- ✔ Mahali pa mwanamke kuwa nyumbani au haruhusiwi kufanya kazi ofisini au kuongoza
- ✔ Kulazimishwa kuvaa mavazi aina fulani na kukatazwa kuvaa aina mengine
- ✔ Kufanyishwa kazi za nyumbani kama mtumwa

Kudhibitiwa na wanaume zao kwa sababu ya vivu.
Kunyimwa ajira kwa vile akipata mimba atajikokota kazini na atahitaji likizo baada ya kujifungua.
Ajira ya mtoto wa kike ambapo anafanyishwa kazi ya sulubu na kupewa mshahara duni

**Suluhisho**

Hatua kali za kisheria kwa wanaowapiga, wanaowabaka na wanaotekeleza mila ya tohara na ndoa za mapema
Kufanya kampeni dhidi ya mila zinazochangia udunishaji wa wanawake
Kuwashauri watoto wa kike badala ya kuwapasha tohara
Kuanzisha makao ya watoto wa kike wanaotishiwa na mila mbaya
Kumwelimisha mwanamke kuhusu haki zake
Kuhimiza wanawake kupigania haki zao
Serikali kutenga pesa za kuelimisha watoto wa kike ili kuwapa uwezo wa kiuchumi kwani wengi hunyanyaswa kutokana na umaskini na ujinga.
Mashirika ya kutetea haki za wanawake kama FIDA na Maendeleo ya Wanawake.
Hazina ya kutoa mikopo kwa makundi ya wanawake k.v. K.W.F.T
Kuwapa wanawake nafasi sawa za ajira na katika uongozi.
Kupunguza alama ambazo wasichana wanazopaswa kufikisha ili kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.
Kubuni sheria za kuwawezesha kumiliki mali

**Jinsi Wanaume Wanavyodhulumiwa**

Kupigwa
Kuchomwa kwa maji moto
Kukatwa sehemu nyeti
Wanawake kutokuwa waminifu kwao
Kutusiwa
Kutofuliwa nguo
Kunyimwa chakula
Kunyimwa unyumba kama njia ya kulipiza kisasi au kumwadhibu
Kufanyishwa kazi fulani k.v. kufulishwa nguo na kupikishwa mke akiwepo hata mbele ya wageni
Kuzomewa/ kugombezwa
Kunyimwa pesa kama hana ajira

**Ufisadi**

- Uovu, ubaya au uharibivu.

**Aina**

Wanafunzi kudanganya katika mtihani
Kufanyiwa mtihani na watu wa nje
Kutoza mwanafunzi wa kidato cha kwanza pesa au chakula kama nyama ili kuwalinda.
Kujipakulia chakula kingi.
Waalimu wakuu kuitisha hongo ili kuruhusu wanafunzi wajiunge na shule zao
Kupita wengine katika foleni wanapokwenda kupata chakula au chai hata benki
Kurudishiwa bakaa/chenji nyingi dukani na kutoirejesha kwa muuza duka.
Kuokota pesa njiani na kutoulizia ni za nani
Kughushi stakabadhi za mtihani, hati za umiliki shamba
Kunakili kanda za muziki za wengine na kuziuza
Waajiri kuajiri watu wa familia zao au makabila yao
Daktari kuitisha hongo ili amhudumie mgonjwa
Polisi kuitisha hongo ili aruhusu magari ya huduma kwa umma yasiyofaa kupita
Kutohoa maziwa au kuyaongezea maji ili yawe mengi
Wenye maduka kuuza bidhaa kwa bei ghali
Kuuza bidhaa kama sukari, nyama, nafaka, gesi na mafuta ya petroli ambazo hazijatimiza uzani unaotakikana
Madereva wanaoendea mafuta ya petroli kuuza kiwango fulani cha hayo mafuta na kuongezea ya taa au diseli
Kuuzia watu dawa bandia zisizotibu magonjwa
Ulanguzi wa dawa za kulevya
Kuiba pesa kwa kutumia risiti bandia au kufuruisha bei za bidhaa ili pesa zilizo juu wahusika wagawane
Kutoa ushahidi wa uongo
Kunyang'anya wajane na yatima mali zao
Uporaji wa mali ya umma k.v. nyanja za kuchezea watoto na misitu
Hakimu kuchukua hongo aididimize kesi
Madaktari kutoza wawele ada ya juu hata kuwafanyia upassuaji wasiouhitaji ili wapate pesa.
Wafanyakazi wa halmashauri za miji kujificha wanapomwona mtu akiegesha gari ili wadai anakwepa kulipa ada ya uegeshaji ili wahongwe au walikokote gari wapate pesa zaidi.

**Sababu Ya Watu Kuushiriki Ufisadi**

- ✔ Tamaa ya kutajirika
- ✔ Kutofahamu madhara/matokeo yake
- ✔ Kukosa njia za kukimu mahitaji
- ✔ Mishahara au mapato duni yasiyomwezesha mtu kukimu mahitaji yake au ya familia
- ✔ Kutotosheka kwa kile mtu alichonacho
- ✔ Hofu ya kupata hasara au kukosa ajira
- ✔ Kutomjua mungu hivyo hawana imani
- ✔ Kuzugwa au kutekwa nyara kimawazo na kuwa mtumwa na shetani
- ✔ Wengine hulichukulia kama jambo la kawaida tu au hali ya maisha
- ✔ Imani kuwa siku hizi mtu hawezi kupata chochote bila kutoa hongo

**Madhara**

- ✔ Vifo kutokana na aajali barabarani au kutotibiwa bila hongo
- ✔ Majeruhi wa ajali za ajalini wengine hulemaa wasiweze kujifanyia kazi zao
- ✔ Kufutiliwa kwa matokeo ya mtihani
- ✔ Kufukuzwa shuleni au chuoni
- ✔ Umaskini kutokana na utoaji hongo ya pesa nyingi kisha kutopata kazi na ununuzi wa bidhaa kwa bei ghali
- ✔ Kushuka kwa viwango vya elimu wasiohitimu ipasavyo wanaporuhusiwa kujiunga na shule ama vyuo fulani
- ✔ Kushuka kwa viwango vya huduma kwa umma kutokana na kuajiriwa kwa watu ambao hawajahitimu vizuri.
- ✔ Afisi za serikali kuchomwa wafisadi wakijaribu kusitiri ushahidi wa ufisadi
- ✔ Nchi kurudishwa nyuma kiuchumi na kimaendeleo kutokana na pesa za miradi au ambazo zingewekezwa katika vitega uchumi kuporwa
- ✔ Kupoteza ajira baada ya kufutwa kazi kutokana na ufisadi
- ✔ Familia kuteseka baada ya kupoteza ajira
- ✔ Kufungwa jela kwa wanaopatikana na kosa la ufisadi
- ✔ Uharibifu wa mazingira na madhara yanayoendana nao kutokana na ufyekaji wa misitu
- ✔ Kudidimiza haki pale kesi inakatwa vibaya kutokana na hongo hata asiye na makosa aweza kufungwa
- ✔ Viongozi wafisadi katika mashirika na asasi kupoteza nyadhfa

**Suluhisho/Njia za Kuukabili Ufisadi**

- ✔ Hatua kali kisheria kwa wafisadi

- ✔ Kulipa wafanyakazi mishahara mizuri
- ✔ Kuelimisha kuhusu madhara ya usisadi
- ✔ Kufuta kazi wafisadi
- ✔ Kunyang'anywa pesa au mali walizopata kifisadi
- ✔ Watu kutangaza mali zao k.v. kwa kujaza fomu kudhihirisha hayo
- ✔ Shirika la kukagua vipimo na ubora wa bidhaa
- ✔ Majina ya wafisadi kutangazwa hadharani
- ✔ Ukaguzi wa hesabu za matumizi ya pesa katika asasi za serikali
- ✔ Shirika la kupambana na ufisadi
- ✔ Kufumania wafisadi
- ✔ Kupiga picha kwa kamera ya video wafisadi k.v. polisi wakichukua hongo
- ✔ Kujifunza kutosheka kwa kile mtu alichonacho na kuishi maisha ya kiwango chake.
- ✔ Kuarifu polisi au shirika la mkupambana na ufisadi kuhusu visa vya ufisadi
- ✔ Kumjua na kumcha Mungu

**Dawa za Kulevya/Mihandarati**

- ☝ Dawa ambazo huathiri utendakazi wa mwili.

**Sababu za Kutumiwa**

- ✔ Masurufu au kuwapa vijana pesa nyingi za matumizi
- ✔ Kujipa burudani
- ✔ Shinikizo la rika kwa vijana
- ✔ Ukosefu wa ushauri/kutojua madhara
- ✔ Matangazo ya biashara
- ✔ Shida k.v. ukosefu wa ajira na mahitaji ya kimsingi
- ✔ Marafiki wabaya
- ✔ Kukaa katika mazingira zinamotumiwa
- ✔ Malezi
- ✔ Kuvunjika kwa ndoa
- ✔ upweke
- ✔ Kujitoa haya k.m. makahaba
- ✔ Shida kazini
- ✔ Kudanganywa zina manufaa k.m. kumpa mtu nguvu ya kufanya kazi au kuerevusha
- ✔ Kujipa hisia za kuwa huru na ujitambuaji

**Madhara**

- ✔ Magonjwa k.v. saratani na ya zinaa

- ✔ Vifo kutokana na ajali, magonjwa au dawa zenyewe
- ✔ Kuiba ili kupata pesa za kununulia dawa za
- ✔ Ubakaji
- ✔ Hufilisi watu kwa kutumia pesa nyingi hata kuuza au kuzikodisha mali zao ili kuzigharamia
- ✔ Jamaa kuathirika kisaikolojia wanapoona mwenzao akiKushindwa kuendelea na masomo.
- ✔ Visa vya ubakaji.
- ✔ Kupotoka kimaadili k.m. kuwa mwenye matusi, kupiga wengine, kuwa mgomvi hata mzinifu.
- ✔ Kuwa mchafu kama fungo k.m. kutooga, kutofua nguo, kutochanua nywele n.k.
- ✔ Kuhisi mambo yasiyokuwepo (hallucination).
- ✔ Wengine kushindwa kuolewa na kutoweza kupata watoto k.m. watumiaji wa miraa.
- ✔ Kuvunjika kwa ndoa kutokana na kupiga mke, kutumia pesa vibaya.
- ✔ Kufutwa kazi k.m. kutokana na ulevi.
- ✔ Wazimu
- ✔ Uhalifu
- ✔ Jamaa ya mtumizi kuteseka ikimwona mwenzao akiangamia kutokana na kuzitegemea dawa za kulevya
- ✔ Mhusika huathirika kimwili na kisaikolojia
- ✔ Huathiri ukuaji wa mwili na akili
- ✔ Wazimu
- ✔ Huathiri uwezo wa kufikiri kwa kuua seli za ubongo
- ✔ Hufanya mtu kupotoka kimaadili k.m. upyaro, vita, uchoyo, uzinifu
- ✔ Kuvunjika kwa ndoa
- ✔ Kufukuzwa shuleni
- ✔ Kufungwa jela
- ✔ Kuzaa watoto ambao hawajatimiza uzani wa wastani
- ✔ Kufa kwa neva na viungo kukatwa

**Suluhisho**

- ✔ Kuelimisha watu kuhusu madhara ya dawa za kulevya
- ✔ Watu kumjua Mungu
- ✔ Matibabu ya kurekebisha watumwa wazo
- ✔ Kujitenga na marafiki wabaya
- ✔ Kutoingia katika mandhari zinamotumiwa

- ✔ Maelekezo kuhusu dawa za matibabu kufuatwa ipasavyo
- ✔ Kutotumia dawa za matibabu kwa matumizi mengine yasiyo ya kutibu
- ✔ Ukaguzi wa wageni na mizigo katika viwanja vya ndege
- ✔ Hatua za kisheria kwa walanguzi, wauzaji na watumiaji
- ✔ Kuongeza nafasi za ajira
- ✔ Kukomesha matangazo ya biashara ya dawa hizo
- ✔ Kuandika matahadharisho katika chupa na pakiti za vileo

**Uhalifu/Utovu wa Usalama**

**Chanzo**

- ✔ Umaskini kusababisha wizi na uisadi
- ✔ Dawa za kulevya kusababisha wizi au kubaka
- ✔ Marafiki wabaya
- ✔ Malezi mabaya
- ✔ Malezi mabaya k.m. mtoto akiiba na kupelekea wazazi, wazazi hawamuulizi alikotoa vitu hivyo.
- ✔ Tamaa ya mali kufanya watu kuiba, kushiriki ufisadi, n.k.
- ✔ Hasira au kushindwa kujidhibiti kusababisha kumpiga na kumuumiza mtu hata kumuua
- ✔ Tamaa kubwa au uchu kusababisha ubakaji.
- ✔ Chuki na wivu huweza kusababisha mauaji

**Suluhisho**

- ✔ Hatua kali za kisheria
- ✔ Kuongeza askari kwani idadi yao ni dogo ikilinganishwa na raia
- ✔ Kuunda vikundi vya kujilinda
- ✔ Vituo vya polisi kuongezwa
- ✔ Vitu vya thamani kuwekwa mahali salama k.m. benki
- ✔ Kutotembea nyakati za usiku
- ✔ Kutoendea mahali kusikofaa k.v. vichochoroni
- ✔ Kuweka ua na lango
- ✔ Mavazi yanayofaa kuzuia ubakaji
- ✔ Kutoa mafunzo ya kujikinga
- ✔ Nambari za simu za dharura za kuripotia uhalifu
- ✔ Kumjua Mungu
- ✔ Kuongeza nafasi za ajira

**Haki za Binadamu**

- ✔ Kuishi
- ✔ Kuingiliana/kutangamana
- ✔ Uhuru na usawa
- ✔ Elimu
- ✔ Makazi
- ✔ Afya
- ✔ Kiwango cha kurithisha cha maisha
- ✔ Chakula
- ✔ Kuabudu
- ✔ Ajira ya watoto
- ✔ Kufanya kazi
- ✔ Kumiliki mali
- ✔ Kutunzwa uzeeni/ hifadhi ya jamii/wasio na uwezo
- ✔ Kupiga kura
- ✔ Kutobaguliwa
- ✔ Kutoteswa kuminya habari
- ✔ Uhuru wa kuongea/usemi
- ✔ Kutembea na kuishi popote
- ✔ Kesi kuendeshwa kwa haki
- ✔ Kujitetea
- ✔ Kuoa au kuolewa na unayemtaka
- ✔ Utulivu k.m. mtoto au mke asipigwe ama kuteswa
- ✔ Huduma za matibabu
- ✔ Jina na utaifa wakati wa kuzaliwa
- ✔ Mtoto mlemavu apewe huduma maalum
- ✔ Alindwe kutokana na mateso, kazi ya sulubu na kuhusishwa vitani
- ✔ Alindwe dhidi  ya mila na tamaduni zisizofaa
- ✔ Haki ya kupata burudani
- ✔ Haki ya faragha/ kuhifadhi siri zake
- ✔ Asiajiriwe
- ✔ asiteswe

**Jinsi ya kuwalinda na kuwatunza watoto**

- ✔ Sheria kubuniwa za kuwalinda
- ✔ Hatua kali kisheria kwa wanaodhulumu watoto
- ✔ Shirika la kupigania haki za watoto
- ✔ Makao ya watoto wanaokimbia wa dhuluma
- ✔ Hazina ya wizara na maeneo bunge ya kufadhili watoto maskini (bursary)

- ✔ Watoto kuelimishwa kuhusu haki zao
- ✔ Kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda mtoto
- ✔ Elimu ya bure ili watoto maskini wafaidi
- ✔ Shule maalum kwa watoto walemavu
- ✔ Wananchi kuchanga kusaidia watoto maskini
- ✔ Makanisa kusaidia watoto yatima
- ✔ Shule kuwapa watoto maskini ufadhili

**Mazingira**

- Hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anakoishi.

**Jinsi Yanavyoharibiwa**

- ✔ Kufyeka misitu ili kupata mahali pa makazi ama kulima
- ✔ Kufuga mifugo kupita kiasi
- ✔ Kutupa taka ovyoovyo
- ✔ Moshi kutoka katika magari na viwanda huchafua hewa
- ✔ Dawa na mbolea za kemikali za kilimo huchafua udongo na maji.
- ✔ Migodi kuacha mashimo ardhini ambayo hujaa maji na kuwa hatari kwa binadamu na kizalio cha mbu.
- ✔ Kelele za vyombo vya mziki, viwanda, honi za magari na ndege
- ✔ mafuriko kuchanganya choo pamoja na maji safi
- ✔ Taka kutoka nyumbani na viwandani kuelekezwa mitoni.

**Madhara**

- ✔ Ongezeko la joto duniani
- ✔ Mvua za gharika
- ✔ Uhaba wa mvua
- ✔ Ukame na njaa
- ✔ Uhaba wa maji
- ✔ Kufa kwa wanyama wa majini kama samaki
- ✔ Magonjwa na vifo kutokana na kuathiriwa na maji machafu
- ✔ Magonjwa ya mapafu kutokana na hewa chafu

**Suluhisho**

- ✔ Kupanda miti kusiko na miti na kule misitu imefyekwa
- ✔ Elimu kuhusu madhara ya kuharibu mazingira na jinsi ya kuyatunza Uhaba wa maji.
- ✔ Kukagua viwabda na hatua za kisheria kama vinavyoachilia taka katika mazingira

- ✔ Kutumia samadi badala ya mbolea za kemikali na dawa za kiasili kuua wadudu katika mimea na mifugo
- ✔ Kutaifisha misitu
- ✔ Askari wa kulinda misitu
- ✔ Kutumia kawi mbadala na ambazo hazichafui mazingira k.v. kutokana na maji na jua
- ✔ Mashimo na mapipa ya kutupa taka
- ✔ Kuweka mifugo kulingana na eneo la malisho
- ✔ Kutolima kando ya mito
- ✔ Kutia choo cha binadamu dawa kabla ya kukiachilia mitoni
- ✔ Kutumia magari ya umma
- ✔ Kutumia taka kama malighafi na kutumia vile vitu vyaweza kutumika tena

**Usalama Barabarani**

**Vyanzo vya ajali**

- ✔ Madereva kutohitimu vizuri
- ✔ Magari mabovu
- ✔ Kutotii sheria za barabarani
- ✔ Njia mbovu
- ✔ Kubeba abiria na mizigo kupita kiasi
- ✔ Kuendesha magari kwa kasi
- ✔ Waabudu shetani kusababisha magari kupoteza mwelekeo
- ✔ Kupita magari mengine bila uangalifu
- ✔ Ulevi
- ✔ Wenda miguu kutokuwa waangalifu wanapovuka barabara
- ✔ Kutodhibiti usukani vizuri
- ✔ Uchovu kusababisha usingizi
- ✔ Dawa za matibabu
- ✔ Abiria kutolalamika au hata kumwambia dereva aendeshe kwa kasi wafike haraka
- ✔ Kuchanganyikiwa

**Suluhisho**

- ✔ Hatua za kisheria kwa wakiukaji kanuni za barabarani
- ✔ Kuondoa polisi wafisadi barabarani
- ✔ Kukarabati barabara
- ✔ Ukaguzi wa magari ili kuhakikisha yafaa kuwa barabarani
- ✔ Kufunza madereva upya

- ✔ Mikanda au mishipi ya kujifunga kuzuia kujeruhiwa vibaya na vifo ajali ikitokea
- ✔ Kuweka vidhibiti mwendo
- ✔ Vifaa vya kutambulia madereva walevi na kasi ya magari
- ✔ Uangalifu wakati wa kupita magari mengine
- ✔ Kuwa mwangalifu wakati wa kuvuka barabara

**Sayansi na Teknolojia**

- ✔ Uvumbuzi wa umeme unaotumiwa kuangazia na kuendesha vyombo vingi
- ✔ Matibabu kuwezesha watu kuishi kwa muda mrefu k.m. dawa,chanjo, upasuaji, upachikwaji viungo, miale ya kutibu saratani, n.k.
- ✔ Kurahisisha na kuharakisha usafiri k.m. magari, pikipiki, ndege, k.m.
- ✔ Kurahisisha na kuharakisha mawasiliano kunakosaidia wakati wa dharura k.m. rununu, mtandao, nukulishi, n.k.
- ✔ Upashaji wa habari kuwezesha kupata habari kutoka kote duniani k.m. satalaiti, mtandao, redio, runinga, n.k.
- ✔ Utengenezaji bidhaa viwandani kuharakishwa kutokana na mitambo inazoendesha na tarakilishi
- ✔ Mimea na mifugo wanaokomaa haraka na walio na mazao mengi
- ✔ Roketi inayowezesha kwenda katika mwezi na sayari nyingine
- ✔ Silaha kama bunduki za kupambana na maadui na wahalifu
- ✔ Burudani bora k.m. sidi, video, mtandao, n.k.

**Madhara**

- ✔ Uavyaji mimba
- ✔ Mauaji ya huruma
- ✔ Tishio la dunia kuangamia kutokana na silaha za nuklia na viini vinavyotengezezewa maabarani
- ✔ Uhalifu kuongezeka kutokana na wingi wa bunduki, simu na mtandao
- ✔ Vyakula kutokana na mimea ina mifugo iliyokuzwa kisayanzi kudhuru afya
- ✔ Wizi wa viungo vya mwili hata kuhasiwa bila hiari
- ✔ Ajali za barabarani na za ndege zinazoua watu wengi
- ✔ Upotoshaji kimaadili kama vile filamu chafu katika mitandao na sidi
- ✔ Kutumia vijusi kutengenezea viungo
- ✔ Ongezeko la joto duniani kutokana na uchafuzi wa hewa
- ✔ Ugaidi kutokana unaotekelezwa kwa mabomu

**Simu za Rununu**

**Faida**

- ✔ Kurahisha na kuharakisha mawasilano
- ✔ Kupunguza gharama za usafiri
- ✔ Mtandao huelimisha na hufahamisha habari
- ✔ Kutuma pesa
- ✔ Kuweka pesa/akiba
- ✔ Burudani k.m. nyimbo, michezo
- ✔ Kupiga nduru uhalifu unapotokeo
- ✔ Ajira kwa wauzaji na watengenezaji
- ✔ Ushuru kwa serikali
- ✔ Shajara, kalenda, kamera, kikokotozi

**Madhara**

- ✔ Burudani kusababisha ajizi
- ✔ Uhalifu
- ✔ Gharama kubwa hasa kuweka chaji na malipo kabla ya kutumia kuongea au mtandao
- ✔ Mtandao kupotosha kimaadili
- ✔ Hutoa miale ambayo yaweza kusababisha saratani
- ✔ Kudanganya katika mitihani
- ✔ Kufungwa jela kutokana na arafa za vitisho na matusi

**Runinga/magazeti**

- ✔ Burudani
- ✔ Habari
- ✔ Ajira kwa wanahabari na watangazaji
- ✔ Matangazo ya biashara
- ✔ Kufunza maadili k.m. michezo ya kuigiza na vichekesho.
- ✔ Kutuwezesha kufahamu sehemu nyingine za nchi na dunia
- ✔ Kuelimisha k.v. vipindi vya fasihi
- ✔ Utalii
- ✔ Kuangazia sehemu na watu wenye shida
- ✔ Kukuza lugha
- ✔ Kukuza uzaleno

**Madhara**

- ✔ Ajizi

- ✔ Kupotosha kimaadili
- ✔ Filamu ziazohimiza watu kuwa wazinifu.
- ✔ Matangazo ya vileo
- ✔ Kuenezea chuki na propaganda
- ✔ Kuiga utamaduni wa kigeni usiofaa k.v. mavazi, talaka
- ✔ Gharama ya kununulia
- ✔ Kutopata muda wa kushauri watoto na kuomba
- ✔ Wanafunzi kutosoma jioni
- ✔ Mke na mume kutoongea kujadili mwelekeo wa familia
- ✔ Wanaume kuchelewa kurudi nyumbani usiku wakitazama mpira
- ✔ Migogoro kwa kutaka kutazama vipindi tofauti
- ✔ Kelele na usumbufu kwa waliolala

**Utalii**

hali ya kusafiri mbali ili kuvinjari au kufurahia mandhari

**Faida**

- ✔ Fedha za kigeni
- ✔ Ajira katika hoteli, udereva, n.k.
- ✔ Uhifadhi wa mazingira
- ✔ Kuboreshwa kwa miundo msingi
- ✔ Mapato kwa serikali kutokana na ada ya kuingilia mbugani na kodi za mikahawa
- ✔ Amani na maelewano nchini na duniani
- ✔ Kuhifadhi mila na tamaduni zetu
- ✔ Kupa nchi umaarufu duniani
- ✔ Maeneneo kame kuweza kutumiwa ipasavyo kama kivutio chao
- ✔ Soko kwa mazao ya kilimo
- ✔ Kuwapa wauzaji vinyago mapato

**Ubaya**

- ✔ Magonjwa k.v. ya zinaa
- ✔ Matumizi ya mihandarati
- ✔ Tabia zisizofaa k.v. Usenge zinazovunja ndoa na kueneza magonjwa kama ukimwi
- ✔ Upuuzaji wa miradi ya maendeleo serikali ikijengea watalii hoteli za kifahari na viwanja vya ndege ambavyo hutumika kwa nadra sana

- ✔ Kusababisha watoto kuacha shule ili wawe wanawaelekeza wapate pesa
- ✔ Kuhimiza mauaji wa wanyama kwa kununua pembe na ngozi
- ✔ Kelele za magari yao husumbua wanyama na kukanyaga na kuharibu lishe yao

**Jinsi ya kuvutia watalii zaidi**

- ✔ Kudumisha usalama
- ✔ Kuimarisha miundo msingi
- ✔ Kutangaza nchi na vivutio nje
- ✔ Kupunguza malipo katika hoteli za watalii
- ✔ Kufahamisha wananchi kuhusu vivutio kupitia vyombo vya habari
- ✔ Kuongezea wafanyakazi mishahara ili kuweka akiba waweze kuzuru maeneo yenye vivutio
- ✔ Kuwapa wafanyakazi likizo ya kutosha

**Umaskini**

**Suluhisho**

- ✔ Kuongeza nafasi za ajira
- ✔ Kutoa mikopo rahisi kulipa
- ✔ Kupunguza bei ya pembejeo
- ✔ Elimu ya bure
- ✔ Kupigana na ufisadi
- ✔ Upangaji uzazi ili kupunguza idadi ya watu
- ✔ Bei bora ya mazao ya kilimo
- ✔ Kazi kwa vijana

**Ukeketaji**

**Sababu**

- ✔ Kupunguza tamaa
- ✔ Njia ya kukomaa
- ✔ Mila na tamaduni

**Madhara**

- ✔ Kifo kwa kutokwa na damu sana
- ✔ Uenezaji wa magonjwa
- ✔ Shida wakati wa hedhi na kujifungua
- ✔ Ndoa kuvunjika
- ✔ Kibali cha kujiingiza katika myenendo isiyofaa
- ✔ Utengano kati ya waliotahiriwa na ambao hawajatahiriwa -migogoro

- ✔ Kuzua utabaka baina ya waliopashwa na wasiopashwa tohara

**Suluhisho**

- ✔ Hatua za kisheria
- ✔ Elimu kuhusu madhara
- ✔ Mawaidha kwa wasichana
- ✔ Makao ya watoto

**Njaa**

- ✔ Kilimo cha unyunyizaji maji
- ✔ Kupunguza bei za pembejeo
- ✔ Njia bora za kuhifadhi mazao
- ✔ Mimea na mifugo inayokomaa haraka
- ✔ Utumizi wa samadi na mbolea
- ✔ Kuelimisha wakulima kuhusu kilimo bora
- ✔ Kutayarisha mashamba mapema
- ✔ Serikali kununua mazao ya wakulima na kuyahifadhi

**Dini**

**Uzuri**

- ✔ Kufunza maadili
- ✔ Kusaidia maskini
- ✔ Kuanzisha shule na hospitali
- ✔ Ajira kwa padri, kasisi n.k.
- ✔ Kuandaa watu kwa maisha baada ya kifo
- ✔ Kufariji/kuliwaza wenye dhiki

**Ubaya**

- ✔ Tamaa ya pesa
- ✔ Biashara
- ✔ Ubakaji wa watoto
- ✔ Kuuza uponyaji
- ✔ Nyingine kutosaidia wenye shida
- ✔ Vita/jihadi
- ✔ Kuruhusu waovu bora watoe pesa
- ✔ Kutoenda hospitalini
- ✔ Kuendeleza maovu k.v. uzinifu, ushirikina, uabudu shetani, n.k.

**Maasi ya vijana**

- ✔ dawa za kulevya
- ✔ shiniko la kikundi
- ✔ filamu mbaya
- ✔ kudhibitiwa kupita kiasi
- ✔ kukosa nidhamu
- ✔ malezi mabaya/udekezaji
- ✔ kubomoka kwa msingi wa jamii
- ✔ Ufukara kusababisha kujiunga na makundi haramu
- ✔ Kukata tamaa
- ✔ Kutumiwa vibaya na wanasiasa

**Suluhisho**

- ✔ Kujiondoa kundini
- ✔ Kuimarisha uchumi
- ✔ Kuwashauri vijana
- ✔ Kujenga udhabiti wa jamii
- ✔ Kuwaadhibu kulingana na makosa yao
- ✔ Vijana kujisaka na kujikosoa
- ✔ Vijana kumjua mungu
- ✔ Uhuru wa kadiri
- ✔ Uongozi bora
- ✔ Malezi bora
- ✔ Kuongeza nafasi za ajira

**Umoja na Utangamano katika Familia**

- ✔ Kuheshimiana
- ✔ Utiifu na unyenyekevu
- ✔ Kuwa na usemi
- ✔ Kuvumiliana na  kusameheana
- ✔ Uaminifu na kuaminiana
- ✔ Kutochagulia watoto taaluma na wachumba
- ✔ Wazazi kutolazimisha watoto taaluma au kozi wasizotaka
- ✔ Kutumia pesa vyema bila ubadhirifu
- ✔ Kutopendelea na kulinganisha watoto kiuwezo
- ✔ kutotumia dawa za kulevya
- ✔ Kuomba pamoja
- ✔ wazazi kutopendelea watoto fulani
- ✔ Baba kutimiza majukumu yake ya kukimu jamii

- ✔ Kutodhibiti mke na watoto kupita kiasi
- ✔ Uadilifu
- ✔ Kushiriki kazi

**Mambo yanayoathiri utaifa/umoja na utangamano/amani**

- ✔ Ufisadi k.v. kuajiri watu kimapendeleo
- ✔ Ukabila
- ✔ Viongozi kueneza chuki
- ✔ serikali kutoakisi uwakilishaji wa taifa zima
- ✔ Usalama kukosekana
- ✔ Ukosefu wa ajira
- ✔ Matamshi mabaya ya viongozi
- ✔ Kupanda kwa gharama ya maisha
- ✔ Majanga ya kiasili
- ✔ Kutojenga miundo msingi kwa usawa
- ✔ Kupendelea maeneo fulani katika ugawaji wa raslimali
- ✔ Ukimbizi wa ndani kwa ndani
- ✔ Ubomoaji wa nyumba

**Suluhisho**

- ✔ Lugha ya taifa
- ✔ Kukabiliana na ufisadi
- ✔ Usawa katika ugawaji wa raslimali
- ✔ Kuelimisha kuhusu umoja wa kitaifa
- ✔ Tamasha za kitamaduni
- ✔ Kutalii sehemu nyingine za nchi
- ✔ Ndoa za makabila tofauti
- ✔ Serikali ya muungano
- ✔ Viongozi wachochezi kuchukuliwa hatua kisheria

**Matatu**

**Faida**

- ✔ Kurahisisha na kuharakisha usafiri
- ✔ Ajira
- ✔ Ushuru
- ✔ Biashara
- ✔ Huduma za dharura

**Madhara**

- ✔ Ajali
- ✔ Wizi
- ✔ Ufisadi wa polisi kuongezeka
- ✔ Kuongeza nauli ghafla
- ✔ Ujeuri wa madereva na mataniboi
- ✔ Kuchelewesha watu njiani

**Magazeti**

- ✔ Habari za taifa na kimataifa
- ✔ Kuelimisha k.m. kuhusu afya
- ✔ Kuburudisha k.m. vibonzo
- ✔ Matangazo ya biashara
- ✔ Ajira k.m. wahariri, wauzaji
- ✔ Mapato kwa serikali
- ✔ Kutangaza nafasi za ajira
- ✔ Elimu k.m. uchambuzi wa vitabu vya fasihi na mashairi
- ✔ Hutumiwa kufungia bidhaa

**Ubakaji**

- ✔ Sura mbaya
- ✔ ulevi
- ✔ Ulemavu
- ✔ Unyonge wa kiakili
- ✔ Kushindwa kudhibiti jicho na tamaa za mwili
- ✔ Njaa ya kimapenzi
- ✔ Kisasi
- ✔ Kujihisi duni
- ✔ Kisomo duni
- ✔ Mavazi

**Athari**

- ✔ Waliobakwa huathirika kisaikolojia
- ✔ Kujikosea heshima na kujihisi mchafu
- ✔ Magonjwa ya zinaa
- ✔ Mimba zisizotakikana
- ✔ Vifo
- ✔ kujeruhiwa
- ✔ Kupoteza imani na wanaume/wanawake
- ✔ Kutengwa

✔ Kufungwa jela

**3. UTUNGAJI WA KISANII**

a) Mashairi mepesi (huru/arudhi)
b) Hadithi fupi
c) Vitendawili
d) Mafumbo/chemshabongo
e) Vitanza ndimi
f) Michezo ya kuigiza

**Mambo ya Kuzingatia katika Uadishi wa Insha**

maagizo
Usijibu swali usilolielewa
Uandishi mzuri wa nambari ya swali unalofanya
Kuandika vidokezi
Kuandika kila hoja katika aya yake
Kuanzia aya kwa njia tofauti
Lugha sahili
Miundo tofauti ya sentensi
maudhui
muundo
Kichwa kwa herufi kubwa, kipigwe mstari na kisizidishe maneni sita
Upatanisho/uwiano za kisarufi
Tahajia/hijai
Kuakifisha
Mtiririko
Uhalisi
tafsiri ya moja kwa moja k.m. kurudisha mlango, mguu wa gari, kutoa/kuweka nguo
Maadili (lugha na mawazo safi na mtazamo wa kusaidia taifa)
Urefu
Uasilia (utungo wako si kurejelea vitabu vya fasihi)
Usafi (mwandiko unaosomeka na ambao haujapigwapigwa mistari na kufutwa)
Tamathali za usemi
Msamiati na tamathali zinazokubalika wala si za kupachika. Usitumie msamiati wa kishairi k.v. mtima, ja, n.k.
Kutofupisha k.v. k.m., n.k., Bi.

Kutumia kistari ikiwa neno linaendelea katika mstari wa pili na kutokata silabi
Herufi f, u, i, j, m, l
Kutaja na kueleza kikamilifu
Kukamilisha maneno
Kutotenganisha sehemu za neno k.m. walilo zungumzia, walioenda
Kutounganisha maneno k.m. kwasababu, ni mimi
Mdokezo kuoana na maneno yako.
Usiongeze maneno kwenye dondoo la kumalizia.
Kutoweka dondoo ni kupotoka
Kusoma insha baada ya kuandika

**4. UANDISHI WAKAWAIDA**

**Ufahamu**

Kuelewa
Kuandika idadi ya hoja kulingana na alama
Hoja kwa muhtasari
Andika hoja ulizo na uhakika nazo kwanza
Kuorodhesha hoja kwa nambari wala si kistari
Jibu lililokamilika
Kutoa majibu kutoka katika ufahamu si fikra zako
Maana za maneno kama yalivyotumiwa kwa muundo ule ule

**Muhtasari/Ufupisho**

Kutoa mawazo makuu huku kiini cha taarifa kikidumishwa.

**Hatua**

✔ Andika nambari za aya
✔ Soma makala
✔ Elewa swali
✔ Andika mambo muhimu ukizingatia swali ukiondoa maneno yasiyo muhimu
✔ Usibadilishe chochote hata kama unatakiwa kutumia maneno yako
✔ Andika hoja kikamilifu
✔ Andika nakala safi ukizingatia mtiririko
✔ Epuka viunganishi vingi
✔ Zingatia idadi ya maneno uliyopewa
✔ Zingatia kanuni za uandishi
✔ Piga mshazari nakala chafu

**Matumizi ya lugha**

- ✔ Kuzingatia sehemu za swali
- ✔ Sehemu zinazobadilika
- ✔ Kuzingatia neno moja moja
- ✔ Kuzingatia hatua au mbinu
- ✔ Kutojibu maswali kwa pupa
- ✔ Kusoma jibu ili kusahihisha makosa
- ✔ Kuelewa swali k.m. tunga sentensi moja, eleza maana
- ✔ Tunga sentensi fupi
- ✔ Kuonyesha neno, fungu la maneno au kiambishi unachotumia kutunga sentensi
- ✔ Kubainisha (eleza kikamilifu kwa kuandika neno au maneno na jina lake)
- ✔ Tahajia k.m. yabwa, kitendo

**Isimu jamii**

- ✔ Kutaja, kueleza na kutoa mifano

**Fasihi**

- ✔ Kufikiri ili kuelewa swali
- ✔ Usijibu maswali zaidi ya manne. Kama jibu halikuridhishi, lipige mshazari
- ✔ Maagizo (swali la kwanza ni la lazima, usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- ✔ Chagua maswali utakayoweza kujibu na kupata hoja nyingi
- ✔ Andika nambari vizuri
- ✔ Usiandike hoja nyingi kuliko alama
- ✔ Andika hoja ulizo na uhakika nazo kwanza
- ✔ Hoja kwa aya moja
- ✔ Kutaja, kueleza kikamilifu na kuthibitisha kwa mifano kutoka kitabuni (kutaja alama moja, kueleza mbili)
- ✔ Usirudie hoja kwa njia tofauti
- ✔ Kutochanganya wahusika
- ✔ Kusoma vitabu mara nyingi ili kujua dondoo limetolewa wapi
- ✔ Maswali ya dondoo (msemaji, anayeambiwa, wapi, lini)
- ✔ Maswali ya kujadili
- ✔ Swali la methali
- ✔ kulinganisha

# FASIHI SIMULIZI 1

**Fasihi** ni sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu.

**Sanaa** ni ufundi wa kuwasilisha fikra na hisia za binadamu kama vile maneno, maandishi, uchoraji, uchongaji, ufinyanzi n.k.

**Fasihi simulizi ni sanaa kwa vile:**

a) Huwasilisha ujumbe kuhusu binadamu kuhusu utamaduni na uchumi.
b) Huwa na umbo mahsusi k.m. hadithi huwa na mwanzo, kati na mwisho na mashairi huwa na beti, mishororo, n.k.
c) Hutumia lugha kwa ufundi k.v. ya kitamathali.
d) Husawiri mandhari/mazingira mahsusi kwa ufundi mkubwa.
e) Hujenga wahusika kwa ustadi mkuu ili kusawiri tabia za watu katika jamii.

**Tofauti Kati ya Fasihi na Sanaa Nyingine**

| fasihi | sanaa nyingine |
|---|---|
| Kutumia lugha | Kutotumia lugha |
| Sanaa tendi | Si tendi |
| Kutumia wahusika kuwasilisha maudhui | Hutumia maumbo kumithilisha watu |
| Kutumia maudhui na fani kuwasilisha ujumbe | Kutumia maumbo na sura za vitu |
| Kujikita katika mazingira na wakati maalum | Hazijikiti katika muktadha na wakati maalum. |

**Aina/makundi ya fasihi**

a) **Fasihi simulizi**
⇒ Fasihi inayowasiolishwa kwa njia ya mdomo.
b) **Fasihi andishi**
⇒ Fasihi inayowasilishwa kwa njia ya maandishi.

**Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi/sifa za fasihi simulizi/zinazofanya utanzu uwe wa fasihi simulizi**

**a)** Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo ilhali fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.

**b)** Fasihi simulizi huhifadhiwa akilini ilhali fasihi aandishi huhifadhiwa kwa maandishi.

**c)** Fasihi simulizi ni mali ya jamii ilhali fasihi andishi ni mali ya mtu binafsi/mwandishi.

**d)** Fasihi simulizi ina wahusika wa kila aina k.v binadamu, wanyama na ndege, mazimwi na majitu, miungu, mizimu, mashetani na vitu visivyo na uhai k.v. mawe na miti ilhali fasihi andishi ina wahusika binadamu kwa kiasi kikubwa.

**e)** Fasihi simulizi ina tanzu nyingi kuliko fasihi andishi.

**f)** Uwasilishaji wa fasihi simulizi huweza kuandamana na utendaji k.v matumizi ya ishara, nyimbo, makofi, kuimba, kubeba zana katika majigambo n.k ilhali ule wa fasihi andishi hauandamani na utendaji isipokuwa inapowasilishwa mbele ya hadhira.

**g)** Fasihi simulizi huwasilishwa mbele ya hadhira ilhali fasihi andishi si lazima iwasilishwe mbele ya hadhira.

**h)** Fasihi simulizi huwasilishwa mahali maalum k.v jandoni, matangani, arusini, n.k ilhali fasihi andishi haina mahali maalum.

**i)** Fasihi simulizi huandamana na shughuli fulani ya kitamaduni ilhali fasihi andishi haiandamani na shughuli ya kitamaduni.

**j)** Fasihi andishi huhitaji muda kutunga ilhali baadhi ya fasihi simulizi huzuka papo hapo k.m. semi, maigambo.

**k)** Fasihi simulizi ina uwezo mkubwa wa kubadilishwa na fanani anapowasilisha ufaraguzi) bali fasihi andishi haibadiliki isipokuwa mwandishi aiandike upya.

l) Fasihi simulizi ina historia ndefu kuliko fasihi andishi kwa kuwepo tangu mwanzo wa maisha ya binadamu

m) Fasihi simulizi huwasilishwa wakati maalum k.v. usiku, kipindi fulani cha mwaka ilhali andishi haina wakati maalum.

- **Tofauti kati ya hadhira**

**n)** Hadhira ya fasihi simulizi huweza kuwasiliana moja kwa moja na mwasilishaji ilhali ile ya fasihi simulizi sio lazima iwasiliane na mwandishi.

**o)** Hadhira huchangia katika uwasilishaji wa fasihi simulizi k.v kwa kuimba, kupiga makofi n.k (hadhira tendi/hai) ilhali hadhira ya fasihi andishi haichangii katika uandishi.

**p)** Hadhira ya fasihi simulizi huonana na mwasilishaji ilhali ile ya fasihi andishi si lazima ionane na mwandishi.

**q)** Hadhira ya fasihi simulizi ni kubwa kuliko ile ya fasihi andishi kwani huhusisha hata wasiojua kusoma na kuandika.

**r)** Hadhira ya fasihi simulizi ni hai yaani inajulikana na fanani ilhali ile ya fasihi simulizi si hai yaani haijulikani na mwandishi.

**s)** Hadhira ya fasihi simulizi hainunui kazi ilhali ile ya fasihi andishi hununua kazi.

**t)** Hadhira ya fasihi simulizi yaweza kumiliki kazi ya fanani lakini ile ya fasihi andishi haiwezi kumiliki kazi ya mwandishi.

**u)** Hadhira ya fasihi simulizi huchagua kwa kulenga watu wa rika fulani lakini ile ya fasihi andishi hailengi watu wa rika yoyote.

**Jinsi Fasihi Simulizi na Andishi Zinavyofanana**

a) Zote mbili hushughulikia masuala yanayohusu maisha maisha ya binadamu.
b) Zote mbili Huhumia lugha kwa ubunifu kuwasilisha maudhui.
c) Zote mbili huwa na vipengele viwili vikuu, maudhui na fani (jumla ya mbinu msanii alizotumia kuwasilisha maudhui).
d) Zote mbili majukumu sawa k.v. kuburudisha, kuadilisha, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, n.k.
e) Zote mbili zina utendaji-pale tamthilia na riwaya zinapoigizwa.
**f)** Zote mbili huzaliwa, hukua na hufa kutegemea mabadiliko ya wakati.
**g)** Zote mbili huwa na wawasilishaji-fanani k.m. mtambaji/mganaji au manju/yeli katika fasihi simulizi na mwandishi upande wa fasihi andishi
h) Fasihi simulizi imekopa tanzu za fasihi simulizi k.v. methali, mashairi, n.k.

**Majukumu ya Fasihi Simulizi/Umuhimu wa Kufunza Fasihi Simulizi Katika Shule za Upili**

a) Kuburudisha-kustarehesha, kufurahisha, kuchangamsha, kutuliza, kusisimua na kupumbaza akili na kiwiliwili - nyimbo, hadithi, vitendawili
b) Kufunza maadili kwa wanajamii kwa kuwahimiza kuiga sifa chanya na kukataa sifa hasi za wahusika.
c) Kukuza uwezo wa kufikiri/kudadisi k.m vitendawili na chemshabongo.
d) Kufariji k.m mbolezi na methali k.m. ‘Baada ya dhiki faraja’.
e) Vipengele vya fasihi simulizi k.v mashairi, nyimbo, nahau, hutumiwa katika uandishi wa fasihi andishi.
f) Kuhifadhi historia ya jamii k.m. mighani, visaviini, mapisi, tarihi n.k.
g) Kukejeli tabia zinazokiuka matarajio ya jamii k.v soga, methali, n.k.
h) Kuendeleza tamaduni za jamii kwani husawiri imani na desturi za jamii. k.v kitendawili ‘Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini siwezi kulichuma.’ - Mtu hawezi kumwoa dadake.
i) Kuunganisha watu pamoja kwa kuwajumuisha pamoja wakati wa ngoma, kuimba, utambaji, n.k.

j) Kukuza lugha k.v. misimu inapokita kimatumizi na kujumuishwa katika lugha sanifu.
k) Kukuza uwezo wa kutumia lugha kadiri mtu anapoendelea kuwasilisha k.v. hotuba, vitanza ndimi husaidia kuboresha matamshi na kutofautisha maana za maneno.
l) Kuza uwezo wa kubuni k.v. malumano ya utani, vitanza, ndimi ngonjera, n.k.
m) Kukuza uzalendo kwa kufanya wanajamii kuonea fahari jamii zao na kuiga mashujaa au watu waliotendea jamii makuu.
n) Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, n.k.

**Sababu za Ufaraguzi/Kubadilika kwa Fasihi Simulizi**

**a)** Kuwasilishwa vibaya.
**b)** Fanani kusahau na kubadilisha yaliyomo na mtiririko.
**c)** Kubadilisha ili kukidhi mahitaji ya hadhira k.m. umri na uelewa wao- kutumia lugha nyepesi kwa watoto na pevu kwa watu wazima.
**d)** Mabadiliko ya mandhari/mazingira-vitu vilivyo katika mazingira halisi kukosekana katika mazingira ya usimulizi na msimulizi kutumia vitu katika mazingira yake vinavyokaribiana navyo.
**e)** Kutoeleweka na hivyo kuhifadhiwa vibaya.
**f)** Mabadiliko ya wakati k.m kitendawili cha wakati wa mkoloni kutumia mzungu na cha wakati wa mwarabu kutumia mwarabu na maana ni ile ile-Mzungu/mwarabu amesimama kwa mguu mmoja-mwavuli.
g) Mabadiliko ya falsafa ya vizazi na maingiliano katika jamii kusababisha kurithisha tu yale ambayo ni muhimu na kuacha mengine.
h) Kila fanani huwa na mtindo wake wa kuwasilisha/kisanii.
i) Ubunifu wa fanani ili uwasilishaji uweze kuvutia saidi na uwezo wake wa lugha.
j) Teknolojia kusababisha kuhifadhiwa na hivyo kuiua.

**Wahusika katika Fasihi Simulizi**

⇒ Wahusika ni viumbe wa sanaa ambao hutumiwa katika kazi ya fasihi kuwasilisha maswala mbalimbali.
a) Fanani-anayetunga na kuwasilisha fasihi simulizi.
b) Hadhira-kusikiliza, kutazama, kushiriki wa kuimba, kuuliza maswali, kutegua vitendawili, kupiga makofi, n.k. kuna aina mbili za hadhira: (i) hadhira tendi/hai na (ii) hadhira tuli.
c) Wanyama-wanaofanya kama binadamu na kuwakilisha sifa kama vile ujanja, ulaghai, tamaa na ujinga na wanaobakia wanyama tu.

d) Binadamu
e) Mazimwi na majitu-viumbe vyenye matendo na maumbile ya kutisha kama vile jicho moja, vichwa viwili au zaidi, nusu mtu na nusu myama, wenye tamaa iliyokithiri ya kuweza kumeza kila kitu, kuhifadhi na kutunza binadamu ananyoyapendeza.
f) Wahusika vitu (visivyo na uhai) mawe, miti, vijaluba, vibuyu-hutumiwa kuibua imani za kidini.
g) Mizimu-roho za waliokufa-hutembea, hula na huathiri binadamu.
h) Miungu-viumbe vyenye uwezo mkubwa dhidi ya binadamu k.m. katika mighani na visasili.

**Njia za Kukusanya Fasihi Simulizi**

**a) Kuchunza/utazamaji**

⇒ Kutazama kwa makini yanayotokea na kuandika.

**Umuhimu/ubora/uzuri**

a) Kupata habari za kutegemewa na kuaminika.
b) Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
c) Ni njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika
d) Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
e) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji

**Udhaifu**

a) Shida ya mawasiliano.
b) Ugeni wa mtafiti kusababisha washiriki kumshuku na kusitisha uwasilishaji
c) Ghali kwa kumbidi mtafiti kusafiri
d) huhitaji muda mrefu

**b) Kusikiliza wasanii wakiwasilisha tungo zao.**

**Umuhimu**

a) Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
b) Kupata habari za kutegemewa na kuaminika.
c) Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
d) Kikwazo cha mawasiliano-Si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
e) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji.

**Udhaifu**

a) Shida ya mawasiliano-Si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
b) Huhitaji muda mrefu-kusafiri na kusikiliza.
c) Ugeni wa mtafiti kusababisha washiriki kutowasilisha ipasavyo.

d) Ghali kwa gharama ya usafiri.

**c) Mahojiano**

⇒ Kuhoji wanaofahamu mengi kuhusu fasihi simulizi.

**Umuhimu**

a) Kuweza kung’amua wakati mhojiwa anatoa habari zisizo za kweli.
b) Kuweza kufafanulia mhojiwa maswali ili kuweza kupata habari sahihi zaidi.
c) Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
d) Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
e) Kupata habari za kutegewa na kuaminika

**Udhaifu**

a) Huhitaji muda mrefu.
b) Mhojiwa kutotoa habari kwa kutomwamini mtafiti kwa ugeni wake.
c) Kikwazo cha mawasiliano-si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
d) Ghali kwa gharama ya usafiri.

**d) Kurekodi katika kanda za sauti/tepurekoda**

**Umuhimu**

a) Kuweza kudumu na kufikia vizazi vingi.
b) Sifa za uwasilishaji/uhai kama vile toni na kiimbo kuhifadhiwa.
**c)** Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa.
d) Kupata habari za kutegewa na kuaminika
e) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji

**Udhaifu**

a) Chaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
b) Hakiwezi kunasa uigizaji.
c) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
d) Ghali kwa kuhitaji kununua kifaa na kumbidi mtafiti kusafiri.

**e) Kurekodi kwa filamu na video**

⇒ Hunasa picha zenye miondoko na sauti.

**Umuhimu**

a) Video huhifadhi uigizaji, ishara na kiimbo/toni.
b) Kuonyesha uhalisi wa mandhari
c) Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa
**d)** Kazi iliyokusanywa hivi hudumu kwa muda mrefu.
e) Njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika
f) Kupata habari za kutegewa na kuaminika

**Udhaifu**

a) Chombo chaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
b) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
c) Njia ghali.
d) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
e) Ghali kwa gharama ya ya usafiri na kununua filamu na kamera ya video.
f) Data yaweza kufisidiwa na hivyo kutowafikia walengwa.

**f) Kupiga picha kwa kamera**

⇒ Hunasa picha zisizo na miondoko na sauti

**Umuhimu**

a) Huonyesha uhalisi wa mandhari.
b) Huweza kuhifadhi ishara.
c) Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa.
d) Kupata habari za kuaminiwa na kutegemeka.

**Udhaifu**

a) Ghali kwa gharama ya ya usafiri na kununua kamera.
b) Sifa za uhai kama vile kiimbo haziwezi kuhifadhiwa.
c) Yaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
d) Data yaweza kufisidiwa na hivyo kutowafikia walengwa

**f) Kushiriki katika kazi ya fasihi simulizi k.v. ngoma, soga, n.k.**

**Umuhimu**

a) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji.
b) Kupata habari za kutegewa na kuaminika.
c) Njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
d) Kukuza utangamano wa mtafiti na wanajamii.
e) Kuweza kunasa na kuhifadhi sifa za kiimbo, toni na ishara.

**Udhaifu**

a) Kuchukua muda mrefu.
b) Ugeni wa msanii kusababisha washiriki kuwa na wasiwasi na kutotenda kama kawaida.
c) Njia ghali kwa kuhitaji mtafiti kusafiri mbali.
d) Mtafiti aweza kusahau kwa kuhifadhi akilini.

**g) Kutumia hojaji**

⇒ Fomu yenye maswali funge au wazi.

**Umuhimu**

a) Gharama ya chini.
b) Yaweza kutumika katika mahojiano.
c) Huokoa muda kwani mtafiti aweza kuituma na kuachia mhojiwa kujaza.
d) Hupatia habari za kuaminika na kutegemeka.

**Udhaifu**

a) Utata wa maswali kusababisha majibu yasiyo sahihi.
b) Si nzuri kwa wasiojua kusoma na kuandika.
c) Kutopata sifa za uwasilishaji kama vile kiimbo, toni na ishara.
d) Wahojiwa kukataa kuijaza kutokana na mwelekeo hasi dhidhi ya hojaji na hivyo kukwamiza utafiti.

**Vifaa vya Kukusanya Fasihi Simulizi na Udhaifu Wake**

a) Vinasa sauti/tepu rekoda
b) Kamera
c) Filamu na video
d) Diski za kompyuta
e) Kalamu na karatasi

**Umuhimu**

a) Kuweza kudumu na kufikia vizazi vingi.
b) Si rahisi kusahaulika-hubakia vile vile.
c) Si njia ghali kama vile video

**Udhaifu**

a) Sifa za uwasilishaji kama vile toni, kiimbo/toni na ishara haziwezi kuhifadhika hivyo kupotea.
b) Hupunguza hadhira kwa kulenga tu wanaojua kusoma na kuandika na hivyo kuathiri usambazaji wake.

**Mbinu za Kuhifadhi Fasihi Simulizi**

a) Huhifadhiwa na binadamu akilini k.m. ngano hupokewa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
b) Katika maumbile au mazingira k.m. fisi daima huchechemea , kinyonga naye hutembea pole pole.
c) Katika vifaa meme k.m. nyimbo, hadithi, maigizo n.k. huweza kuhifadhiwa katika kanda za sauti, video, sidi na diski za kompyuta.

d) Katika michoro k.m. picha huhifadhi matukio maalum k.v. za kabila fulani likiwinda au likisherehekea.

**Umuhimu wa Kukusanya/Kuhifadhi Fasihi Simulizi**

**a)** Ili isipotee k.m. kwa kusahaulika.
**b)** Kuirekodi ili kuiendeleza kwa kuirithisha kwa vizazi vijavyo.
**c)** Ili kulinganisha fasihi simulizi za jamii mbalimbali na kuonyesha tofauti zake.
**d)** Ili kuhakikisha mtiririko katika uwasilishaji.
**e)** Kutunza historia ya jamii ili vizazi vijavyo viijue.
**f)** Ili kuziba mapengo ya utafiti yaliyomo kwa vile kuna tungo ambazo hazijatafitiwa kwa kina.
**g)** Kuendeleza elimu ya jadi ya jamii.
**h)** Kuingiliana na jamii iliyo chanzo cha fasihi humwezesha kuelewa na utamaduni na fasihi yake kwa ujumla
**i)** Humwezesha mwanafunzi kuona vipengele hai vya fasihi k.v. uigizaji, toni na kiimbo ambavyo husaidia kuielewa kwa kina.
**j)** Husaidia kuhifadhi tamaduni za jamii kwa nia ya kuzipitisha kwa vizazi vijavyo.
**k)** Husaidia kuelewa utamaduni wa jamii nyingine.
**l)** Humwezesha mwanafunzi kupata maarifa ya kufanya utafiti katika taaluma nyingine k.v. sosholojia.
**m)** Kujua fasihi simulizi za jamii nyingine humfanya mtafiti kuzielewa na kuzikubali jamii hizo na hivyo kuendeleza amani katika nchi.
**n)** Ili kusahihisha mawazo mapotovu kuhusu baadhi ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi.

**Matatizo Yanayomkabili Mkusanyaji wa Fasihi Simulizi**

a) Gharama ya utafiti kuwa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu k.v. kusafiria, kununulia vifaa.
b) Kutojaziwa hojaji kutokana na mtazamo hasi wa jamii dhidi ya ujazaji wake.
c) Wanajamii kukataa kutoa habari wakishuku mtafiti anawapeleleza au kwa kuona haya.
d) Wanajamii wengine kudai walipwe kabla ya kutoa habari na hivyo kukwamiza utafiti.
e) Mbinu nyingine k.v. hojaji huhitaji watu wanaojua kusoma na kuandika na ikiwa mhojiwa hajui utafiti utakwamizwa.
f) Uchache wa wazee na wataalamu wa fasihi simulizi kusababisha kukosekana au kupatikana kwa data isiyo ya kutegemewa.
g) Utawala kukataa kutoa idhini ya kufanya utafiti.

h) Kukosa ufadhili na utafiti kutofanywa kwa kutomudu gharama.
i) Muda wa utafiti kutotosha na hivyo kutopata habari za kutosha kuhusiana na mada yake.
j) Kikwazo cha mawasiliano ikiwa mtafiti na mhojiwa hawatumii lugha moja na mhojiwa hajui lugha nyingine na kumbidi mtafiti kukodi mkalimani na gharama kuongezeka.
k) Ukosefu wa vyombo vya usafiri kunakocheleweshа utafiti na kutomalizika katika muda uliopangwa.
l) Ukosefu wa usalama k.v. kuvamiwa kwa kushukiwa anapeleleza na kuibiwa vifaa.

**Changamoto Zinazokabili Ukusanyaji wa Fasihi Simulizi**

a) Ukosefu wa utafiti wa kutosha kwani kuna vipera ambavyo bado havijaandikwa.
b) Uchache wa wataalamu wa kutafitia na kuendeleza utafiti.
c) Watu kuhamia mijini na kuingiliana na wa jamii nyingine na kufanya uhifadhi na urithishaji wa fasihi kutowezekana.
d) Mtaala wa elimu kupuuza lugha ya kiasili inayotumiwa kuhifadhia na kurithisha fasihi simulizi na hivyo kukatiza ukuaji wake.
e) Fasihi simulizi kuhusishwa na ukale na hivyo kutoona haja ya kuirithisha na kuihifadhi.
f) Kuhifadhiwa kwa fasihi simulizi akilini kusababisha kusahaulika, kubadilika hata kufa kwake.

**Jinsi Jamii ya Sasa Inavyojaribu Kuhifadhi Fasihi Simulizi**

a) Tamasha za muziziki kunakokaririwa na kuimbwa mashairi.
b) Sherehe za arusi, jando, mazishi mawaida.
c) Utegaji na uteguaji wa vitendawili kupitia redio na runinga.
d) Sarakasi za wasanii huhifadhi kipera cha vichekesho.
e) Ngoma za kienyeji kama isukuti katika hafla za kisiasa na harusi.
f) Utambaji wa hadithi hasa katika sehemu za mashambani.

**Tanzu za Fasihi Simulizi**

⇒ Tanzu ni aina za tungo zenye muundo uliokaribia kufanana.
e) hadithi
f) semi
g) ushairi
h) mazungumzo
i) maigizo

⇒ Kipera ni utungo wa fasihi simulizi unaowasilishwa mbele ya watu.

**HADITHI**

⇒ Masimulizi yanayotumia lugha ya mtiririko au nathari.

**Sifa**

**a)** Hutumia ya lugha ya mtiririko au nathari-kueleza matukio moja kwa moja.
b) Hurithishwa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
**c)** Huwasilishwa mbele ya hadhira
**d)** Hutambwa mahali maalum k.v. ndani ya nyumba, chini ya mti, uwanjani, n.k.
**e)** Huweza kutokana na matukio halisi (kihistoria) au ya kubuni.
**f)** Huwa na mafunzo fulani kwa jamii/hadhira.
**g)** Hutumia wahusika wa aina tofauti k.v. nyumbani, wanyama, ndege, mazimwi, n.k.
**h)** Hutumia aina nyingine za sanaa k.v nyimbo, methali, ushairi, n.k.
**i)** Huwa na utendaji k.v. mtambaji kuiga fisi anavyokula.
j) Aghalabu hutambwa jioni.

**Sababu za Ngano Kutambwa Jioni/Usiku**

a) Ndio wakati watu walikuwa wamejumuika nyumbani baada ya kazi.
b) Utambaji ulikuwa njia ya kupitisha wakati chakula kikingojewa.
c) Wakati huu ulihakikisha mwanajamii hapotezi wakati wa kazi.

**Majukumu ya Hadithi**

**a)** Kufunza maadili yaliyo nguzo kuu kwa wanajamii.
**b)** Kukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani.
**c)** Kuburudisha baada ya kazi ya kutwa.
**d)** Kukuza uwezo wa watoto wa kukumbuka ili kutamba baadaye.
**e)** Kueleza asili ya mambo k.m visaviini, visasili na ngano za usuli.
**f)** Kutahadharisha wanajamii dhidi ya kufanya mambo yasitofaa.
**g)** Kuunganisha watu katika jamii wanapojumuika pamoja kusikiliza utambaji.
**h)** Ngano za mtanziko hukuza uwezo wa kutathmini na kutoa uamuzi ufaao.
**i)** Kukuza lugha hasa kwa hadhira ya watoto.
**j)** Kuhifadhi na kuendeleza historia ya jamii k.v. mighani, tarihi, n.k.
**k)** Kuelimisha hadhira kuhusu utamaduni wao.
**l)** Njia ya kupokeza kizazi historia na utamaduni wa jamii.

**Sifa za Mtambaji/Mganaji Bora**

**1.** Asiwe mwoga ili kuweza kuzungumza hadharani.
**2.** Asiwe na haya ili kuweza kuzungumzia mambo ya aibu inapobidi.

**3.** Awe na uelewa wa mazingira na masuala ibuka katika jamii ili kuweza kuwasilisha dhana zisizopatikana katika mazingira yake k.m. kutumia rais kuelezea dhana ya mfalme.
**4.** Awe na ufahamu mpana wa lugha ili aweze kuitumia kwa uhodari na kuwasilisha kwa wepesi.
**5.** Awe mchanganfu na mcheshi ili kunasa makini ya hadhira na kuzuia isikinai.
**6.** Awe na ufahamu mpana wa utamaduni husika ili kuzuia kutumia maneno na ishara zinazoweza kuwaudhi au kupingana na imani za hadhira.
**7.** Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira k.v. kuimba, maswali ya balagha ili isikinai, n.k.
**8.** Aweze kujua, matarajio, kiwango cha elimu na tajriba ya hadhira ili kuweza kubadilisha kwa kiwango kinachofaa.
**9.** Awe na uwezo wa kuingiliana vizuri na hadhira ili aivutie.
**10.** Awe na kumbukumbu nzuri ili usimulizi wake utiririke vizuri.
**11.** Awe na uwezo wa kudramatisha ili kuonyesha picha fulani k.v. kuiga toni, sauti, na kiimbo kulingana na swala analowasilisha.
**12.** Kubadilisha toni au kiimbo ili hadhira isikinai.
13. Awe na ujuzi wa kutumia ishara za uso, mwili na miondoko kulingana na hali anayoigiza.
14. Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
15. Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v. huzuni
16. Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira kwa nyimbo na maswali ya balagha ili kuondoa uchovu wa kutazama na kusikiliza.
17. Awe na uwezo wa ufaraguzi/ kubadilisha utambaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika kutoka katika mazingira ya hadhira.
**18.** Awe na uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusisitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

**Aina za Hadithi**

**a) Hadithi za Kubuni**

⇒ Hazisimulii matukio ya kweli bali ya kutungwa

**b) Hadithi za Kisalua/Kihistoria**

⇒ Zinazosimulia matukio yaliyowahi kutendwa na wahusika waliowahi kuishi.
⇒ Huongezewa ubunifu ili kuvutia zaidi.

**1. Hadithi za Kubuni**

**Ngano**

⇒ Hadithi zinazosimulia kisa chenye funzo na zenye wahusika aina ya binadamu, viumbe na vitu visivyo na uhai.

**Sifa za Ngano**

**j)** Zina fomyula ya kuanzia/mwanzo maalum.
**k)** Zina fomyula ya kumalizia/mwisho maalum.
**l)** Zina wahusika aina mbalimbali.
**m)** Zina matumizi ya nyimbo.
**n)** Hutumia takriri (usambamba) ili kusisitiza k.m. zimwi likakimbia, likakimbia.
**o)** Huwa na na maadili/mafunzo
**p)** Hutumia maswali ya balagha kuongeza taharuki.
**q)** Hutumia tanakali za sauti.
**r)** Zina matumizi ya fantasia au matukio yanayokiuka uhalisi/mambo ya ajabu k.v. binadamu kuruka kama ndege, zimwi kumeza watu na baadaye kutapika wote, n.k.

⇒ Kutambua mbinu zilizotumiwa katika hadithi/ngano
⇒ Kutambua wahusika

**Aina za Fomyula za Kuanzia/Mianzo Maalum**

i) Paukwa, Pakawa. Sahani. Ya mchele. Giza. La mwizi. Na kiboko je? Cha mtoto mrorofi…
ii) Hapo zamani za kale/za kongamawe…
iii) Ilitokea…
iv) Hadithi! Hadithi! Hadithi njoo…
v) Kaondokea chenjangaa, kajenga nyumba kakaa, mwanangu mwanasiti, kijino kama chikichi, cha kujengea kikuta, na vilango vya kupita…
vi) Hapo jadi na jadudi…

**Umuhimu wa Fomyula ya Kuanzia/Mwanzo maalum**

i) Kuvuta makini ya hadhira.
ii) Kumtambulisha mtambaji kwa hadhira.
iii) Kuashiria mwanzo wa hadithi.
**iv)** Kutoa hadhira kutoka ulimwengu halisi hadi ule wa hadithi.

**Aina za Fomyula za Kumalizia/Miishio Maalum**

**ii)** Hadithi inaishia hapo.
**iii)** Tangu siku hiyo…
**iv)** Wakaishi raha mustarehe.

**v)** Maadili

**Umuhimu wa Fomyula ya Kumalizia/Mwisho Maalum**

i) Kuashiria mwisho wa hadithi.
ii) Kutoa hadhira katika ulimwengu wa hadithi hadi ule halisi.
iii) Kumpisha/kumpa fursa mtambaji anayefuata.
iv) Kupisha shughuli inayofuata.
v) Kutoa funzo la hadithi kwa muhtasari.
vi) Kupa hadhira nafasi ya kupumzika baada ya kuwa makini kwa muda.

**Umuhimu wa Nyimbo katika Ngano**

**i)** Kushirikisha hadhira.
**ii)** Kusisimua hadhira na kuondoa ukinaifu
**iii)** Kuteka makini yao.
**iv)** Kuwasilisha mafunzo/maadili.
**v)** Kutenganisha matukio katika hadithi.
**vi)** Kuburudisha hadhira.
**vii)** Kupunguzia hadhira mwemeo.

**Umuhimu wa Tanakali za Sauti/Onomatopeya katika Ngano**

**i)** Kuongeza utamu.
**ii)** Kusaidia msomaji kupata picha kamili.
**iii)** Kusaidia kupata hisia halisi

# AINA ZA NGANO

**i) Hurafa**

⇒ Hadithi zenye wahusika wanyama na ndege.
⇒ Hurafa za kijanja ni hadithi ambapo wanyama wadogo hutumia ujanja wa hali ya juu ili kujinasua na hali ngumu au mitego wanayotegewa.

**Sifa**

a) Wahusika ni wanyama au na au ndege.
b) Wanyama na ndege hupewa sifa za binadamu
c) Ni kazi ya ubunifu.
d) Hutoa mafunzo kwa njia ya kuchekesha na isiyoumiza.
e) Huwa na ucheshi mwingi.
f) Hutumia mbinu ya uhuishi.
g) Huwa na sifa zinazohimizwa na zinazoshutumiwa.
h) Ujanja au uongo hujitokeza katika hurafa za kijanja.

i) Ushindi hujitokeza katika hurafa za kijanja.
**Umuhimu**

a) Kutahadharisha watu dhidi ya kuwa wa danganyifu/kudanganyika kwa urahisi.
b) Kuonyesha jinsi tabia ya udanganyifu inavyoweza kujitokeza na kuathiri watu.
c) Hurafa za kijanja hufunza jinsi ya kupampana na hali ngumu.

**ii) Hekaya/Ngano za Kiayari**

⇒ Hadithi zinazomsawiri mhusika anayetumia ulaghai kupata matilaba yake kutoka kwa wengine (Abunuwasi).

**Sifa**

a) Wahusika wakuu ni binadamu.
b) Huwa na ubunifu mkubwa.
c) Hustaajabisha na kuchekesha.
d) Ujanja na uongo hujitokeza.
e) Ushindi hujitokeza.
f) Ni za kubuni.

**Umuhimu**

a) Hutahadharisha watu dhidi ya kuhadaika kwa wepesi.
b) Huonya dhidi ya matokeo yanayoweza kuwapata wanaojinyakulia mali kwa udanganyifu.
c) Kuonya dhidi ya usaliti.
d) Kukashifu viongozi dhalimu na matendo maovu.
e) Kukejeli wanaotumia nguvu badala ya akili/hekima.

iii) **Visasili**

⇒ Hadithi zinazoeleza asili ya matukio fulani katika jamii k.m. kifo, jua, lugha, zilizala n.k.

**Sifa**

a) Husimulia mambo ya kiimani na kidini.
b) Huwa na misingi ya kihistoria.
c) Hueleza asili ya matukio katika jamii.
d) Wahusika ni wanyama na binadamu.
e) Huwa na maadili.
f) Hurithishwa kizazi hadi kingine.

**Umuhimu**

a) Kueleza asili ya mambo kama vile kifo, utamaduni n.k.
b) Kueleza utaratibu wa kutekeleza desturi k.v. mahari.

c) Kuhalalisha baadhi ya mila na desturi za jamii k.v. ulipaji mahari, uabudu miti, n.k.
d) Kukitisha mizizi imani fulani ya watu.
e) Kupunguza athari za majanga kama vile kuhalalisha kifo.
f) Kutambulisha jamii kwani kila jamii ina aina yake ya visasili.
g) Kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii

**iv) Ngano za usuli**

⇒ Hadithi zinazoeleza asili ya hali, tabia, mahusiano au wasifu. k.v. asili ya kuku kuchakura, asili ya kinyonga kwenda kwa tahadhari, n.k.

**Sifa**

a) Wahusika ni wanyama na binadamu
b) Ni kazi ya kubuni.
c) Hueleza kuhusu asili ya sifa, tabia au hali.
d) Hutumia mbinu ya uhuishi.
e) Huwa na maadili.

**Umuhimu**

a) Kueleza sababu ya tabia, hali au sifa Fulani.
b) Kuonya dhidi ya tabia hasi kama vile ulafi.

**v) Ngano za mazimwi**

⇒ Hadithi ambazo wahusika ni mazimwi.

**Sifa**

a) Wahusika ni mazimwi
b) Mazimwi huwakilisha sifa hasi za binadamu k.m ulafi, ukatili, uovu n.k.
c) Hujaa uharibifu.
d) Huwa na matumizi mengi ya fantasia.
e) Kipengele cha safari hujitokeza k.v. kwenda nchi za mbali kutafuta suluhisho.
f) Ushindi hujitokeza (mazimwi hushindwa).
g) Ni kazi ya kubuni.
h) Huwa na maadili.
i) Mazimwi huwa na sifa zinazokiuka mipaka ya binadamu k.m. kinywa kisogoni, jicho moja kubwa, n.k.

**Umuhimu**

a) Kukashifu tabia ya uovu, ulafi, na ukatili.
b) Kutahadharisha dhidi ya kuwa na ulafi, ukatili n.k.

c) Kutia moyo waliodhulumiwa kuwa waliowanyanyasa wataadhibiwa siku moja.

**vi) Ngano za Mashujaa**

⇒ Ambazo zinazohusu watu waliotenda matendo ya kishujaa katika jamii zao kama vile kuokoa jamii.

**Sifa**

a) Kipengele cha motifu au kusafiri nchi za mbali, kupigana na mazimwi kuokoa jamii.
b) Husawiri mapigano kati ya wema (lila) na ubaya (fira).
c) Uovu huwakilishwa na mazimwi au viongozi dhalimu
d) Hatimaye wema hushinda uovu kwa juhudi za mashujaa

⇒ Ngano za mashujaa ni za kubuni ilhali katika mighani, mashujaa wanaaminiwa waliishi.

**Umuhimu**

a) Kuhimiza uzalendo na ujasiri miongoni mwa vijana.
b) Kuhimiza ujasiri miongoni mwa vijana.
c) Kusifu mashujaa katika jamii
d) Kuelimisha jamii kwa kuwapa maarifa ya kukabiliana na changamoto, inda na ila.
e) Kuhimiza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga mashujaa na kupigania jamii.
f) Kuonya dhidi ya matendo hasi k.v. ukatili.
g) Kuhimiza watu kutokata tamaa

**vii) Ngano za mtanziko**

⇒ Hadithi ambapo mhusika hukabiliwa hali ngumu ya kuamua baina ya mambo wawili au zaidi yanayomkabili.

**Sifa**

a) Wahusika ni wanyama au binadamu.
b) Ni kazi ya kubuni.
c) Mhusika hulazimika kufanya uteuzi mgumu.
d) Hali mbili au zaidi zinazotatanisha huwepo.

**Umuhimu**

a) Hutuerevusha jinsi ya kupambana na hali ngumu.
b) Kuonya/kutahadharisha dhidi ya kujiponza.

c) Kukuza uwezo wa kupima mambo na kuteua lililo muhimu.
d) Kuonya dhidi ya kutenda bila kuwaza kwa kina.

**viii) Ngano za Kimafumbo**

⇒ Ambazo huwa na maana ya ndani/iliyofichika.

**a) Istiara**

⇒ Hadithi ambayo maana yake huwakilisha maana nyingine iliyofichika k.v. hurafa ambapo wanyama huwakilisha binadamu.

**b) Mbazi**

⇒ Hadithi fupi inayotolewa inayotolewa kama mfano kumkanya au kumwelekeza mtu k.v. katika biblia.

**2. Hadithi za Kisalua/Kihistoria**

**i) Mighani**

⇒ Hadithi za mashujaa/majagina wa jamii fulani k.m. Rwanda Magere wa Waluo, Fumo Liyongo wa Wapate, Koome Njue wa Wameru, Wangu wa Makeri wa Wakikuyu na Syokimau wa Wsakamba.

**Sifa**

a) Huhusu mashujaa wa jamii fulani.
b) Wahusika hupambana na hali ngumu inayosababishwa na maadui.
c) Wahusika hupewa sifa na uwezo usiokuwa wa kawaida k.v. ukubwa wa ajabu, nguvu katika kivuli, nguvu katika nywele, kutoulika n.k.
d) Wahusika hupigania haki za wanyonge.
e) Mhusika hukomboa jamii yake dhidi ya maadui.
f) Mhusika hufa kifo cha huzuni (tanzia) kwa kusalitiwa na mtu wa karibu k.v. mwanamke au jamaa zao.
g) Mashujaa huuliwa kwa njia ya ajabu kama vile kunyolewa nywele, kivuli kuchomwa mkuki, kuchomwa shindano ya shaba kitovuni
h) Mighani huzungumzia matukio ya kihistoria.
i) Kuna tabia ya kupiga chuku matukio yaliyo hadithini.
j) Mighani hurithishwa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
k) Huchukuliwa na jamii kama hadithi zenye ukweli na jamii hujinasibisha na mighani hiyo.
g) Husimulia mambo ya kiimani na kidini.

**Umuhimu**

a) Kutambulisha jamii kwani kila jamii ina aina yake ya mighani.
b) Kuhifadhi na kumbusha historia yajamii.
c) Kusifu mashujaa katika jamii.
d) Kuhimiza ujasiri miongoni mwa vijana.
e) Kuelimisha jamii kwa kuwapa maarifa ya kukabiliana na adui au changamoto.
f) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga mashujaa na kupigania jamii.
g) Kuonya dhidi ya matendo hasi kama vile usaliti.
h) Kuhimiza watu kutokata tama.

**Tofauti Kati ya Mighani na Visasili**

| mighani | visasili |
| --- | --- |
| ⇛ Husimulia kuhusu mashujaa. | ⇛ Husimulia asili ya vitu. |
| ⇛ Husimulia historia ya jamii. | ⇛ Husimulia mianzo ya vitu au mambo. |
| ⇛ Wahusika wakuu ni majagina. | ⇛ Wahusika ni k.v. binadamu, miungu, wanyama, n.k. |
| ⇛ Hueleza sifa za majagina. | ⇛ Hueleza mianzo ya desturi. |

**ii) Visakale**

⇒ Masimulizi ya matukio yaliyotendeka zamani k.v. vita, majanga kama njaa na magonjwa na hamahama za jamii k.v. waisraeli kutoka misri.

**iii) Visaviini**

⇒ Hadithi zinazoeleza chimbuko la jamii Fulani

**iv)Mapisi**

⇒ Maelezo ya kihistoria yasiyo na ubunifu wowote k.v. chimbuko la kundi la wabantu kutoka Afrika ya Kati na kuenea sehemu mbalimbali za Afrika.

**v) Tarihi**

⇛ Maelezo kuhusu matukio ya kihistoria kulingana na yalivyofuatana ki wakati

**vi)Kumbukumbu**

⇒ Maelezo ya kitawasifu kuhusu mtu au jamii inayotambulika kwa kutoa mchango fulani mkubwa.

**3. Vipera Vingine vya Hadithi**

**i) Soga**

⇒ Hadithi fupi za kuchekesha zinazolenga kutania au kudhihaki.

**Sifa**

a) Wahusika ni wa kubuni.
b) Hutaja ukweli unaoumiza.
c) Hutumia vichekesho kupunguza ukali wa dhihaka.
d) Hutumia chuku kupita kiasi.
e) Huhusu tukio moja.
f) Ni fupi.

**Umuhimu**

a) Kukashifu matendo hasi kwa njia ya ucheshi
b) Kuonya na kutahadharisha dhidi ya matendo hasi k.v. ulaghai.
c) Kufunza maadili.
d) Kuburudisha kwa kuchekesha.

**ii) Vigano**

⇒ Hadithi fupi zinazosimulia kuhusu matendo mabaya katika jamii na wakati uo huo kuonya na kuelekeza dhidi yayo.
⇒ Aghalabu huandamana na methali kwa lengo la kufafanua linalokusudiwa au kudhibitisha funzo la methali fulani.

**Sifa**

a) Huwa vifupi.
b) Husimulia kisa kimoja tu.
c) Wahusika ni binadamu na wanyama.
d) Hufunza maadili kutokana na methali.

**iii) Kisa**

⇒ Masimulizi mafupi yenye tukio moja lenye funzo kwa njia ya kufurahisha.

**Mambo ya Kuzingatia katika Uchambuzi wa Hadithi/Ngano**

a) Kueleza aina ya ngano kwa kuzingatia wahusika na maudhui
✔ Ngano yaweza kuwa ya mazimwi na ya mashujaa kwa wakati mmoja.
✔ Ngano yaweza kuwa hurafa, ya usuli na ya kiayari.
b) Kutaja wahusika
c) Kufafanua sifa za wahusika wakuu
d) Maadili/mafunzo yanayojitokeza katika hadithi
e) Kubainisha sifa za ngano/hurafa/hekaya, n.k. zinazojitokeza katika hadithi.
f) Kueleza umuhimu wa fomyula ya kuanzia/wimbo uliotumiwa katika hadithi.
g) Kubainisha tamathali za usemi zilizotumiwa katika hadithi fulani
h) Kuonyesha jinsi ngano inavyoshughulikia maudhui fulani.

i) Kufafanua ufaafu wa methali fulani zilizotumiwa katika hadithi.
j) Katika ngano ya mtanziko, ungekuwa mhusika mkuu ungefanya nini?
k) Kubainisha matumizi ya mbinu ya fantasia
l) Kufafanua maswala ibuka/maudhui yaliyoshughulikiwa k.m. usaliti, ujinga, ulaghai, n.k.
m) Kuchanganua utungo kifani-ploti, wahusika, mbinu za lugha, fantasia, nyimbo, n.k.
n) Kueleza majukumu ya hadithi.

**SEMI**

⇒ Tungo fupi zinazowasilisha ujumbe kwa kufumba au kuchora picha.

**Sifa**

**a)** Huwa fupi kwa kuwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache.
**b)** Ni tanzu tegemezi kwa hutegemea tanzu nyingine kama vile hadithi, mazungumzo, n.k.
c) Hazibadiliki vivi hivi.
d) Baadhi ni kielelezo cha maadili k.v. methali.
e) Hutumia lugha ya kimafumbo.
f) Huibua taswira.
g) Huwa na mchezo wa maneno.
h) Baadhi huwa na muundo maalum k.v. methali na vitendawili.
i) Nyingine ikikosa kutumika hutoweka k.v. misimu.

**Umuhimu**

a) Kuonya k.m methali, 'Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.'
b) Kukuza uwezo wa kufikiri k.m. vitendawili na chemsha bongo.
c) Kutafsidi lugha au kupunguza ukali wa maneno k.m. nahau 'jifungua' badala ya 'zaa'.
d) Kuburudisha k.m. vitendawili, chemsha bongo na vitanza ndimi.
e) Kuhifadhi siri k.m. nahau, misemo, misimu.
f) Kuelimisha k.m. kutofanya mambo kwa pupa-mla kwa pupa hadiriki kula tamu.
g) Kuongeza utamu katika lugha.
h) Kuboresha matamshi k.m. vitanza ndimi.
i) Kukuza lugha k.m misimu.
j) Kukuza utangamano katika jamii kwa kuleta watu pamoja wakati zinawasilishwa.

**Vipera vya Semi**

**i) Methali**

⇒ Semi fupi ambazo hueleza kwa muhtasari au mafumbo ukweli fulani wa kimaisha.

**Sifa**

a) Huwa fupi k.m. 'Msafiri kafiri.'
b) Hutumia tamathali za usemi.
c) Hutumkia lugha ya kimafumbo.
d) Huwa na maana ya ndani na nje.
e) Kunazo hufanana kimaana k.m. 'Haraka haraka haina baraka' na 'Polepole ndio mwendo.'
f) Hupingana zenyewe k.m 'Polepole ndio mwendo' na 'Chelewa chelewa utamkuta mwana si wako.'
g) Huwa na sifa za kishairi k.v. ukwapi, utao na vina -Ha**b**a na ha**ba,** hujaza kiba**ba.**
h) Sifa za utegemezi kwa kuingiliana na tanzu nyingine za fasihi.
i) Huwa na muundo maalum wa sehemu mbili:
   i) Wazok.m 'Haba na haba…'
   ii) Kukamilisha wazo '…hujaza kibaba.'

**Umuhimu**

a) Kukuza uwezo wa kufikiri kwani mpokezi hufikiri ili kupata maana ya ndani.
b) Kuonya dhidi ya matendo yasiyofaa k.m. 'Mchimba kisima huingia mwenyewe'na 'Ukiambiwa jiambie usijeishia kumbe.'
c) Kufariji walio katika hali ngumu, Baada ya dhiki faraja, Hakuna marefu yasiyo na ncha, Liandikwalo ndilo liwalo, Ajaliwalo ndilo apatalo.
d) Kuhimiza watu kujitahidi maishani/kuonyesha jambo jema huja kwa kufanyiwa kazi k.m. 'Mtaka cha mvunguni sharti ainame,' 'Chumia juani ulie kivulini.'
e) Kupamba lugha iwe na mvuto kwani huwa na usanii mkubwa.
f) Kuhimiza ushirikiano, 'Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, 'Jifya moja haliijiki chungu.'
g) Kuelimisha mtu ajue jambo muhimu k.m. 'Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi', 'Pema usijapo pema ukipema si pema tena.'
h) Kushauri k.m. 'Enga kabla ya kujenga' na 'Mchama ago hanyeli.'
i) Kufupisha maadili katika ngano.
j) Kubuni lakabu k.m. 'kikulacho.'

k) Kufunza maadili k.m. kuwa na subira-'Subira huvuta heri.'
l) Kuhimiza kutokata tama k.m. 'Bandu bandu huisha gogo' 'Papo kwa papo kamba hukata njiwe.'
m) Kuonyesha umuhimu wa kuthamini jamaa zako kuliko marafiki k.m. 'Damu ni nzito kuliko maji' 'Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.'
n) Kuonyesha umuhimu wa kuthamini vitu vyako-'Usiache mbachao kwa msala upitao' 'Afadhali dooteni kama ambari kutanda,'
o) Kukashifu ubinafsi k.m. 'Mwamba ngoma huvutia kwake' 'Kila mchukuzi husifu mzigo wake.'
p) Kukashifu kiburi k.m. 'Maskini akipata matako hulia mbwata' 'Zingwi zingwi lipe nguo utaona mashauo.'

**Mbinu za Lugha/Fani /Tamathali za Usemi katika Fasihi**

⇒ Maneno au vifungu vya maneno vinavyotumiwa kutia fasihi urembo ili kufanya ujumbe ueleweke vyema zaidi.

**Aina**

1. Tashbihi

⇒ Ulinganishi kwa kutumia viunganishi kama, mithili, mfano na sawa.

2. Sitiari/ Istiara

⇒ Ulinganishi usio wa moja kwa moja.

3. Tashhisi/Uhaishaji

⇒ Kukipa kitu sifa ya uhai.

4. Taashira/ Ishara

⇒ Kitu kuwakilisha kingine.

5. Chuku/udamisi

⇒ Kutia chumvi au kufanya kitu kionekane kikubwa sana au kidogo sana.

6. Takriri

⇒ Urudiaji wa neno au mafungu ya maneno.

7. Tanakuzi

⇒ Maneno yaliyo kinyume

8. Tabaini

⇒ Msisitizo kwa njia ya kinyume kwa kutumia kikanushio si.

9. Ritifaa

⇒ Kusemesha asiyekuwapo kama yupo.

10. Taharuki

⇒ Kuacha msomaji akiwa na hamu ya kutaka kujua kipi kitakachojiri halafu.

11. Majazi

⇒ Majina yanayooana na sifa za wahusika, vitu au mahali.

12. Mbinu rejeshi

⇒ Kukumbusha mambo yaliyopita.

13. Methali

⇒ Semi fupi ambazo hueleza kwa muhtasari au mafumbo ukweli fulani wa kimaisha.

14. Nahau

⇒ Fungu la maneno lenye maana tofauti na maana ya kawaida ya maneno hayo.

15. Misemo

⇒ Semi zinazobeba ukweli wa kujumla Mifano:

16. Mdokezo

⇒ Mambo kuachwa bila kumalizwa.

17. Balagha

⇒ Maswali yasiyohitaji majibu.

18. Taswira

⇒ Ujenzi wa picha akilini.

19. Kinaya

⇒ Mhusika kutumia maneno au matendo yaliyo kinyume cha inavyotarajiwa.

20. Koja

⇒ Kuorodhesha maneno na vitenzi kwa kutumia koma.

21. Kejeli

⇒ Kudharau au kubeza.

22. Jazanda

⇒ Kufananisha vitu kwa mafumbo k.m. katika biblia.

23. Nidaha/ Siyahi

⇒ Maneno ya kuonyesha hisia za moyoni.

24. Tanakali/onomatopeya

⇒ Miigo ya sauti zinazotokea baada ya kitendo.

25. Uzungumzi nafsia

⇒ Kujisemesha mwenyewe.

26. Dayalojia

27. Utohozi/ Uswahilishaji

28. Kuchanganya ndimi

⇒ Kutumia lugha ngeni.

29. Tafsida/usafidi

⇒ Kutumia lugha ya adabu au kupunguza ukali wa maneno.

30. Mkengeuko

⇒ Kwenda kinyume na matakwa ya jamii k.v. usenge, ndoa ya watu wasio wa rika rika moja, mapenzi nje ya ndoa.

31. ulinganuzi

⇒ Kuweka pamoja mambo yanayopingana ili kulinganisha

32. Kweli kinzani

⇒ Hoja mbili zinazopingana/kutowezekana.

**Matumizi ya Lugha Katika Methali**

**Sitiari**

a) Mgeni ni kuku mweupe.
b) Ahadi ni deni.
c) Upweke ni uvundo.
d) Mgeni ni kuku mweupe.
e) Ujana ni moshi.
f) Mapenzi ni kikohozi.
g) Kukopa arusi kulipa matanga.

**Tashbihi**

a) Kawaida ni kama sheria.
b) Riziki kama ajali ijapo huitambui.
c) Usilolijua ni kama usiku wa giza.
d) Ufalme kama mvua hupiga na kupita.

**Tashhisi**

a) Siri ya mtungi muulize kata.
b) Paka akiondoka panya hutawala.
c) Jembe halimtupi mkulima.
d) Ukupigao ndio ukufunzao.
e) Adhabu ya kaburi aijuaye maiti.

**Takriri**

a) Haba na haba hujaza kibaba.
b) Chovya chovya humaliza buyu la asali.
c) Hauchi hauchi unakucha.
d) Hayawi hayawi huwa.
e) Mtoto wa nyoka ni nyoka.
f) Bandu bandu huisha gogo.

**Balagha**

a) Pilipili usiyoila yakuwashiani?
b) Angurumapo samba mcheza ni nani?
c) Wameshindwa wenye pembe seuze wewe kipara?
d) Simba mla watu akiliwa huwani?
e) Mzigo uko kichwani, kwapa lakutokeani jasho?
f) Mavi usiyoyala wayawingiani kuku?
g) Mla ni mla leo mla jana kalani?

**Taswira**

a) Mpanda farasi wawili hupasuka msamba.
b) Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.
c) Mtupa jongoo hutupa na ung`ong`o wake.
d) Angeenda juu kipungu hafikii mbingu.

**Chuku**

a) Mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.
b) Maji ya kifuu bahari ya chungu.
c) Usipoziba ufa utajenga ukuta.

**Tanakali za sauti**

a) Chururu si ndondondo!
b) Ndo! Ndo! Hujaza ndoo.
c) Kiliacho pa kijutie.

**Kinaya**

a) Bara Hindi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wapo.
b) Kwenye miti hakuna wajenzi.
c) Asante ya punda ni mateke.
d) Kigumba kwa nguruwe kwa binadamu ki uchungu.
e) Kikiharibika cha fundi kikiongoka cha bwana Sudi.

**Kejeli/dhihaka/stihizai**

a) Umekuwa mung`unye waharibikia ukubwani.
b) Hawi Musa kwa kubeba fimbo.
c) Ucha Mungu si kilemba cheupe.
d) Kichwa cha kuku hakistahili kilemba.
e) Kichwa cha nyoka hakibandikwi mtungi.

**Jazanda**

a) Joka la mdimu hulinda watundao

⇒ Mtu mwovu huwanyima wengine vitu asivyovihitaji.
b) Kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma
⇒ Ni rahisi kujitia katika matata kuliko kujitoa.

**Taashira**

a) Kimya kingi kina mshindo mkubwa.
b) Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.

**Kweli kinzani**

a) Wagombanao ndio wapatanao.
b) Ukupigao ndio ukufunzao.
c) Kuinamako ndiko kuinukako.
d) Mwenye kelele hana neno.
e) Kimya kingi kina mshindo mkubwa.

**Tanakuzi**

e) Tamaa mbele mauti nyuma.
f) Mpanda ngazi hushuka.
g) Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.
⇒ Kuainisha methali kutokana na matumizi ya lugha ni kusema mbinu ambazo imetumia.

**Vigezo vya Kuainishia Methali/Kuziweka Pamoja na kuzichambua**

a) Mandhari/mazingira k.m. kilimo.
⇒ Ukipanda pantosha utavuna pankwisha.
⇒ Jembe halimtupi mkulima.
b) Maudhui k.m. ulezi
⇒ Samaki mkunje angali mbichi.
⇒ Mcha mwana kulia hulia yeye

c) fani/tamathali k.m. takriri

⇒ Haba na haba hujaza kibaba
⇒ Mtoto wa nyoka ni nyoka.

d) Jukumu k.m. kuonye

⇒ Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
⇒ Ukiambiwa jiambie usijeishia kumbe.
f) Maana k.m. sawa
⇒ Haraka haraka haina baraka.
⇒ Polepole ndio mwendo.

**Vigezo zaidi vya kuchambua methali**

g) Inarejelea vitu gani? K.m. Hindi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wapo.
⇒ Nchi-Hindi
⇒ Vitu-nguo
⇒ Watu-waendao uchi
h) Inakupa wazo gani kuhusu jamii husika?
⇒ Utamaduni na njia za kiuchumi.

**ii) Vitendawili**

⇒ Semi ambazo hutolewa kwa mtu kwa mfano wa swali ili azifumbue.

**Sifa**

a) Huwa vifupi kimaelezo.
b) Hutumia lugha ya kimafumbo.
c) Hutolewa mbele ya hadhira.
d) Hutumia ufananisho wa kijazanda.
e) Kunazo huhusiana na methali k.m. mzee amekufa vyombo vimevunjikavunjika.
f) Huwa na wakati maalum wa kutolewa yaani jioni.
g) Huwa na mchezo wa maneno k.m. Ukiona njigi utadhani njege.
⇒ Maziwa na tui
h) Hujisimamia vyenyewe.
i) Kunavyo huwa na jibu zaidi ya moja k.v. Gari la kila mtu
⇒ miguu, kifo au jeneza
j) Hutumia tamathali za lugha kwa ufanifu mkubwa
k) Huweza kuwa na fomyula/muundo maalum

i. Mteguaji: Kitendawili
ii. Mteguaji: Tega
iii. Mteguaji: Kitendawili chenyewe- Popoo mbili zavuka mto
iv. Mteguaji : Mlango
v. Mtegaji: Umenoa. Nipe mji.
vi. Mteguaji: Ninakupa Nairobi.
vii. Mteguaji: Nilienda Nairobi watu wa Nairobi wakaniambia nije niwasalimu. Jibu ni macho.

**Umuhimu**

a) Kuburudisha jioni baada ya kazi.
b) Kukuza ubunifu wa kuvitunga kwa kulinganisha vitu katika mazingira ili kuviunda.

c) Kuimarisha uwezo wa kukumbuka.
d) Kukuza uwezo wa kufikiri kwani mfumbiwa huhitaji kufikiri sana ili kupata jibu.
e) Kuleta umoja na ushirikiano katika jamii kwa kuleta watu pamoja wakati vinategwa.
f) Kuimarisha ujuzi wa kujieleza kwa lugha.
g) Kupanua ujuzi wa mazingira wa mtoto.
h) Kuendeleza utamaduni wa jamii k.m. Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini. siwezi kulichuma
⇒ Ndugu wa kiume asimuoe nduguye wa kike.
i) Kukejeli au kudharau tabia mbaya k.m. Wazungu wawili wanachungulia dirishani
⇒ makamasi

**Aina za vitendawili**

a) Sahili
⇒ Vina muundo rahisi/maneno machache k.m Akiona mwangaza wa jua hufa-samaki.
b) Tata
⇒ Vyenye majibu tofauti
c) Kisimulizi
⇒ Masimulizi k.m. Kulikuwa na baba ng'ambo moja ya mto na binti zake wawili ng'ambo ya pili. Alikuwa na maembe mawili aliyopaswa kuyavukisha pamoja apelekee binti zake. Angefanya nini?
d) Vya tanakali k.m. Parrrr! Mpaka Makka-utelezi.
e) Mkufu
⇒ Vyenye sehemu zinazochangizana kimaana k.m. Nikitembea yuko lakini nikiingia nyumbani hupotea-kivuli.

**Matumizi ya Lugha Katika Vitendawili**

**Tashhisi**

a) Amefunika kote kwa blanketi lake jeusi-giza.
b) Akivaa nguo hapendezi, akiwa uchi hupendeza mno-ndizi.
c) Anakula lakini hashibi-kifo/mauti.
d) Amchukuapo hamrudishi-kaburi.
e) Akizungumza kila mtu hubabaika-radi.
f) Daima nasababisha mafarakano-uke wenza.

- **Tashbihi**

a) Boi wangu kazama kaibuka kama mzungu-mwiko wa ugali.

**Sitiari**

b) Bibi hatui mzigo-konokono.
c) Mamangu hachoki kunibeba-kitanda.
d) Fatuma mchafu-ufagio.
e) Saa yetu kadiri inavyotembea ndivyo inavyopunguza nguvu-moyo.
f) Mzungu kujishika kiuno- kikombe.
g) Nina mapapai yangu mawili ambayo siwezi kuyala- matiti ya mwanamke.
h) Ng`ombe wangu nisipomshika mkia hali nyasi-jembe.
i) Kitu changu kitumiwacho na wengine kuliko mimi-jina.
j) Popoo mbili zavuka mto-macho.
k) Gari la kila mtu-miguu.
l) Dada ni mrembo lakini akiguzwa analia-papai.

**Takriri**

a) Huku ng`o na kule ng`o-giza.
b) Amezaliwa Ali, amekufa Ali, amerudi Ali-nywele.
c) Huku fungu katikati bahari-naz.i

**Tanakali**

a) Parrr! Mpaka Makka-utelezi.
b) Huku pi kule pi-mkia wa kondoo atembeapo.
c) Ba funika ba funua (Bak bandika, bak bandua)-nyayo.
d) Tang! Yaanguka-sarafu.

**Kweli kinzani**

a) Ana meno lakini hayaumi-kitana.
b) Ajenga ingawa hana mikono-ndege.
c) Hukopa lakini halipi-kifo.
d) Nina shamba langu kubwa lakini nikivuna halijai hata kofi-nywele.
e) Hufa akifufuka-bahari kupwa.
f) Nameza lakini sishibi-mate.

**Taswira**

a) Adui tumemzingira lakini hatumwezi-moto.
b) Nyama nje, ngozi ndani, mchanga ndani-firgisi ya kuku.
c) Wanatazamana tu lakini hawaamkiani-ardhi na bingu.
d) Askari wangu wote wamevaa kofia upande-mahindi shambani.
e) Samaki wangu aelea kimgongomgongo-merikebu.

f) Babu amebeba machicha meupe kichwani- mvi.

**Stihizai/dhihaka/kejeli**

a) Akivaa miwani hafanyi kazi vizuri-mlevi.
b) Mzungu anachungulia dirishani-makamasi.
c) Uzi mwembamba umefunga dume-usingizi.
d) Mtani wangu hata akiishi majini hatakati-chura.
e) Kisiki chetu hakikui-mbilikimo.
f) Nimemuona bi kizee amejitwika machicha-mvi.

**Jazanda**

a) Mungu alinipa shilingi mbili, moja nitumie nyingine niweke-ardhi na mbingu.

⇒ Kuchambua kitendawili kwa kueleza mbinu za lugha zilizokiunda.

**Kulinganisha vitendawili na methali**

**Kufanana**

- ✔ Zote mbili ni tungo fupi.
- ✔ Zote mbili huwa na maana fiche.
- ✔ Zote mbili hutumia lugha inayojenga taswira.
- ✔ Zote mbili hupata maana kulingana na jamii.
- ✔ Zote mbili Huwa na muundo maalum.
- ✔ Zote mbili hufumbata ukweli fulani wa kijamii.

**Tofauti**

| **Vitendawili** | **Methali** |
|---|---|
| Vina fomyula maalum ya uwasilishaji. | Hazina fomyula. |
| Fumbo lazima lifumbuliwe papo hapo. | Fumbo halifumbuliwi papo hapo. |
| Maarufu zaidi miongoni mwa watoto/vijana. | Kuonyesha hekima hasa miongoni mwa watu wazima na wazee. |
| Hutolewa katika vikao maalum. | Si lazima zitengewe vikao. |
| Hadhira tendi inayotoa maana | Hadhira si tendi. |
| Hutumia lugha ya majibizano. | Kauli moja ya msemaji |

**iii) Chemsha Bongo**

⇒ Maswali ambayo huhitaji mtu kutumia akili na ujuzi kuyajibu.

⇒ Mafumbo ni kauli zenye maana iliyofichika na hujumuisha vitendawili na chemshabongo.

**Mifano**

a) Kilo moja ya chuma na kilo moja ya nyama ipi nzito?
b) Amada ana wafanyikazi saba, wanne hufanya kazi vizuri, wawili ni kama wamekufa, mmoja ni kama mwenda wazimu- miguu, pembe na mkia wa ng'ombe.
c) Kipungu alipita juu, mama na ndege wawili wakamwangalia. Je macho mangapi yalimuona kipungu?- manne.
d) Nina watu wangu watatu, wawili ni watoto na wawili ni baba- mtoto, baba na babu.
e) Chura alitumbukia katika shimo la futi 30 na anaruka futi 10. Aruke mara ngapi ili atoke?- Hawezi.
f) Watu watatu wanavuka mto. Mmoja aliyaona maji na kuyakanyaga. Wapili aliyaona lakini hakuyakanyaga. Watatu hakuyaona wala kuyakanyaga. Watu hao ni kina nani?

**Sifa**

a) Ni kauli fupi au ndefu.
b) Hutuia lugha ya kimafumbo.
c) Hutumia ufananisho wa kijazanda.
d) Huhitaji mtu kuwaza ili kupata jibu.
e) Hujengwa na vitu vinavyotokana na mazingira.
f) Hazina muundo maalum kama methali, nahau na vitendawili
g) Hupima uwezo wa msikilizaji wa kutambua jambo lililofichwa.

**Umuhimu**

a) Kuimarisha stadi ya kusikiliza.
b) Kunoa uwezo wa kufahamu.
c) Kutoa mawaidha.
d) Kufunza kuhusu maumbile.
e) Kuimarisha uwezo wa kukumbuka.
f) Kufunza mambo kuhusu mazingira na maumbile.
g) Kukuza uwezo wa kutumia lugha.
h) Kukuza uwezo wa kufikiri.
i) Kuburudisha na kuchekesha.
j) Kukuza uwezo wa kubuni.

**iv)Vitanza Ndimi**

⇒ Sentensi zenye mfuatano wa sauti zinazotatanisha kimatamshi zinapotamkwa kwa haraka.

**Mifano**

c) Wataita wataita Wataita wa Taita.
d) Waite wale wana wa liwali wale wali wa liwalii
e) Kupa mpe akupao kumpa asokupa si kupa ni kutupa.
f) Shirika la Reli la Rwanda limefungwa.
g) Hilo lililoliwa ndilo nililolitaka.
h) Mchuuzi wa mchuzi hana ujuzi wa mjusi wa juzi.
i) Cha mkufuu mwanafuu ha akila hu cha mwanafuu mkufuu hu akila ha
j) Pema usijapo pema ukipema si pema tena
k) Nguo zisizotakikana zitachomwa zote.

**Sifa**

a) Ni kauli fupi.
b) Huwa na mchezo wa maneno.
c) Huundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi.
d) Hutumia maneno yenye maana zaidi ya moja au yenye sauti sawa.
e) Hutanza/hutatiza ndimi za wengi wakalemewa kutamka.
f) Hukanganya kimatamshi.

**Umuhimu**

a) Kukuza matamshi bora mtu anapoendelea kutamka.
b) Kukuza uwezo wa kufikiri haraka ili kujua maana za maneno ili kutamka ipasavyo.
c) Kupanua ujuzi wa msamiati.
d) Kuburudisha kwa kufurahisha na kuchangamsha.
e) Husaidia kutofautisha maana za maneno.
f) Kujenga stadi ya kusikiliza.
g) Kukuza ubunifu kwa kuteua maneno yanayotatanisha kisauti na kimaana.
h) Kujenga uhusiano bora kwa ucheshi.

**v) Lakabu**

⇒ Jina la msimbo/kupanga/ambalo mtu hupewa au hujipa kutokana na sifa zake.

**Asili ya Lakabu**

a) Tabia
b) Sifa za kimaumbile
c) Matendo
d) Nasaba atokayo mtu.

e) Tabaka
f) Jinsi mtu anavyotamka maneno k.m. ung'eng'e.

**Mifano**

**a)** Nyayo
⇒ Moi
**b)** Simba wa Yuda
⇒ Haille Selassie
**c)** Mkuki uwakao
⇒ Kenyatta
**d)** Nyundo/Tingatinga
⇒ Raila
**e)** Baba wa taifa
⇒ Rais
**f)** Mama wa Taifa
⇒ Mke wa Rais

**Sifa**

a) Huwa neno au fungu la maneno kadha.
b) Huwa na maana iliyofumbwa.
c) Huoana na sifa hasi au chanya za aliyepewa.
d) Huwa za kusifu au kudhihaki.
e) Huweza kudumu hata kusahaulisha jina halisi la mtu.
f) Hutumia sitiari k.m. chui kumaanisha mkali.
g) Hutumia taswira.
h) Hushika sana kimatumizi miongoni mwa watu.

**Umuhimu**

a) Kufahamisha sifa za mtu kwa kifupi.
b) Huwa njia ya washairi ya kujitangaza bila kujisifu moja kwa moja.
c) Hutumiwa kama ishara ya heshima kwa anayestahili heshima k.m. kiongozi.
d) Kuficha utambulisho au jina halisi la mtu.
e) Hutumiwa katika majigambo na mhusika kuonyesha ubingwa wake.
f) Kuficha siri ili anayemrejelewa asijulikane k.m. kikulacho.
g) Kukuza uhusiano bora miongoni mwa watani wanaporejeleana kwa lakabu.
h) Kusifu tabia njema kwa kumpa mtu lakabu nzuri.
i) Kudhihaki au kukashifu tabia mbaya kwa kumpa mtu lakabu mbaya
j) Kutambulisha asili ya mtu.

**vi)Misemo**

⇒ Semi zinazobeba ukweli wa kijumla.

**Mifano**

a) Binadamu ni udongo.
b) Mwili haujengwi kwa mbao.
c) Umaskini si kilema.
d) Lila na fira havitangamani.
e) Ndio kwanza mkoko ualike maua.
⇒ Mambo kuzidi kushika kasi.
f) Mgomba haupandwi changaraweni ukamea
⇒ Jambo halifanywi mahali pasipofaa likapendeza.

**Sifa**

a) Hutumia lugha ya muhtasari.
b) Hutoa ukweli kwa jumla.
c) Hazina muundo maalum.

**Umuhimu**

a) Kusisitiza ujumbe.
b) Kuongeza utamu katika lugha.
c) Kusisitiza jambo fulani.
d) Kufunza maadili au kuhimiza.
e) Kuchochea hisi fulani.

**vii) Nahau**

Fungu la maneno lenye maana tofauti na maana ya kawaida ya maneno hayo.

**Mifano**

a) Kuasi ukapera
✔ kuoa
b) Kupiga vijembe
✔ sema kwa mafumbo
c) Ndege mbaya
✔ bahati mbaya
d) Kidudu mtu
✔ mfitini
e) Paka mafuta kwa mgongo wa chupa

- ✔ Danganya au hadaa mtu

f) Visha kilemba cha ukoka

- ✔ Mpa mtu sifa za uongo ili umpumbaze

g) Kubali shingo upande

h) Kuyavulia maji ngu

- ✔ kumaliza jambo fulani ulilolianzia

i) Arusi ya ndovu kumla mwanawe

- ✔ kubwa

**Sifa**

a) Hutumia lugha ya kimkato.
b) Maneno huwa na maana tofauti na ya kawaida.
c) Kunazo huwa na maana zaidi ya moja k.v. kuja jamvi-kumaliza shughuli au kuondoka.
d) Huundwa kwa neno moja, mawili au zaidi.
e) Huibua taswira.
f) Zina muundo maalum/huundwa kwa aina mbalimbali za maneno.

i. T+T
- ✔ kufa kupona
- ✔ kufumba na kufumbua

ii. T+N
- ✔ kupiga domo
- ✔ kata kamba

iii. T+E
- ✔ Kujikaza kisabuni
- ✔ kufa kiofisa

iv. N+N
- ✔ donda dugu
- ✔ domo kaya

v. N+V
- ✔ nyota njema
- ✔ dege mbaya

vi. N+T
- ✔ damu kumkauka
- ✔ akili kumruka

**Umuhimu**

a) Kukuza na kuendeleza msamiati wa maneno.

b) Kupunguza ukali wa maneno (tafsida).
c) Kuongeza utamu/ladha katika lugha.
d) Kuhifadhi siri kwani sio wote wanajua maana.
e) Kujaribu uwezo wa msikilizaji kufichua maana iliyofichika.

**viii) Misimu/simo**

⇒ Semi ambazo huzuka katika mazingira na kipindi fulani.

**Aina za Mizimu**

1. Inayotumika na kutoweka
2. Inayokita kimatumizi kuingizwa katika Kiswahili sanifu k.m. toa chai, chokora, n.k.

**Asili**

a) Ufupishaji maneno
✔ komp
b) Utohozi
✔ Fathee
✔ hepi
c) Sitiari/jazanda
✔ nyani-mlinda lango
✔ fisi- mlafi
d) Tanakali
✔ mtutu- bunduki
✔ ndala- malapulapu
e) Uundaji maneno mapya
✔ hanya
f) Kupa maneno maana mpya
✔ chuma-gari
✔ toboa- faulu
g) Kugeuza maneno
✔ risto-stori
h) Kuboronga lugha
✔ ashu-ashara/kumi

**Mifano**

a) Jisikia sukari
⇒ kuringa

b) Kaa ngumu
⇒ kutotishika/kuvumilia
c) Chongoa mtu
⇒ mfanyia mzaha
d) Kula njaro
⇒ kupuuza kazi
e) Piga nduthe
⇒ kimbia/toroka
f) Piga ngeta
⇒ kukaba koo
g) Leta diambo
⇒ zozana/lalamika
h) Ingia baridi
⇒ kuogopa
i) Pewa msomo
⇒ gombezwa
j) Kusota
⇒ kuishiwa na pesa
k) Ingia mitini
⇒ toweka/toroka
l) Kung`ara
⇒ kuvaa vizuri
m) Marehemu George
⇒ nguo za mitumba
n) Vaa chupa
⇒ vaa suruari nyembamba
o) Kujisikia poa
⇒ kuwa na furaha
p) Kula hepi
⇒ kuburudika
q) Lala kibahasha
⇒ tulia tuli baada ya kushindwa katika jambo

**Sifa**

a) Ni kauli fupi.
b) Hutumiwa na kundi dogo la watu.
c) Huzuka katika mazingira na kipindi maalum.

d) Ni lugha ya kimafumbo.
e) Hutumiwa na kundi dogo la watu katika jamii.
f) Huzuka na kutoweka baada ya muda.
g) Kunazo hudumu na kukubaliwa kama lugha sanifu k.v. matatu, bodaboda, chai, chokora, daladala, n.k.
h) Huwa na maana nyingi k.m. 'mahewa' humaanisha mziki, uongo au ulevi wa dawa za kulevya.
i) Maneno yana maana tofauti na ya kawaida.
j) Si lugha sanifu na hivyo haipaswi kutumiwa katika mazungumzo rasmi.
k) Hupendeza miongoni mwa watumizi.
l) Hutoweka baada ya matumizi kwa muda.
m) Hubadilika k.m. mbuyu na buda humaanisha baba.

**Umuhimu**

a) Kuficha siri ya wanaoitumia.
b) Kupanua lugha kimsamiati ikikubalika.
c) Kurahisisha mawasiliano kwa kuondoa uchovu wa urasmi.
d) Kuonyesha ubingwa wa lugha kwa kuhisi huonyesha umaarufu wa lugha
e) Kutenga wasio wana kikundi.
f) Kutafsidi/kupunguza ukali wa maneno k.m. Amepata bol-mimba.
g) Kupamba lugha na kuifanya ivutie
h) Kufanya wanakikundi wajihisi kuwa pamoja.
i) Kujitambulisha na watu wa kikundi fulani.

**ix) Shirikina**

⇒ Semi ambazo huonyesha imani fulani ya kundi ya watu

**Mifano**

a) Ukijikuna kiganja cha mikono utapata pesa.
b) Ukila chakula gizani utakula na shetani.
c) Kuzaliwa ukiwa na vidole sita ni kuwa na bahati.
d) Bundi akilia karibu na nyumba mtu mmoja wa nyumba ile atafariki.

**Umuhimu**

a) Kukataza maovu.
b) Kuhifadhi utamaduni.
c) Kuchangia umoja wa kitaifa kwa aina moja ya itikadi kupatikana katika jamii nyingi.
d) Kutujulisha kuhusu itikadi za watu.

**x) Tanakali za Sauti (Onomatopeya)**

⇒ Maneno ambayo huiga sauti ya jambo, tendo au tukio fulani

**Mifano**

a) Boboka bobobo!
✔ payuka ovyo ovyo
b) Bwakia bwaku
✔ akia upesi upesi
c) Bwatika bwata
✔ enda chini kwa mshindo
d) Bweka bwebwebwe!
✔ lia kama mbwa
e) Chaga ngungundu
✔ shikilia jambo
f) Ng'o!
✔ kutoambulia chochote
g) Legalega lege
✔ kosa kuwa imara
h) Chakua nyakunyaku
✔ tafuna kwa kutoa sauti ya kuudhi
i) Bingirika bingiribingiri!
✔ pinduka
j) Birua biru!
✔ angusha na kupindua
k) Shindilia ndi!

**Mianguko**

a) Pu/kacha
✔ tawi
b) Pu, pu, pu
✔ mfululizo
c) Pukupuku!
✔ mvua
d) Pwa!
✔ kwa matope
e) Pwata!
✔ kitu kinene
f) Tang'!

- ✔ sarafu pagumu

g) Tapwi
- ✔ matopeni

h) Tifu
- ✔ mchangani

i) Tubwi/ chubwi
- ✔ majini

**Sifa**

a) Ni kauli fupi.
b) Ni miigo ya sauti zinazotokea baada ya tendo fulani.
c) Hazina muundo maalum.
d) Hujumuishwa katika fani nyingine.
e) Hutumia takriri.

**Umuhimu**

a) Kuwezesha kuunda taswira ya jinsi mambo yanavyotokea.
b) Kuonyesha hisia fulani.
c) Kuongeza uzito kwa maneno.
d) Kuongeza utamu katika mazungumzo.
e) Kusisitiza jambo.
f) Kuipa lugha ladha na mvuto.
g) Kujenga tabia ya kusikiliza kwa makini ili kutambua mlio.
h) Kukuza ustadi wa kuiga na kuigiza.
i) Ni mbinu mojawapo ya mawasiliano.

**xi)Takriri za maana**

⇒ Mafungu ya maneno yanayosisitiza na kueleza maana zaidi ya kitendo.

**Mifano**

a) Haambiliki hasemezeki
b) Siku nenda siku rudi
c) Tilia huku ukitolea kule
d) Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini

**Umuhimu**

a) Kutia ladha katika lugha na kuifanya iwe na mnato.
b) Kusisitiza jambo.
c) Kuonyesha ukwasi wa lugha ya mnenaji.

**xii) Tashbihi**

⇒ Misemo ya ulinganisho

**Sifa**

a) Ni fupi.
b) Hutumia viungio kama, mithili ya, n.k.
c) Hulinganisha.
d) Huwa na ujumbe wa kina.
e) Hutoa taswira ambayo husaidia keleza hulka kikamilifu.

**Umuhimu**

a) Kueleza sifa za kinazozungumziwa
b) Kuongeza lugha utamu
c) Kuonyesha umilisi wa lugha wa mtumizi

**USHAIRI**

⇒ Utanzu wa fasihi unaotumia lugha ya mkato inayoeleza maudhui yake kwa ufupi.

**Sifa**

a) Hutumia lugha ya kimkato.
b) Huwasilishwa mbele ya hadhira.
c) Huwasilishwa na mtu mmoja au kundi la watu.
d) Huwa na muundo maalum k.v. beti, vipande na vina.
e) Hutegemea sauti iliyo kipengele muhimu.
f) Huandamana na ishara za mikono, uso n.k.
g) Una mpangilio maalum wa maneno.
h) Una uteuzi maalum wa maneno.
i) Uwasilishaji wake huandamana na vitendo/uigizaji.
j) Hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa mdomo.
k) Huandamana na shughuli maalum k.v. matanga, kazi, n.k.
l) Huwa na mapigo ya kimziki au huweza kuimbika.
m) Huweza kuambatana na ala za mziki.
n) Hadhira hushiriki katika uwasilishaji wa ushairi simulizi.

**Majukumu**

a) Kuburudisha watu katika sherehe au shughuli fulani ya kijamii.
b) Kutakasa hisia au kutoa hisia zinazomsumbua mtu.
c) Kufunza maadili au tabia zinazokubalika na jamii.
d) Kufariji watu kutokana na maafa, kifo au kushindwa.
e) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga waliotendea jamii mambo makuu k.v. mashujaa.
f) Kuhifadhi historia ya jamii k.m. maghani simulizi na tenzi.
g) Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa jamii.
h) Kuelimisha kuhusu suala fulani.
i) Kukashifu/kukejeli sifa mbaya za wabaya.
j) Kukuza umoja na ushirikiano katika jamii kwa kujumuisha watu pamoja.
k) Kusifu na kutukuza mashujaa katika jamii (tenzi).
l) Kukanya/kutahadharisha dhidi ya matendo maovu.

m) Kukuza urembo au usanii wa lugha kwa kuwa una ufundi mkubwa wa matumizi ya lugha.
n) Kuhamasisha jamii k.v. kisiasa.
o) Kukuza ubunifu kwa mtunzi na mwasilishaji
p) Kukuza ubunifu kwa kutunga kwa kuzingatia beti, mizani, vina na uteuzi maalum wa maneno.

**Vipera vya Ushairi**

a) wimbo
b) maghani
c) mashairi mepesi (utungo unaokaririwa)
d) ngojera (kwa majibizano)
e) tendi au rara (husimuliwa kwa mapigo ya kishairi)

**1. Wimbo**

⇒ Uungo wenye mahadhi ya kupanda na kushuka

**Sifa**

a) Huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
b) Hutolewa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti.
c) Hutumia lugha ya mkato.
d) Hadhira yaweza kuwepo au isiwepo.
e) Huwa na mwimbaji au waimbaji wanaoimba.
f) Waimbaji wanaweza kujivika maleba.
g) Huweza kuambatana na ala k.v. ngoma, zeze, kayamba n.k.
h) Huwa na urudiaji wa mstari au kifungu.
i) Aghalabu huimbwa na kupokezanwa baina ya kiongozi na waimbaji
j) Huimbwa tu au huambatana na kucheza.
k) Huweza kuandamana na shughuli fulani k.v. arusi, kazi, matanga, n.k.
l) Huwa na muundo maalum wa beti, mistari, vina, n.k.

**Majukumu**

a) Kuburudisha k.m. tumbuizo.
b) Nyenzo ya kiuchumi kwa baadhi ya watu.
c) Kuliwaza k.m. mbolezi.
d) Kuhimiza watu wakiwa kazini k.m. hodiya.
e) Kuelimisha kuhusu suala fulani k.m. ukimwi, ufisadi, n.k.
f) Kuhimiza uzalendo k.m. za siasa na taifa.
g) Kumbembeleza mtoto aache kulia au alale k.m. bembelezi.
h) Kukashifu/kukejeli mwenendo mbaya k.v. uchoyo, vivu, n.k.

i) Kufunza maadili au tabia inayokubaliwa na jamii k.v. ukarimu, uaminifu, n.k.

**Ubaya wa nyimbo**

a) Kutumiwa kueneza hisia za kikabila.
b) Kutia watu kasumba.
c) Hutumiwa kueneza propaganda ili kushawishi watu.
d) Kupotosha kimaadili k.v. kuhimiza zinaa.
e) Mtu akizizoea humlevya.

**Aina za nyimbo**

**i) Bembelezi/bembea**

⇒ Nyimbo zilizoimbwa kumbembeleza/kumwongoa mtoto aache kulia au alale.

**Sifa**

a) Huimbwa na mama au walezi.
b) Aghalabu huwa fupi.
c) Huimbwa kwa sauti ya chini.
d) Huimbwa kwa sauti nyororo.
e) Zina mapigo ya polepolena taratibu.
f) Huwa na mahadhi mazuri.
g) Huimbwa aghalabu mtoto akiwa amebebwa kwa mbeleko na mwimbaji akimpapasapapasa.
h) Zina urudiaji wa maneno ya kibwagizo.
i) Huwa na lugha ya kushawishi k.v. kutoa ahadi ya kununulia mtoto zawadi.

**Majukumu**

a) Kumnyamazisha mtoto anapolia.
b) Kuwaongoa watoto walale.
c) Kutumbuiza watoto.
d) Kusuta wasiowapa watoto malezi mema.
e) Kuonya mtoto dhidi ya tabia hasi k.v. kulia ovyo.
f) Kusifu mtoto.
g) Kuonyesha msimamo wa jamii kuhusu mtoto.
h) Kumfariji mtoto k.m. kutokana na kuumia akicheza.

**ii) Nyimbo za watoto/chekechea**

⇒ Zilizoimbwa na watoto wakati wa kucheza/shughuli zao

**Majukumu**

a) Kuburudisha watoto.
b) Kuwaelimisha watoto kuhusu jamii.

c) Kukuza umoja na ushirikiano baina ya watoto kwa kuwajumuisha pamoja na kucheza bila kujali kabila, tabaka, n.k.
d) Kukashifu tabia hasi miongoni mwa watoto k.v. uchoyo.
e) Kukuza ubunifu miongoni mwa watoto wanapobuni nyimbo zinazooana na michezo yao.
f) Kuifanya michezo ya watoto ipendeze.

**iii) Nyimbo za sifa/sifo**

⇒ Za kujisifu au kusifu mtu kwa mchango wake katika jamii.

**Sifa**

a) Zaweza kuwa nyiso, za arusi za kutawazwa n.k.
b) Huimbwa katika muktadha maalum k.v. arusini, jandoni, n.k.
c) Hutumia sitiari au kufananisha na mnyama, mkuki, n.k.
d) Hupiga chuku sifa za anayesifiwa.

**Majukumu**

a) Kusifu mtu kutokana na matendo yake mazuri.
b) Kutangaza mchango na mafanikio ya anayesifiwa.
c) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga matendo mazuri ya anayesifiwa.
d) Kuburudisha watu katika sherehe fulani.
e) Kuangazia matendo ya wahusika.

**iv)Hodiya/yimbo za Kazi**

⇒ Zilizoimbwa wakati wa kazi.

**Sifa**

a) Huimwa watu wakifanya kazi k.v. uwindaji, ukulima, uvuvi, ubaharia, n.k.
b) Huimbwa na mfanyakazi mmoja au kundi lao.
c) Zina maneno ya kuhimiza.
d) Urefu wake hutegemea kazi.
e) Mdundo hutegemea kasi ya kazi ikama inafanywa kwa kasi mdundo ni wa kasi, kama polepole mdundo ni wa polepole.

**Majukumu**

a) Kuburudisha watu wakifanya kazi.
b) Kurahisisha kazi kwa kupunguza fikra za uchovu.
c) Kuhimiza bidii kazini.
d) Kuhimiza watu wapende kazi zao.
e) Kuondoa uchovu na ukinaifu wakati wa kazi.
f) Kuwatia moyo wafanyakazi wasikate tamaa.

g) Kutambulisha jamii kwa kuonyesha shughuli zake za kazi.
h) Kusifu kazi.
i) Kukashifu uvivu.
j) Kuonyesha matatizo na changamoto za wafanyikazi.
**k)** Kujenga umoja na ushirikiano baina ya wafanyakazi wanapoziimba pamoja. **Aina za hodiya**

**a) Wawe/vave**

⇒ Zinazoimbwa wakati wa kulima.

**b) Nyimbo za uwindaji**

⇒ Zilizoimbwa watu wakienda au kutoka katika uwindaji.

**Majukumu**

a) Kumburudisha mwindaji.
b) Kumtoa mwindaji upweke.
c) Kusifu mnyama.
d) Kujasirisha wawindaji.

**c) Kimai**

⇒ Zinazoimbwa katika shughuli za majini k.v. uvuvi na ubaharia.

**Majukumu**

a) Kuburudisha wavuvi na mabaharia.
b) Kuwajasirisha ili kukabili adha za baharini.
c) Kuwatoa upweke.

**v) Nyimbo za mapenzi**

⇒ Zilizoimbwa kutoa hisia za mapenzi.

**Sifa**

a) Huwa na ujumbe wa kimapenzi.
b) Maneno matamu yenye hisia nzito.
c) Matumizi ya chuku k.m. sili wala silali.
d) Huwa zina sifa au kashfa.

**Mjukumu**

e) Kuburudisha anayezisikiliza.
f) Kuomba uchumba au mapenzi.
g) Kusifu tabia au urembo/umbo la mpenzi.
h) Kusifu wapenzi.
i) Kukashifu mpenzi asiye na sifa nzuri.
j) Kusuta waliodhani penzi lisingefaulu.

k) Kupunguza uzito wa hisia k.v. huzuni au udhia baada ya kusalitiwa na mpenzi.

**vi)Nyimbo za arusi**

⇒ Zinazoimbwa wakati wa kufunga ndoa.

**Sifa**

a) Huimbwa kuonyesha hisia za wazazi, jamaa na marafiki
b) Hushauri maharusi na waliohudhuria kuhusu majukumu ya ndoa
c) Wakati mwingine husifia maharusi.

**Majukumu**

a) Kutumbuiza maharusu na waliohudhuria.
b) Kusifu maharusi.
c) Kutoa pongezi kwa Bw. na Bi. arusi kwa kujihifadhi vyema.
d) Kufunza majukumu ya ndoa.
e) Kutoa mwongozo wa kupambana na vikwazo ndoani
f) Kusuta mahasidi waliodhani ndoa isingefaulu.
g) Kukanya na kutahadharisha watu wanaoingilia ndoa za watu kuziharibu.

**vii) Nyimbo za Dini**

⇒ Zilizoandamana na shughuli za kidini.

**Majukumu**

a) Kuabudu Mungu ama miungu.
b) Kusifu mungu/miungu.
c) Kutoa shukrani kwa mungu.
d) Kuomba mema kutoka kwa Mungu au miungu.
e) Kutoa mafunzo ya kidini.

**viii) Tumbuizo**

⇒ Nyimbo za kujipa burudani
⇒ Huimbwa wakati wa mapumziko

**Majukumu**

a) Kutumbuiza watu k.v. ngomani, arusini, n.k.
b) Kuwapa vijana mwongozo/kuadilisha.

**ix)Nyiso/Nyimbo za Tohara**

⇒ Zinazohusiana na tohara.

**Mfano**

*Ewe kilizi*

*Ulozowea kujificha*

*Nyuma ya mama kujikinga, dhidi ya milio*

*ya radi ilo juu mbinguni*

*Jua kesho ni siku ya siku*

*Siku ya kujua mbichi na mbivu*

*Kutofautisha jogoo na vipora,*

*Ngariba taposhika, chake kijembe*

*Ndipo utakapojua bayani*

*Ukoo wetu si wa kunguru*

*Ikiwa hu tayari*

*Kisu kukidhihaki*

*Sithubutu kamwe, wanjani kuingia*

*sije kuniaibisha miye, amiyo na akraba nzima!*

**Sifa**

a) Huambatana na shughuli za jando (wavulana) na unyago (wasichana).
b) Huimbwa faraghani katika mazingira ya tohara pekee.
c) Huimbwa usiku wa kuamkia siku ya tohara.
d) Zilitoa sifa kwa waliotahiriwa, wazazi na wasimamizi wao.
e) Ziliimbwa kuwapa wavulana ujasiri wa kukabili kisu cha ngariba.
f) Zilitoa mafunzo kuhusu majukumu mapya baada ya kutahiriwa.
g) Hujumuisha watu maalum walioteuliwa kushiriki katika sherehe.
h) Huhusisha watu wa jinsia na umri fulani.
i) Maudhui yake hutegemea jinsia.

- **Majukumu**

a) Kuonyesha vijana wamevuka kutoka utotoni hadi utu uzima.
b) Kuwaandaa vijana kwa uchungu watakaouhisi kupitia kijembe.
c) Kuhimiza ujasiri na ukejeli uoga.
d) Kusifu wahusika kwa ujasiri wa kukabili kisu na kuingia katika utu uzima.
e) Kuburudisha waliohudhuria shughuli ya jando au unyago.
f) Kuelekeza vijana kwenye matarajio mapya ya jamii.
g) Kufunza majukumu katika utu uzima.
h) Kukuza umoja na ushirikiano katika jamii kwa kuwaleta wanajamii pamoja.

**x) Mbolezo/Mbolezi**

⇒ Nyimbo za kuomboleza.

**Mfano**

*Nalitazama jua likichwa,*

*Matumaini yangu yakizama pamoja*

*na miale miekundu*

*Nalidhani lilikuwa jinamizi tu*

*Kwamba ulikuwa kesha n'acha*

*Walikuwa wameisha n'ambia*

*Walimwengu*

*Ela nilikataa katakata walosema*

*Nikajitia kuamini waloamba yalikuwa*

*Uzushi*

*Hadi siku hii nilopokea waraka,*

*Waraka ambao ulikuwajeneza ka kuzikia*

*Pendo letu la miongo miwili.*

**Sifa**

**a)** Huimbwa wakati wa maafa, kifo, makumbusho ya mtu au kushindwa katika jambo k.v. vita.
b) Huimbwa kwa sauti ya chini.
c) Hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.
d) Huwa na mapigo ya polepole au taratibu.
e) Huimbwa kwa toni ya huzuni/uchungu kuibua hisia za ndani za mwombolezaji.
f) Aghalabu haziandamani na ala.

**Majukumu**

a) Kuwafariji au kuwasaidia waliofiwa kukabiliana na uchungu wa kupoteza mpendwa wao.
b) Kusifu aliyekufa kwa kutoa sifa zake chanya au michango yao.
c) Kubembeleza roho za wafu(mizimu) ili kusitokee maafa mengine.

d) Kuonyesha msimamo wa jamii kuhusu matokeo ya kifo k.v. husababishwa na pepo, maovu, njia ya kuingia mbinguni.
e) Kutakaswa hisia za huzuni za aliyefiwa kumpunguzia uzito wa kumpotezea mpendwa wake.
f) Kueleza kutoepukika kwa kifo.
g) Kukejeli kifo.

**xi)Nyimbo za Taifa**

⇒ Nyimbo zinazoimbwa na watu wa taifa fulani.

**Majukumu**

a) Kutambulisha taifa fulani.
b) Kuonyesha utaifa.
c) Kuonyesha uzalendo (mapenzi kwa nchi).
d) Kuhimiza uzalendo.
e) Kukashifu wasio wazalendo.
f) Kusifu taifa fulani.

**xii) Nyimbo za Siasa**

⇒ Zinazoimbwa katika shughuli za kisiasa.

**Mfano**

*Ewe mainga wa Ndumi*

*Siwe uloambia akina mama*

*Siku tulopiga foleni*

*Chakula cha msaada kupata*

*Turudishe vifaranga kwenye miji*

*Wageuke vijusi tena*

*Njaa isiwaangamize?*

*Siwe ulopita*

*Matusi ukitema*

*Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?*

*Ukatununua vihela uloturushia*

*Ukatununua kura ukapata?*

*Sasa miaka mitano imetimia*

*Waja tulaghai tena*

*Huna lolote safari hii*

*Ubunge umekudondoka ukitazama*

*Wanyonge tumea/mua*

*Kwingine kujaribu*

**Majukumu**

a) Kuburudisha watu katika shughuli za kisiasa.
b) Kupinga dhuluma za viongozi.
c) Kusifu viongozi na sera zao.
d) Kukashifu/kukejeli wanasiasa wabaya.
e) Kuonyesha matarajio ya watawaliwa kwa viongozi.
f) Kusambaza elimu ya kisiasa.
g) Kuwatia wananchi kasumba.
h) Kueneza propaganda za kisiasa.
i) Kuzindua au kuhamasisha jamii kisiasa.
j) Kuliwaza wahasiriwa wa migogoro ya kisiasa.
k) Kutia watu ari ya kufanya jambo fulani k.v. kupigania haki zao.

**xiii) Nyimbo za Vita**

⇒ Zinazoimbwa na askari vitani au baada ya vita.

**Majukumu**

b) Kuburudisha washiriki.
c) Kufunza namna ya kukabiliana na adui.
d) Kujasirisha washiriki.
e) Kusifu askari vitani.
f) Kukejeli uoga.
g) Kusifu mashujaa wa zamani.
h) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga masujaa.

**xiv) Kongozi**

⇒ Za kuaga mwaka katika jamii za waswahili.

**xv) Jadiiya**

⇒ Nyimbo za jadi ambazo hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

⇒ Huhusu matukio ya kihistoria k.v. shujaa, mateso, njaa, n.k.

**xvi) Nyimbo za Kuzaliwa kwa Mtoto**

⇒ Za kuonyesha au kuadhimisha kuzaliwa kwa mtoto.

**2. Maghani**

⇒ Ushairi ambao hutolewa kwa kalima.

**Sifa**

a) Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanapotambwa.
b) Hutolewa kwa kalima.
c) Hutungwa papo hapo.
d) Hutongolewa mbele ya hadhira
e) Hutungwa kwa ufundi mkubwa.
f) Hutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.

Aina za Maghani

**a) Maghani ya kawaida**

⇒ Ambayo hugusia maswala ya kawaida kama mapenzi, siasa, harusi, kazi, maombolezo n.k.

⇒ Husemwa/huganwa tu bila kusimuliwa.

**b) Maghani Simulizi**

⇒ Maghani ambayo husimulia hadithi kuhusu tukio la kihistoria.

⇒ Huhusu, mtu, tukio, kitu, mnyama, n.k.

**Sifa**

a) Hutokea kama hadithi.
b) Husimulia tukio la kihistoria.
c) Ni ndefu.
d) Waimbaji wake huitwa manju/yeli.
e) Huandamana na ala kama zeze, marimba, n.k.

**Tofauti kati ya maghani ya kawaida na maghani simulizi**

| Maghani ya kawaida | Maghani simulizi |
|---|---|
| Ni fupi. | Ni ndefu . |
| Haitumii ala. | Hutumia ala. |
| Huhusu maswala ya kawaida. | Kihistoria. |
| Husemwa. | Huimbwa. |

**Maghani ya Kawaida**

**i) Vivugo/majigambo**

⇒ Utungo wa kujisifu au kujigamba.

**Sifa**

a) Hutungwa baada ya ushindi wa harakati ngumu k.v. kesi, kumuua simba, kuoa msichana aliyependwa na wengi n.k.
b) Fanani ni mwanamme.
c) Hutungwa papo hapo.
d) Hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe.
e) Hutumia chuku k.m. kujisifu kupita kiasi.
f) Anayejigamba hujipa jina la kiistiari k.m. mnyama.
g) Mhusika huvaa maleba yanayooana na tukio analojisifia.
h) Kuna kutaja jina na ukoo wa baba na mama.
i) Anayejisifu huahidi kutenda maajabu zaidi.

**ii) Pembezi/pembejezi**

⇒ Aina ya tondozi inayokusudiwa kusifu watu aina fulani katika jamii kutokana na matendo au mchango wao.

⇒ k.v. watawala, walezi wazuri, mashujaa wa vita, waganga mashuhuri hata wapenzi waliopigania pendo lao.

**Mfano**

*Nani kama wewe mama?*

*Nani anokufana 'mwaitu'*

*Subira uliumbiwa*

*Bidii nd'o jina lako la pili*

*Moyo wenye heba*

*Msimamo usoyumba*

*Anoelekeza kwa imani*

*Anoadhibu kwa mapenzi makuu*

*Mzazi, mlezi na rafiki wa dhati*

*Tangu siku za kusimama dede.*

**iii) Tondozi**

⇒ Utungo wa kutukuza watu, wanyama na vitu.

⇒ k.v. watu mashuhuri, wapenzi, mifugo, miti mikubwa.

**Mfano**

*Kipungu kipungu*

*Nani kama yeye?*

*Hashindiki kwa nia*

*Hashindiki kwa shabaha*

*Hulenga binguni*

*Hutia ghera kufikiwa peo*

*Peo zisofikika kwa wanokata tama*

*Kipungu, kipungu, hachi tufani za anga.*

**Maghani Simulizi**

**i) Sifo**

⇒ Tungo za kusifu watu kutokana na matendo yao ya kishujaa.
⇒ Sifa zake hukaribiana na za tenzi hasa ikiwa ni shujaa anasifiwa.

**ii) Tendi/tenzi**

⇒ Ushairi mrefu unaoelezea maisha ya mashujaa tangu kuzaliwa hadi kufa kwao.
⇒ k.v. Utenzi wa Fumo Liyongo, Sundiata, Shaka Zulu, Wang`ombe waihura n.k.

**Mfano**

*Asiyemjua mjua aliongwe atamjua*

*Namjuza kwa sifa zake alizokuwa nazo*

*Alisimika ufalme uliosifiwa*

*Akawa shujaa asiyetishwa*

⇒ Utungo huu waweza kuwa wimbo wa sifa au utendi!

**Sifa**

a) Huwa masimulizi yanayotolewa kishairi.
b) Hutoa wasifu wa shujaa.
c) Huwa na matumizi ya chuku.
d) Wahusika hupewa sifa zisizo kawaida (kiungu).
e) Ni masimulizi mrefu.
f) Matumizi ya sitiari k.v. kulinganisha wasifiwa na wanyama wakali.
g) Huangazia matendo ya mashujaa.

h) Husimulia matukio ya kihistoria.
i) Huimbwa pamoja na ala ya kimziki.
j) Hutungwa papo kwa papo na kuhifadhiwa katika ubongo.
k) Hujumuisha mbolezi zinazoonyesha anguko la shujaa.

**Lengo**

a) Kuburudisha wanajamii.
b) Kusifu mashujaa wa jamii.
c) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza wengine kuwaiga mashujaa.
d) Kukuza ubunifu kwa kutunga papo hapo.
e) Kuimarisha uwezo wa kukumbuka kwa kutungwa na kuhifadhiwa akilini.
f) Kuburudisha waliohudhuria sherehe ampapo yanatolewa.
g) Kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii
h) Kukuza ufasaha wa lugha kwa fanani.
i) Kufunza maadili.

**iii) Rara**

⇒ Hadithi fupi na nyepesi za kishairi zenye visa vya kusisimua.

**Mfano**

*Alichukua mkoba wake*

*Akanipa kisogo*

*Kana kwamba hakunijua*

*Kana kwamba hakusema, "Hadi mauko".*

*Hakujali penzi letu*

*Hakujali wana*

*Ambao ndiye alowapa uhai*

*Alijua nilimpenda*

*Ila hata hilo alijipa kujipurukusha*

*Akayoyomea*

*Akamezwa na ulimwengu.*

**Sifa**

a) Huhusu mambo ya kubuni au ya kweli k.v. sherehe ya uhuru, kesi ya mauaji, n.k.

b) Huhusu maswala ibuka na ya kawaida.
c) Hadithi huwasilishwa katika beti.
d) Huimbwa.
e) Huandamana na ala za mziki.
f) Hutolewa kwa toni ya kitanzia.
g) Huwa na visa vya kusisimua.
h) Huwa na ucheshi wenye kinaya.
i) Maswala hayatoleai kwa uwazi bali hufumbwa na kudokezwa.
j) Huwa na uigizaji/utendaji.
k) Mambo yanayosimuliwa hupigwa chuku.

**iv) Rara nafsi**

⇒ Ushairi ambao hutungwa na mtu kuelezea hisia, matatizo na fikra zake mwenyewe.

**Mfano**

*Muda umefika wa pingu kutiwa*

*Kutiwa silisili, kwani si utashi wangu*

*Ukoo waniuza, mithili ya kondoo sokoni*

*Mwambieni shangazi kwaheri nampigia*

*Hata angataka kuniopoa hawezi*

*Kwani mahari imetolewa*

*Mifugo kikwi nduguye amepokea*

*Kwaheri mama, kwaheri dada.*

**Sifa**

a) Hugusia maswala yanayoathiri hisia za mtu binafsi kama vile mapenzi, usaliti, talaka, kifo.
b) Huwasilishwa kwa njia ya uimbaji unaoandamana na ala ya mziki.
c) Mzungumzaji huzungumza moja kwa moja na hadhira au aliyeandikiwa rara hii-mkewe, mpenziwe, mwanawe, Mungu, miungu.
d) Hutolewa katika miktadha k.v. mazishi kusifu aliyekufa, harusi na Bi. Arusi kama ameshinikizwa kuolewa.

**3. Ngonjera**

⇒ Mashairi ya kujibizana/kulumbana-yenye muundo wa kimazungumzo.

**Sifa**

a) Huwa na wahusika wawili au zaidi.
b) Mhusika mmoja huuliza jambo na mwingine hujibu.
c) Huendelezwa kwa njia ya wimbo.
d) Wahusika kupingana mwanzoni.
e) Wahusika huafikiana kufikiwa mwisho.

**Umuhimu**

a) Majibizano hukuza ubunifu kwa kila mmoja kuonyesha umaarufu.
b) Kukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani.
c) Kuimarisha stadi ya kuongea.
d) Kuburudisha hadhira.

**4. Mashairi Mepesi.**

a) Mashairi ya kawaida ambayo hupatikana katika ushairi simulizi.
b) Hujumuisha mashairi mafupi ya kihisia, kimapenzi, kusifu na kukosoa watu.

**Vigezo vya Uchanganuzi wa Tungo za Ushairi Simulizi**

a) Kuainisha utungo kimaudhui/aina
b) Kuthibitisha ni aina fulani ya utungo wa kishairi/sifa.
c) Kutaja sifa zinazojitokeza za ushairi simulizi/utungo fulani wa ushairi simulizi.
d) Muktadha ambamo unaweza kutolewa.
e) Kuandika mbinu za kifasihi zilizotumiwa katika utungo huo.
f) Kufafanua sifa za jamii zinazojitokeza katika utungo.
g) Kuandika majukumu ya aina hiyo ya utungo wa ushairi katika jamii.
h) Anayeimba/nafsi imbi ni nani?
i) Kuandika maadili yanayojitokeza katika utungo.
j) Kueleza toni ya utungo huo.

**MAZUNGUMZO**

⇒ Maongezi ya mdomo yenye usanii.

**Sifa**

a) Huwa maongezi yenye usanii mkubwa.
b) Hutolewa mbele ya hadhira.
c) Hutolewa mbele ya hadhira.
d) Hutolewa kwa njia isiyokera.
e) Huambatana na sherehe fulani k.m. taabili katika matanga.
f) Hutegemea sauti na vitendo.
g) Huhusisha matumizi ya ishara k.v. za uso, mikono na miondoko.

h) Huhitaji ustadi wa kuzungumza ili kuteka hadhira.
i) Hutolewa na watu wenye umilisi mkubwa wa lugha.

**Vipera vya Mazungumzo**

**i) Hotuba**

⇒ Maelezo yanayotolewa mbele ya watu kuhusu mada fulani.
⇒ Huhusisha mada maalum sio suala lolote tu.

**Umuhimu**

a) Kuelimisha kwa kupa maarifa ya kukabiliana na maisha k.v. jandoni na arusini.
b) Kuadilisha au kutoa nasaha hadharani.
c) Huimarisha ukakamavu wa kuzungumza kadiri watu wanavyotoa hotuba hadharani.
d) Kukuza ufasaha na umilisi wa lugha.
e) Kupalilia kipawa cha uongozi.
f) Kuelimisha kwa kupatia watu maarifa ya kukabiliana na changamoto za maisha.

**Aina za Hotuba**

a) Risala
⇒ Hotuba inayowasilishwa mbele ya watu kueleza jambo fulani k.m. ya wafanyakazi kwa waajiri wao.
b) Mhadhara
⇒ Hotuba inayotolewa kwa hadhira fulani kufafanua somo au mada fulani.
c) Kumbukizi
⇒ Hotuba zinazohusu tukio fulani la kihistoria kuhusu mtu au kitu.
d) Mahubiri
⇒ Hotuba zinazohusu masuala ya kidini.
e) Taabili
⇒ Hotuba kuhusu aliyeaga dunia zinazohusu sifa zake nzuri.

**ii) Malumbano Ya Utani**

⇒ Mazungumzo ya kutaniana.

**Aina**

i) Utani wa mawifi na mashemeji
ii) Utani wa marafiki
iii) Utani wa vijana
iv) Utani wa watoto
v) Utani wa marika/ watu wa hirimu moja
⇒ *Wewe ni mweusi kiasi kwamba ukiingia chumbani taa zinazimika.*

vi) Utani wa mababu/mabibi na wajukuu

⇒ *Ee mume wangu, mbona walala mapema hivi? Utawezaje kulilinda boma letu ikiwa wewe ndiwe wa kwanza kujizika kitandani.*

vii) Utani wa maumbu (ndugu na dada)

⇒ *Wewe unajifanya jasiri na juzi baba alikukemea kidogo tu ukaanza kutetemeka kama kondoo aliyenyeshewa.*

viii) Utani wa mazishi

⇒ *Afadhali umekufa tukakuzika, sasa maghala yetu yatasalimika.*

ix) Utani wa makabila/ki ukoo

⇒ *Wakikuyu wanapenda pesa kiasi kwamba maiti ikisikia mlio wa sarafu inaweza kufufuka.*

⇒ *Wakamba wa ukoo wa Akanga wanapenda nyama kiasi cha kula kijusi cha mbuzi.*

**Sifa**

a) Huwa kati ya watu wawili au makundi mawili ya watu.
b) Hufanywa kwa kujibizana papo hapo.
c) Hufanywa kwa njia isiyo ya kuudhi.
d) Hutumia maneno ya mizaha.
e) Hutumia lugha ya ucheshi.
f) Hufanywa na watu wenye uhusiano mzuri.
g) Huchukua njia ya ushindani kila mmoja akitaka kumpiku mwenzake.
h) Watanianao huwa wamekubaliana kufanya hivyo.
i) Hufanyika katika wakati unaofaa sio baada ya kukutana tu.
j) Huhusisha masimango au kumkumbusha mtu wema uliomtendea.
k) Hutumia chuku sana kusisitiza au kukejeli sifa fulani hasi.
l) Huhusisha wakati mwingine utaniaji wa wasiokuwepo ukiambatanishwa na uigizaji wa kuchekesha.
m) Hutegemea uhusiano ulio kati ya wanajamii au makabila.
n) Huandamana na sherehe kama matanga.

**Umuhimu**

a) Kuburudisha kutokana na ucheshi.
b) Kuimarisha urafiki wa watu walio na uhusiano mwema wanaotaniana.
c) Hustawisha ufundi wa lugha.
d) Kukashifu tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, wivu, n.k.
e) Kukosoa wanajamii kwa njia ya kejeli/dhihaka
f) Kuimarisha umoja na ushirikiano kati ya wahusika.

g) Kuliwaza k.m. unaofanywa wakati wa maombolezo.
h) Kukuza na kudumisha mila na desturi za jamii.
i) Kukuza utangamano baina ya watu na wanajamii wanapokuja pamoja na kutaniana.
j) Kuhimiza watu kujieleza kwa uwazi kwa kupunguza urasmi miongoni mwa wanajaii.
k) Hudhihirisha uhusiano mwema baina ya watu wa jamii fulani.

**Changamoto Sasa**

a) Mabadiliko katika jamii yaliyosababisha baadhi ya wanajamii kupoteza nyenzo hii.
b) Kuingiliana kwa watu wa jamii mbalimbali.

**iii) Soga**

⇒ Mazungumzo ya kupitisha wakati yasiyozingatia mada maalum.

**Sifa**

a) Hutokea baina ya watu wa rika moja.
b) Humithilisha uhalisia badala ya kuunakili.
c) Hutumia chuku na kufanywa ljambo lionekane kama halina uhalisia.
d) Hukejeli watu au hali fulani.
e) Wahusika ni wa kubuni.
f) Hutumia vichekesho kupunguza ukali wa ukweli uliomo.
g) Wahusika hupewa majina ya wanajamii husika.
h) Huwa na mafunzo au maadili.

**Umuhimu**

a) Kuburudisha kwa kuchekesha.
b) Kufunza maadili.
c) Kukejeli matendo yasiyofaa katika jamii
d) Kukuza ubunifu baina ya washiriki.
e) Kufunza kuhusu matendo na tabia za kibinadamu.
f) Huwa msingi wa utani unaokuwapo katika jamii.
g) Kuonya na kutahadharisha dhidi ya tabia siyokubalika.

**iv) Mawaidha**

⇒ Mazungumzo ya kutoa ushauri kuhusu jambo fulani.

**Sifa**

a) Huwasilishwa mbele ya watu.
b) Hugusia takriban vipengele vyote vya maisha ya binadamu.

c) Aghalabu hutolewa na watu wenye umri mkubwa.
d) Hulenga maudhui maalum na ya aina nyingi kutegemea jinsia, umri, shughuli, n.k.
e) Hutumia lugha ya kubembeleza na isiyoonyesha ukali.
f) Hutumia lugha ya kuathiri hisia.
g) Huwa na ufasaha mkubwa wa lugha.
h) Ni mawazo mazito kuhusu maisha.
i) Hutolewa katika miktadha rasmi na isiyo rasmi.
j) Ujumbe hulenga hadhira maalum k.m. ya kike au kiume.
k) Hutumia fani nyingine za fasihi kama methali, misemo, ngano, nyimbo n.k. kupitisha mawaidha.
l) Huibua maadili yanayohitaji kuzingatiwa.

**Muundo wa Mawaidha**

a) Utangulizi
⇒ Kutoa kauli ya kuvutia makini ya hadhira k.v. 'Utu uzima huenda na uwajibikaji', au kueleza kiini cha mawaidha.
b) Mwili
⇒ Kutoa wosia, maonyo, maelekezo kutegemea suala analotolea mawaidha akitumia jazanda, kupanda na kushuka kwa sauti, kimya, miondoko, kubadilisha kasi ya kuzungumza, kudondoa semi za watu maarufu, n.k.
c) Hitimisho
⇒ Kuonyesha msimamo kuhusiana na suala analozungumzia.
⇒ Kushirikisha hadhira ili kujua msimamo wao kuhusu suala alilowausia.
⇒ Hadhira kutoa changamoto kuhusiana na mawaidha yanayotolewa.

**Umuhimu wa mawaidha**

a) Kuelekeza jamii kimaadili.
b) Kuelekeza kuhusu jinsi ya kukabiliana na changa moto maishani.
c) Kushauri jinsi ya kutenda jambo fulani.
d) Kujasirisha waoga na kuwapa ukakamavu.
e) Kuwaondolea wanajamii ujinga.
f) Kuhifadhi na kuendeleza mila na desturi za jamii.
g) Njia ya kipato kwa baadhi ya watu.
h) Kuelimisha kuhusu maarifa ya kuendeshea maisha, majukumu na matarajio ya jamii.

**v) Ulumbi**

⇒ Uwezo na ustadi wa kuzungumza kwa uhodari mkubwa.

**Miktadha Ambamo Ulumbi Hutumika Katika Jamii**

a) katika mijadala mbungeni
b) katika hotuba za kisiasa
c) katika mahubiri maabadini
d) katika mijadala shuleni
e) kortini
f) katika shughuli za kijamii k.v. posa
g) katika sala/dua
h) katika maapizo
i) katika malumbano ya utani
j) katika majigambo/vivugo

**Sifa**

a) Hufanywa mbele ya hadhira.
b) Huwa na lengo maalum k.v. kushawishi, kuelimisha, kushauri n.k.
c) Hutumia tamathali za usemi kwa ufanifu mkubwa k.v. chuku, misemo, methali, n.k.
d) Lugha huwa yenye mvuto na ufasaha.
e) Hutumia lugha yenye taharuki na ushawishi.
f) Unenaji huambatana na utumizi wa ishara/ viziada lugha.
g) Uwasilishaji huwa sahili na wenye ujumbe mzito.
h) Huwa na urudiaji mwingi ili kusisitiza na kuvutia usikivu.
i) Huwa na matumizi ya taharuki k.v. mtuo.
j) Huwa na mtiririko mzuri wa mawazo.

**Sifa za Mlumbi**

**a)** Asiwe mwoga ili kuweza kuzungumza hadharani.
**b)** Asiwe na haya ili kuweza kuzungumzia mambo ya aibu inapobidi.
**c)** Awe mchanganfu na mcheshi ili kunasa makini ya hadhira na kuzuia isikinai.
**d)** Awe na ufahamu mpana wa utamaduni wa hadhira asitumie maneno na ishara zinazoweza kuwaudhi au kupingana na imani za hadhira.
**e)** Awe na uwezo wa kuingiliana vizuri na hadhira ili aivutie.
**f)** Awe na kumbukumbu nzuri ili ulumbi wake utiririke vizuri.
**g)** Awe na uwezo wa kudramatisha ili kuonyesha picha fulani k.v. ishara za uso, mwili, miondoko kuonyesha picha ya analozungumzia.
h) Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
i) Aweze kubadilisha toni na kiimbo hadhira isikinai.

j) Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira k.v. kwa maswali ya balagha ili kuondoa uchovu wa kusikiliza.

**k)** Awe na uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusisitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

**Umuhimu**

a) Hukuza uwezo wa kujieleza na kusema hadharani kwa kujiboresha kadiri anavyoendelea.

b) Kigezo cha kuteulia viongozi wa baadaye kwani ushawishi humtambulisha mlumbi kama mwenye uwezo wa kuongoza.

c) Kuelimisha jamii kwa njia isiyochosha.

d) Kudumisha umoja na ushirikiano jamii inapokusanyika pamoja kusikilizaulumbi.

e) Kuhamasisha na kuzindua jamii juu ya suala fulani.

f) Kushawishi walengwa wakubali jambo fulani.

g) Kukuza uwezo wa mwanajamii kushawishi na kupatanisha.

h) Kushawishi watu wapende jambo fulani.

i) Kuburudisha wasililizaji.

**vi) Maapizo**

⇒ Maombi maalum ya kumtaka Mungu, miungu au mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani au muovu.

**Mfano**

*Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,*

*Nami ndiye nilompa uhai mwana unoringia,*

*Anokufanya upite ukinitemea mate,*

*Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,*

*Miungu nawaone chozi langu, wasikie kilio changu,*

*Mizimu nawaone uchungu wangu,*

*Radhi zao wasiwahi kukupa,*

*Laana wakumiminie,*

*Uje kulizwa mara mia na wanao,*

*Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,*

*Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,*

*Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!*

**Sifa**

a) Yalitolewa kwa waliokwenda kinyume na matarajio ya jamii.
b) Yalifanywa mahali maalum k.v. makaburini, porini, chini ya miti mikubwa, n.k.
c) Hutolewa kwa ulaji kiapo.
d) Yalitolewa na mwathiriwa au watu maalum walioteuliwa.
e) Maapizo huaminiwa yataleta maafa kwa jamii.
f) Watoaji maapizo walikuwa walumbi.
g) Maapizo hutumia lugha kali inayonuiwa kutia woga ili kutahadharisha dhidi ya maovu.

**Umuhimu**

a) Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya maovu.
b) Kutambulisha jamii kwani kila mojawapo ina aina yake ya kuapiza.
c) Kukuza umoja katika jamii kwani kaida na miiko hufanya wanajamii kujihisi kuwa kitu kimoja.
d) Kuadilisha wanajamii kwa kujifunza kutenda mema ili kuepuka laana.

**MAIGIZO**

⇒ Utanzu wa fasihi simulizi unaoambatana na vitendo.
⇒ Sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na vitendo.

**Sifa**

a) Huwa na watendaji au waigizaji.
b) Huwasilishwa mbele ya hadhira.
c) Huwasilishwa mahali maalum k.v. ukumbini.
d) Huwasilishwa kwa mazungumzo na matendo
e) Waigizaji hujivika maleba yanayooana kutia uhai maigizo.
f) Matayarisho kabambe hufanywa kabla ya maigizo.
g) Huweza kuambatana na ngoma pamoja na uimbaji.
h) Lugha ni yenye ufundi wa juu k.v. picha, mafumbo na tamathali.
i) Huweza kuambatana na sherehe fulani ya kitamaduni k.v. jando, matanga, n.k.
j) Huwasilishwa kwa lugha sahili.
k) Hujaa taswira zinazoweza kutambulika na hadhira.

**Umuhimu**

a) Kuburudisha wahusika na hadhira.
b) Kukuza umoja na ushirikiano kwa kujumuisha watu pamoja.

c) Kuimarisha uwezo wa kuzungumza hadharani-kupata ukakamavu jinsi mtu anapoendelea kuigiza.
d) Kukuza umoja na ushirikiano watu wanapojumuika pamoja kutazama maigizo.
e) Kukuza uwezo wa kukumbuka kwani mwigizaji huhitaji kukumbuka maneno halisi.
f) Kukejeli kitendo kisichofaa/cha kijinga alichofanya mtu.
g) Njia ya kipato/kuwatafutia riziki baadhi ya watu.
h) Kutoa nafasi kwa watu kudhihirisha vipawa vyao.
i) Kuonya na kutahadharisha watu dhidi ya kufaya mambo yasiyofaa.
j) Kuelimisha watu wafahamu jambo fulani k.v. ukimwi, ufisadi, n.k.
k) Kukosoa watu wanaofanya kinyume na matarajio ya jamii k.v. wivu, uchoyo, n.k.
l) Kupitisha maarifa na amali za kijamii.

**Ploti**

a) Utangulizi-kutambulisha mgogoro
b) Ukuzaji wa mgogoro
c) Kilele cha mgogoro
d) Usuluhishaji wa mgogoro

**Aina za maigizo**

**a) Maigizo Ya Kawaida**

⇒ Maonyesho ya jadi yakiwa yameondolewa kwenye mazingira yake halisi.

**b) Sanaa ya Maonyesho**

⇒ Matendo ya kweli yanayojitokeza katika jamii kulingana na mazingira yake halisi k.m. uganga, mazishi, unyago, ngoma, n.k.

**Tofauti**

| Maigizo ya kawaida | Sanaa ya maonyesho |
|---|---|
| Mazingira ya kuzua/maalum | Hutumia mazingira halisi |
| Matukio ya kuiga | Matukio halisi/ ya kila siku. |
| Huwa na wahusika na hadhira maalum | Washiriki na waigizaji walio pia hadhira |
| Matumizi ya ukumbi na jukwaa maalum | akuna haja ya ukumbi wala jukwaa |
| Hutumia maleba na vifaa vya kuzua mazingira maalum | Hakuna vifaa maalum bali huwa mazingira yenyewe. |
| Hugawika katika maonyesho Kutumia lugha kwa njia maalum | Muundo wake hufululuza au hayajagawika katika maonyesho. |

- Wahusika hufanya mazoezi kabla ya igizo halisi
- Hawahitaji kufanya mazoezi kwani ni matukio ya kila siku.

**Maigizo ya kawaida**

**i) Michezo ya Kuigiza**

⇒ Maigizo ambayo huwasilishwa na watendaji jukwaani mbele ya watu.

**Sifa za Mwigizaji bora**

a) Awe jasiri ili aweze kuigiza mbele ya watu/hadharani.
b) Awe na ubunifu ili aweze kufanya uigizaji kuvutia na kuondoa ukinaifu.
c) Awe na ujuzi wa kutumia ishara za uso, mwili na miondoko kuonyesha picha ya hali anayoigiza.
d) Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
e) Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v. huzuni.
f) Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira kwa maswali ya balagha ili kuondoa uchovu.
g) Awe na uwezo wa ufaraguzi/ kubadilisha uigizaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika kutoka katika mazingira ya hadhira.
h) Awe anaelewa utamaduni wa hadhira yake ili asitumie maneno na ishara ambazo zinaudhi ama kukinzana na na imani zao.

**ii) Vichekesho**

⇒ Michezo ya kuigiza inayokusudiwa kuzua kicheko ili kupitisha ujumbe k.m. vioja, vitimbi n.k.

**Sifa**

a) Vichekesho huigizwa.
b) Huwasilishwa kwa lugha sahili.
c) Hujaa taswira zinazoweza kutambulika na hadhira.
d) Hutumia mbinu ya kejeli, kunaya na tashtiti.
e) Vichekesho huwa vifupi.
f) Havihitaji uchambuzi wa ndani ili kuvielewa au kupata maana.

**Jukumu**

a) Kuburudisha hadhira kwa kuchekesha.
b) Kuelimisha kwa kuonyesha jambo la kijinga alilofanya mtu.
c) Njia ya kuwapatia watu riziki.
d) Hutumika katika hadithi kuifanya ivutie.

e) Kukejeli kitendo fulani kisichofaa alichofanya mtu fulani.
f) Kukashifu matendo hasi ya kijinga.
g) Kuadilisha ama kutoa funzo fulani la tabia njema.

**iii) Ngonjera**

⇒ Ngonjera inayoambatana na uigizaji/utendaji.

**Sifa**

a) Kuweko kwa uigizaji/utendaji k.v. ishara za uso na mikono.
b) Huwa na wahusika wawili au zaidi.
c) Huendelezwa kwa njia ya wimbo.
d) Mhusika mmoja huuliza jambo na mwingine hujibu.
e) Wahusika kupingana mwanzoni.
f) Wahusika hufikia uafikiano kufikia mwisho.

**iv) Michezo ya Watoto/Chekechea**

⇒ Michezo inayoigizwa na watoto katika shughuli zao.

**Aina**

a) Mchezo wa baba na mama
b) Kuruka kamba
c) Kujificha na kutafutana
d) Kukimbiza kibaramwezi dhidi ya upepo ili kizunguke
e) Mchezo wa baba na mama

**Sifa**

a) Waigizaji ni watoto.
b) Huhusu shughuli za kiuchumi na kitamaduni k.v. arusi, siasa, ukulima.
c) Huandamana na nyimbo za watoto.
d) Huwa na miondoko mingi k.v. kujificha, kuruka.
e) Huwa na matumizi mengi ya takriri.
f) Huchezwa popote.
g) Huwa na kanuni fulani.
h) Hukoma watoto wakichoka au wakikiuka kanuni

**Umuhimu**

a) Kufunza watoto majukumu yao ya utu uzima.
b) Kuwatanguliza watoto katika sanaa ya uigizaji.
c) Kukuza ubunifu wa watoto kadiri wanapoendelea kuigiza.
d) Kudumisha utamaduni wa jamii.

e) Kuburudisha watoto.
f) Kukuza stadi ya uigizaji miongoni mwa watoto.
g) Kukuza utangamano miongoni mwa watoto kwa kuwajumuisha pamoja.
h) Kukashifu matendo hasi ya watu wazima kwa watoto.
i) Kuwapa watoto ukakamavu na kujiamini wakiwa wachanga.

**v) Majigambo/vivugo**

⇒ Uigizaji ambapo wahusika hujigamba kwa matendo ya kishujaa.

**Mfano**

*Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu*

*Ulojipamba kwa mabingwa*

*Wachezaji hodari wa ngoma*

*Ndimi dume liloingia nyanjani*

*Makoo yakatetemeka*

*Yakang'ang'ania, ngozi kusakata nani*

*Kijiji kizima kilinijua*

*Wazee walilienzi*

*Wakamiminika kiamboni*

*Mabinti kunikabithi.*

**Sifa**

a) Aghalabu huambatana na ngoma.
b) Hujitokeza, kujigamba na kisha kuendelea kucheza ngoma.
c) Anayejigamba hubeba zana zake za vita kama vile mkuki na ngao kuonyesha aliyotenda.
d) Anayejigamba huvaa maleba kuambatana na jambo analojisifia.

**vi) Utambaji**

⇒ Usimulizi wa hadithi unaoambatana na uigizaji.
⇒ Huwa na matumizi ya vizuizui.

**vii) Mazingira**

⇒ Uigizaji wa maumbile asilia yaliyozunguka jamii ya watu k.v. sauti za wanyama.
⇒ Kuna matumizi ya viziuzui, matawi n.k.

**Sanaa ya Maonyesho**

**i) Ngoma**

⇒ Uchezeshaji wa viungo vya mwili kuambatana na mdundo au miondoko maalum.

**Aina**

e) Ngoma za wanawake
f) Ngoma za tohara
g) Ngoma za wanaume
h) Ngoma za sherehe
i) Ngoma za vijana
j) Ngoma za unyago na jando
a) Ngoma za wazee
b) Ngoma za arusi
c) Ngoma za kufukuza mapepo
d) Ngoma za kuaga mwaka

**Sifa**

a) Huandamana na muziki na ala ya muziki k.v. ngoma.
b) Ngoma huchezewa mahali wazi na penye hadhira.
c) Wachezaji huvaa maleba maalum kulingana na funzo linalonuiwa.
d) Huwa na wahusika aina mbili; watendaji na watazamaji kwa wakati mmoja.
e) Huweza kuandamana au kutoandamana na sherehe.
f) Hutofautiana kulingana na jamii husika.

**Umuhimu**

(a) Kuburudisha kwa ufundi wa kucheza kwa kuzingatia miondoko.
(b) Kitambulisho cha jamii kwani kila moja ina aina yake ya ngoma.
(c) Kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii husika.
(d) Kukuza uzalendo kwa kuwafanya wanajamii kuionea fahari jamii yao.
(e) Kukuza umoja na ushirikiano kwa kujumuisha watu pamoja.
(f) Kuelimisha kwa kupitisha mafunzo na maarifa.

**ii) Matambiko**

⇒ Utoaji wa kafara kwa Mungu, miungu, pepo au mizimu ili wasaidiwe kutatua shida, kutoa shukrani au kuomba radhi.

**Sifa**

g) Hutolewa na wazee maarufu walioteuliwa.
h) Hufanywa nahali maalum k.v. pangoni, mwituni, n.k.
i) Huandamana na sala.
j) Huandamana na utoaji kafara k.v. kuchinja mbuzi, n.k.
k) Huandamana na maombi.

**iii) Maigizo Ya Uganga wa Ramli**

**Sifa**

a) Mganga hujitia kujua kwa hivyo vitendo vyake ni maigizo ya uganga wa madaktari.
b) Mengi katika matendo ya mganga hayana mashiko.
c) Aghalabu kafara hutolewa.
d) Waganga wanapopiga bao huvaa maleba kama ngozi, vibuyu, pembe, n.k.
e) Huweza kuwa na fimbo maalum.
f) Lugha maalum anayodai kuitumia kuwasiliana na misimu.
g) Mizimu humshauri mganga kuhusu ugonjwa na tiba inayofaa.
**h)** Mganga humchanja mgonjwa na kumpa dawa za miti shamba.

**Umuhimu**

a) Wakati mwingine mizizi ya mganga huponya.
b) Huwapa watu matumaini hasa walio na magonjwa yasiyo na tiba.
c) Dawa za mganga hupunga mashetani kwa wagonjwa wake.
d) Hukutanisha ulimwengu wa mizimu na ulimwengu halisi.
e) Waganga huburudisha wanapoigiza.

**Hasara**

a) Mgonjwa huenda asipone kwani matendo mengi ya mganga ni ya kukisia.
b) Dawa za uganga zaweza kumdhuru mtu.
c) Malipo ni ghali na mtu hata aweza kufilisika akitafuta tiba ya ugonjwa usiopona.
d) Mazingira ya uganga husheheni uchafu mwingi.
e) Mgonjwa huridhika kwa muda mfupi halafu uhalisia hudhihirika.

**iv)Ngomezi**

⇒ Uwasilishaji wa ujumbe kwa kupiga ngoma au zana nyingine ya kimziki.

**Sifa**

a) Kuwepo kwa ngoma au ala nyingine kama panda.
b) Mapigo ya ngoma hueleweka tu na jamii husika.
c) Mapigo kufuata toni au ridhimu maalum kuwasilisha maneno fulani.
d) Kuwepo kwa hadhira au wasikilizaji.

e) Kueleweka kwa mapigo hayo na wanajamii husika pekee.
f) Makini huhitajika ili kupata midundo.

**Aina za ngomezi**

**a) Taarifa**

⇒ Huarifu kuhusu jambo k.m. msimu wa kuanza kutayarisha mashamba, kuitwa katika mkutano, kazi ya ujima n.k.

**b) Tahadhari**

⇒ Hutoa tahadhari kuhusu mavamizi kama wizi wa mifugo, vita, majanga kama moto, mafuriko n.k.

**c) Uhusiano**

⇒ Kuita watu kwa sherehe.

**Umuhimu wa Ngomezi**

a) Njia ya mawasiliano kwa jamii zisizojua kusoma.
b) Husaidia wanaokabiliwa na ugumu wa mawasiliano.
c) Kuharakisha mawasiliano katika masafa mafupi.
d) Kutoa taarifa kuhusu matukio fulani k.m. ndoa, kifo n.k.
e) Husaidia kupitisha jumbe za dharura.
f) Kutahadharisha wanajamii kuhusu tukio la hatari/dharura k.v. vita, gharika n.k.
g) Kuficha siri kwa kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyoeleweka.
h) Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa jamii.
i) Namna ya kudhihirisha ufundi wa kutumia zana kama ngoma.
j) Kitambulisho cha jamii kwani kila jamii hupitisha ujumbe kwa mapigo tofauti.

**Udhaifu wa Ngomezi**

a) Si kila mtu anaweza kufasiri ujumbe unaokusudiwa.
b) Mapigo hayasikiki mbali na hivyo husikika na idadi dogo ya watu.
c) Mapigo yaweza kuhitilafiana na hivyo kufasiriwa kwa namna tofauti.

**Ngomezi za kisasa**

a) Milio ya ambulensi, magari ya polisi na zimamoto.
b) Kengele za kubisha hodi nyumbani zinazotumia umeme.
c) Kengele shuleni, makanisani, n.k.
**d)** Toni za rununu zinazowakilisha aina mbalimbali za jumbe.
**e)** Ving'ora vya kuashiria moto umetokea katika majumba ya horofa, benki, hospitalini, n.k.

**Changamoto za Ngomezi katika Jamii ya Sasa**

a) Mwingiliano wa jamii mbalimbali unaosababisha kutofasiri ujumbe kwa njia moja inayotakikana.
b) Viwanda na majumba marefu kusababisha kutosikika kwa sauti au milio ya ngoma.
c) Njia nyingine za kisasa za mawasiliano zinazotumiwa kwa wingi na kwa wepesi.
d) Uhaba wa zana kama baragumu na zumari zilizokuwa zinatumika.
e) Mabadiliko ya maisha kuleta ubinafsi na kusababisha wengi kutoitikia wito wa vyombo.

**v) Mivigha**

⇒ Sherehe za kitamaduni ambazo hutokea katika kipindi fulani cha mwaka ambazo huonyesha mwanajamii ametoka kiwango kimoja hadi kingine.

**Aina za Mivigha**

a) Sherehe za tohara
⇒ kutoka utotoni na kuingia utu uzimani.
b) Sherehe za ndoa
⇒ kutoka kapera hadi kuoa
c) Sherehe za kutambika
⇒ kutoa sadaka kwa Mungu, miungu, pepo au mizimu
d) Sherehe kutawazwa kwa kiongozi
⇒ kutoka uraia na kuingia katika uongozi/utawala
e) Shughuli za mazishi/matanga
⇒ kutoka uhai hadi ufu
f) Sherehe za kuwapa watoto majina
g) Sherehe za ulaji kiapo
h) Shughuli za posa
i) ibada

**Hatua**

a) Kutoa mtu rasmi kutoka kundi moja la wanajamii.
b) Kumfundisha majukumu yanayohusiana na wadhifa mpya.
c) Kumwingiza rasmi katika kundi jingine.

**Sifa**

a) Huandamana na matendo au kanuni fulani (mivigha).
b) Maleba maalum huvaliwa na wahusika kuwatofautisha na hadhira.
c) Hufanyika kwa kutumia lugha maalum au kimyakimya.

d) Kuna watu aina tatu: watendaji wanaoshiriki kuimba na kucheza, wale sherehe inafanyika kwa sababu yao na wanaoshuhudia tu.
e) Huhusisha vitendo maalum kama kula viapo, kutoa kafara, kucheza ngoma, n.k.
f) Huandamana na utoaji wa mawaidha.
g) Uigizaji hujitokeza pale mwanajamii anaingizwa katika kundi fulani kutoka jingine.
h) Huhusisha maombi.
i) Hufanywa mahali maalum sherehe hiyo inapofanyika k.m. tambiko hufanywa porini au pangoni.
j) Wahusika huweka ahadi za kutenda wema.
k) Huwa na mpangilio wa shughuli kuanzia mwanzo, kati hadi mwisho.

**Umuhimu**

d) Kuburudisha kwa vile baadhi ya mivigha huhusisha nyimbo, ngoma na uigizaji.
e) Kutoa mafunzo ya utu uzima na elimu ya jadi.
f) Mivigha ya mazishi huliwaza wafiwa.
g) Kukuza utangamano miongoni mwa wanajamii kwa kuwajumuisha pamoja katika mivigha yao.
h) Kuashiria mwanajamii ametoka kiwango kimoja cha maisha hadi kingine.
i) Kujenga uhusiano bora kati ya jamii na miungu au mizimu.
j) Kitambulisho cha jamii kwani kila moja ina aina yake ya mivigha.
k) Kudumisha mila za jamii.
l) Kuelimisha jinsi ya kukabiliana na changamoto maishani.
m) Kuadilisha kwa kufunza tabia zinazokubalika na jamii k.v. uaminifu, utiifu, n.k.
n) Kukashifu vitendo vya uoga.
o) Kukuza uzalendo kwa kuhimiza wanajamii kuonea fahari tamaduni zao.
p) Msingi wa wanajamii kujitambulisha na kuionea fahari jamii yao.

**Hasara**

a) Baadhi ya mivigha huhatarisha afya na maisha k.v. kutahiri watoto wa kike.
b) Baadhi ya sherehe hukiuka maadili kama vile kwa kuruhusu matusi hata kushiriki ngono.
c) Baadhi yaweza kusababisha hasara kama vile kueneza ukimwi k.v. tohara kwa kisu kimoja.
d) Huzua tofauti za kijinsia k.v. mwanamme kujiona bora kuliko mwanamke.
e) Kuzua utabaka baina ya waliopashwa na wasiopashwa tohara.
f) Baadhi ya mivigha hukiuka malengo ya kitaifa k.m. ukeketaji ni ukiukaji wa haki za binadamu

g) Kunayo hujaza watu hofu k.v. kufukuza mapepo kunakohitaji kafara ya binadamu.
h) Baadhi huhusisha ushirikina na hivyo kusababisha uhasama baina ya koo.
i) Baadhi hugharimu kiasi kikubwa cha pesa na kuifilisi familia.

# FASIHI SIMULIZI II

Fasihi ni Sanaa inayotumia lugha au maneno katika sura mbalimbali kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu. Kuna aina mbili kuu za fasihi; fasihi simulizi na fasihi andishi.

**Fasihi simulizi**

Huwasilishwa kwa njia ya mdomo toka kizazi kimoja hadi kingine au masimulizi.

Fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.

**Tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi**

**Fasihi simulizi**

- Huwasilishwa na fanani au masimulizi kwa njia ya masimulizi ya mdomo.
- Huhifadhiwa akilini na kusambazwa kwa njia ya masimulizi.
- Ina uhuru wa kutumia wahusika mbalimbali kama vile binadamu na viumbe vinginevyo.
- Ina tanzu nyingi kuliko fasihi andishi kama vile hadithi, semi, ngonjera, ushairi simulizi, maigizo.
- Ni mali ya jamii nzima inayohusika.
- Ni kongwe kuliko fasihi andishi kwani imekuwepo tangu kuwepo kwa binadamu.
- Hadhira yake ni watu wote katika jamii; watoto, wazee, vipofu, viziwi na kadhalika.
- Hubadilika kulingana na mfumo wa jamii.
- Ina hadhira ya utendaji.
- Ina hadhira hai.
- Inaweza kubadilishwa papo kwa hapo ili kukidhi mahitaji ya hadhira.

**Fasihi andishi**

- Huwasilishwa na mwandishi kwa njia ya maandishi.
- Huhifadhiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa maandishi.
- Ina tanzu chache kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi.
- Mara nyingi wahusika ni binadamu kwani inahusu binadamu na mazingira yake.
- Ni mali ya mwandishi aliyetunga.

**Fafanua sifa za mtambaji/fanani wa fasihi simulizi**

Mtambaji anapaswa kuothi sifa zifuatazo ili awe mtambaji bora wa ngano au hadithi:

- Kuelewa utamaduni; lazima aelewe utamaduni wa jamii husika vizuri.
- Uwezo wa ufaraguzi, awe na uwezo wa kufaragua au kubadilisha sifa fulani za ngano kutegemea hadhira.
- Awe mcheshi, ucheshi ni mbinu ya kuvuta nadhari ya hadhira.
- Kuifahamu lugha vizuri, aelewe maana ya maneno, misemo na methali.
- Ubingwa wa kuwasilishwa kwa matendo, anaweza kutumia ishara za mkono na kuiga miondoko jukwaani ili kuivutia hadhira yake.
- Kuwa mlumbi mzuri, sauti ni nyenzo kuu ya uwasilishaji wa ngano au utambaji. Mtambaji awe anasikika na anaongea lugha kwa namna inayoeleweka na hadhira yake.

**Utangulizi Wa Hadithi**

Kuna vitangulizi vya hadithi au fomula:

A) Mtambaji: Paukwa!

Hadhira: Pakawa!

B) Mtambaji: Paukwa!

Hadhira: Pakawa

Mtambaji: Sahani

Hadhira: Ya mchele

Mtambaji: Giza

Hadhira: La mwizi

C) Mtambaji: Hadithi hadithi

Hadhira: Hadithi njoo…

D) Mtambaji: Kaondokea chanjagaa kajenga nyumba kakaa mwanangu mwana siti vijino kama chikichi nitamjengea nyumba na vilango vya kupitia. Hapo zamani za kale...

**Majukumu ya ufunguzi.**

- Kuvuta nadhari au makini ya hadhira.
- Kubainisha mtambaji wa hadithi.
- Kudhihirisha kuwa msimulizi yuko katika ulimwengu wa hadithi wala si kawaida.
- Kuitathmini hadhira kama iko tayari kwa hadithi.
- Kuashiria mwanzo wa hadithi.
- Kubainisha utanzu wa fasihi simulizi-hadithi.

**Kimalizio cha hadithi**.

Katika kutamatisha hadithi ni lazima iwe na kimalizio kwa mfano:

... Na wakaishi kwa amani milele na milele.

... Hadithi yangu imeishia hapo.

...Tangu siku hiyo paka na panya wakawa adui.

...kweli damu ni nzito kuliko maji.

...Alhamdullilahi.

**Majukumu ya kimalizio.**

- Kuashiria mwisho wa utambaji.
- Njia ya kupumzisha hadhira.
- Kiashiria cha kumwonyesha mtambaji mwengine kuwa anaweza akaanza.

**Umuhimu wa hadithi katika fasihi simulizi**.

- Hadithi hutumiwa kuipatia jamii mwelekeo, kuna methali isemayo kuwa mwacha mila ni mtumwa hivyo basi jamii inayopuuza kale yake au fasihi yake hukosa mwelekeo.
- Hadithi hutumiwa kuendeleza maadili ambayo huwa kama nguzo kuu ya wanajamii.
- Hadithi: huonya, huelimisha na hushauri jamii. Hadithi huwa na wahusika wenye tabia chanya na sifa hasi. Wenye sifa chanya huweza kuangaliwa kama kielelezo kizuri cha jamii na wenye sifa hasi wanafaa kupuuzwa.

- Hutumiwa kurithisha jamii, elimu na thamani muhimu kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Hutumiwa kama burudani.
- Kuendeleza uhusiano uliopo kati ya wanajamii na hasa uhusiano wa kushirikiana.
- Kukuza uwezo wa kumbukizi.
- Kuendeleza ufahamu.

**HADITHI/NGANO**

Ni hadithi za kimapokeo ambazo zimerithishwa na hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

**Sifa za ngano**

- Kuwepo kwa mianzo maalum kwa mfano hapo zamani za kale...
- Kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Uwezekano wa kubadilisha kwa sehemu fulani hutegemea hadhira inayohusika.
- Kuwepo kwa maadili au funzo ambalo liko wazi ama linaloweza kuashiriwa kwa kuwepo kwa methali, misemo au kauli fulani.
- Kuwa na matumizi ya urudiaji kama vile wimbo, vifungu au maelezo.

**VIPERA VYA HADITHI**

**(A) Ngano za kibunifu.**

1. **Hekaya/Ayari**

Ayari ni mdanganyifu au mtu anayetumia ujanja; kimsingi ngano za ayari zina uhusisha mhusika ambaye anajifanya rafiki huku akiwa na dhamira ya kujinufaisha mwenyewe.

Ni ngano ambapo mhusika mmoja anatumia hila au ujanja kulaghai wengine.

**Sifa za hekaya**

- Ni masimulizi ya moja kwa moja kwa lugha nathari.
- Wahusika wake wakuu huwa sana sana sungura na Abunwasi.
- Matendo yao huwa yamejaa ujanja.
- Kisa huwa kifupi.
- Werevu na ujanja hujitokeza bayana kisani.
- Mara nyingi mafunzo huwa: hekima, maadili na mienendo ya jamii, kwa kuonyesha hila na ujanja.
- Werevu unashinda.

Mfano

*Hapo zamani za kale paliondokea sungura na jirani yake Mtajika. Mtajika alikuwa na mali nyingi kama vile sufuria kubwa za kuwapikia wageni naye Sungura alikuwa na visufuria vidogo. Siku baada ya siku Sungura alikuwa akiazima sufuria kwa Mtajika, anaporejesha ile sufuria baada ya kukaa nayo kwa majuma kadhaa anairejesha na nyingine ndogo. Mtajika akamuuliza "Mbona umekawia kunilete sufuria yangu jameni?" Sungura akamjibu kwamba sufuria yako ilikuwa ikizaa ndio maana nimekuletea hii ndogo ambayo ni mtoto wa sufuria yako?" Mtajika alifurahi na kutabasabu kama kibogoyo aliyeota meno wakati wa mlo wa nyama. Siku mosi Sungura alipata wageni wengi na alikuwa na mpango wa kugura eneo hilo. Alimwendea Mtajika na kumwazima sufuria ile kubwa kabisa ili akawapikie wageni wake. Baada ya majuma mawili Sungura alirejea kwa Mtajika huku akionyesha masikitiko usoni. "Sufuria yangu i wapi? Mtajika aliuliza kwa ukali. Sungura akamjibu "Ilikufa ikiwa inajifungua kwani chochote ambacho kina uwezo wa kuzaa pia hufa."*

**Umuhimu Wa Hekaya**

- Kutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja na kuwalaghai.
- Hufunza watu kuhusu matendo mema.
- Huonya dhidi ya upumbavu.
- Hufunza kuwa katika ulimwengu uliojaa hila na udanganyifu silaha ni maarifa,wema na maadilifu.

2. **Khurafa/Hurafa**

Ni hadithi zinazohusisha wanyama kama wahusika.

**Sifa**

- Huwa na wahusika wanyama.
- Wanyama hupewa sifa za binadamu.
- Wanyama huwakilisha binadamu wa kawaida.
- Huonyesha maadili katika jamii.

**Mifano**

**Kuchakulo na Nyani**

*Hapo kale, Kuchakulo alikuwa akiishi mahali palipokuwa na nyani wengi. Nao hao nyani walikuwa wamezoea kumcheka Kuchakulo kila alipopita karibu nao. Tabia hii ilimwudhi sana kuchakulo. Kwa muda, alikaa akifikiria njia ya kuwaadhibu nyani hawa. Siku moja jawabu likamjia. Akaenda mpaka mwituni ambako alipata zabibu tamu sana; akazitia katika mfuko mmoja. Katika mfuko ule ule akatia changarawe. Akaenda moja kwa moja mpaka mahali nyani walipokuwa wamekaa kwa furaha. Akaingiza mkono wake mfukoni na kuzitoa zabibu. Akazitafuna na huku akisema: "Haaa! Meno ya wavulana huzisaga hizi changarawe mpaka unga! Angalieni!"*

*Akazitoa zabibu na kuzitafuna.*

*Wale nyani kuona vile wakamwendea wakisema:*

*" Hebu tupe na sisi tusisage kwa meno."*

*Kuchakulo akaingiza mkono mfukoni na badala ya kuzitoa zabibu akatoa changarawe na kuwapa. Nyani kujaribu kutafuna wakaumwa na meno na kuzitema chini. Kuchakulo akaendelea kuzitoa zabibu kwa akili na kuzitafuna. Hao nyani waliiona hiyo ajabu, wakamwuliza kile kinachomfanya yeye aweze kutafuna kwa urahisi bila kuyaharibu meno na wakati wao hawawezi.*

*Kuchakulo kwanza alicheka kisha akayatema mate chini na kuwaambia "Msinichezee, mimi nimetahiri na ninyi bado. Meno ya mtu aliyetahiri ni magumu, na anaweza kutafuna hata mawe."*

*Akatoa zabibu tena, akizitafuna. Baru! Baru! Baru! Huku akiwaangalia nyani kwa dharau. Lo! Wale nyani wakashangaa sana. Wakaanza kuangaliana kisha wakamwuliza kuchakulo: "Sasa twambie tutafanyaje ili tuweze kutafuna zabibu kama wewe?"*

*Kuchakulo akawaambia: "Hakuna dawa nyingine ila kutahiri tu!"*

*Nyani wakamwambia awaletee ngariba wa kuwatahiri wawe kama yeye. Wakapanga siku ya kumleta huyo ngariba. Kuchakulo alimwendea chui na kumwambia: "Bwana chui, kila wakati nasikia wanitafuta uniue. Nikikupatia nyani uwafanye kitoweo chako utanifaa namna gani?" Chui akamwambia: "Mimi hupenda sana nyama ya nyani na ukinipatia hata mmoja urafiki wetu utadumu."*

*Kuchakulo na chui wakapanga mahali watakapokutana akiwa na wale nyani. Kuchakulo akawaendea nyani na kuwaambia: "Nimempata mtu hodari sana wa kutahiri na amekubali kufanya kazi hiyo bure ili awasaidie." Nyani kusikia hawatalipa kitu wakafurahi sana wakawaendea wengine na kuwapasha habari. Siku ile iliyopangwa na kuchakulo na chui ikaonekana inawafaa vile vile. Siku ilipofika kuchakulo alimwendea Chui kumwambia: "Nifuate."*

*Chui alimfuata mpaka mahali palipokuwa na pango lenye giza akaachwa ndani. Halafu, Kuchakulo aliwaendea nyani na kuwaleta kwenye uwanja uliokuwa karibu na pango lile. Walipokwisha kujipanga, Kuchakulo akawaambia: "Mtakuwa mkija mmoja mmoja mpaka yule wa mwisho."*

*Kuchakulo kaenda tena ndani ya pango na kumwambia Chui ajiweke tayari. Ikawa kazi ya Kuchakulo ni kumpelekea mmoja mmoja akiimba wimbo huu:-*

*"Vumilia, Vumilia*

*Huwezi kufa,*

*Vumulia, vumilia*

*Uondolewe utoto,*

*Hakuna kulia au kufanya kelele,*

*Vumulia tu ufanywe mtu mzima."*

*Kufika pangoni nyani aliingia peke yake na kuchakulo akaachwa mlangoni. Nyani alipofika ndani alimkuta Chui amejiweka tayari kumvunja shingo na kumtupa ndani kabisa mvunguni.*

*Mtindo huu uliendelea mpaka karibu kumfikia nyani wa mwisho. Kila wakati alipompeleka mmoja alikuwa akiimba wimbo ule wake. Walipokuwa wamebaki wawili tu wakamshuku kuchakulo.*

*Mmoja akamwambia mwingine: "Wewe ukifika mlangoni uangalie vile wale wenzetu wanavyofanywa ili tujue yanayofanyika."*

*Kuchakulo akaja tena na kumwambia: "Twende, unasitasita nini? Je, unaogopa?"*

*Yule nyani hakutaka kumwonyesha anashuku kitu. Kuchakulo akaanza: 'Vumilia, vumilia, Huwezi kufa…Heeeeeeeeeee! Huuuuuuuuuuu! Haraka twende!"*

*Yule nyani kufika mlangoni akasimama, akainama na kuangalia ndani. Kwa mwangaza kidogo akamwona Chui Mkubwa mwenye madoadoa ya manjano na meusi anamkodolea macho. Kuangalia uvunguni akawaona wale wenzake wote wamelala wamekufa fo! fo! fo! Akaondoka mbio mpaka alimpomwacha mwenzake na wote wakatimua mbio wakatokomea msituni Kuchakulo alijaribu kuwafukuza asiwapate akarudi kwa Chui. Chui akamshukuru sana akimpigapiga mgongoni na kumhakikishia kuwa urafiki wao utadumu.*

*Kuchakulo akamwacha Chui na mizoga ya nyani na kurudi nyumbani.*

*Wale Nyani wawili ndio waliowazaa nyani tunaowaona siku hizi, na tangu siku ile hawajadhubutu kumcheka tena kuchakulo*.

Mfano **2**

**Nyani na Mamba**

*Hapo zamani paliondokea nyani na mamba amboa walikuwa marafiki wa kufa kupona wallishi katika kijiji cha mla chake. Maskani ya mamba yalikuwa majini nayeo ya nyani yalikuwa mitini. Siku moja mamake maba aliugua maradhi yasyokuwa na tiba alipoenda kwa mganga alielezwadawa ilikuwa figo ya nyani. Aliprejea nakumsimulia nyani kuhusu masaibu ya mamake nyani alipigwa na mshangao na akajua maisha yake yamo hatarini. Alipanga safari ya kwenda katika kijiji kilochokuwa upande mwingine wa mto, alimjia rafikiye Mamba na kumjuza kwamba kuna figo nyingi upande ngambo ile nyingine na hivyo alimwomba mamba ambebe hadi wavuke mto ili akamchukulie figo.Mamba kusikia hivyo alimbeba hadi wakuvuka mto. Nyani alipovuka mto aliupanda mti uliokuwa karibu na akuonekeana tena*

**Umuhimu wa khurafa.**

- Humwezesha msimulizi na hadhira yake kusema mambo ambayo kwa kawaida ingekuwa muhali kuyatamka hadharani.
- Huwakashifu binadamu bila kuudhi mmoja kati ya hadhira.
- Husaidia katika kupiga chuku mambo yanayotendwa na binadamu na hivyo kuwakosoa.

-  Huwakilisha sifa za binadamu kama vile ulafi.

3. **Ngano za mazimwi**

Ni hadithi ambazo huwa na mazimwi kama wahusika wakuu. Zimwi ni kiumbe ambacho ni zao la akili ya binadamu. Zimwi linapofananishwa na bidanadamu, hupewa sifa fulani zinazojitenga na binadamu wa kawaida kama vile kuwa na jicho moja, mikono mingi na miguu kubwa ajabu.

**Sifa za mazimwi**

-  Ni ujumbe wa kuogofya.
-  Kila wanapopata nafasi huwatesa wanadamu.
-  Huwa na sifa zinazojitenga na wanadamu wa kawaida kama vile macho matatu.
-  Ni wenye uwezo kuliko binadamu.
-  Ni wajinga, binadamu huweza kuwashinda kwa sababu ya ujanja wao.
-  Kiwango cha taharuki ni cha juu.
-  Hujumuika na binadamu katika ndoa, densi na vita.
-  Ni wadanganyifu na huwa na akili ya binadamu.

**Umuhimu wa ngano za mazimwi**

- Huonyesha ubunifu wa binadamu, wanabuni mazimwi kwa mawazo yao.
- Kukemea ukatili katika jamii.
- Kuonyesha kuwa wema hushinda uovu kila mara.
- Kuhimiza moyo wa ushujaa.
- Kukaza uwezo wa kufikiri miongoni mwa watoto kupitia fantansia.
- Kuburudisha.
- Kusifu wema.
- Kuendeleza uhusiano katika jamii.
- Kuboresha uwezo wa kukumbuka.

**4. Ngano za usuli**

Husimulia visa vinavyoeleza asili ya vitu kimaumbile au hali fulani.

Aghalabu sifa fulani za ndege au wanyama huelezwa.

**Sifa za ngano za usuli**

- Huchukuliwa na wanajamii kuwa ukweli.
- Ni maarufu miongoni mwa jamii nyingi.
- Huonyesha uhusiano wa karibu sana kati ya binadamu na wanyama.
- Huwa na mwelekeo wa kihistoria.

**Umuhimu**

- Kueleza dhana ambazo ni nzito kueleza kisayansi.
- Kuelezea utamaduni wa jamii.
- Kukuza uwezo wa kufikiria.

Kwa mfano; kwa nini harage lina jicho moja?

Kwa nini fisi ana madoadoa.

**KWA NINI KUKU HUCHAKURACHAKURA**

*Hapo zamani palitokea kuku na mwewe .Ndege hawa walikuwa masaibu wakufa kuzikana . Waliishi pamoja kwa miaka na mikaka.Walishirikiana na kusaidiana kwa lolote lililotokea, la majonzi na la furaha. Walishirikiana katika kazi zote zilizowahusu. Kila mmoja wao alikuwa na bidii ya mchwa walipofanya kazi. Waligawana kazi mbalimbali na kuzifanya bega kwa bega. Kazi ya mwewe ilikuwa kutafuta chakula chao cha kila siku naye kuku alikuwa na wajibu wakuwatunza watoto wao. Alihitajika kuwapa chakula cha kutosha na kuhakikisha walitulia. Kuku pia alihitaji kuwaamsha wengine kulipokucha Ndege hawa waliishi pamoja kwa amani, utulivu na ushirikiano bila ya kukumbwa na tatizo lililowashinda kutatua waliahidiana kuwa wangekuwa marafiki; hadi kifo chao. Urafiki wao wa chanda na pete uliwafanya walale njaa nyakati zingine ili watoto wapate chakula cha kutosha. Sikumoja kuku na mwewe walialikwa katika karamu Fulani na ndege wenzao. Walitarajia kwenda karamuni pamoja na watoto wao. Mwewe aliandaa wanawe na kuhakikisha kuwa walikuwa tayari kwa karamu hiyo kubwa. Kuku aligundua kuwa vifaranga wake walikuwa na kucha ndefu zilizoonekana mbaya. Aliamua kumwomba mwewe wembe, "Tafadhali nipe wembe nikatie wanangu kucha,"*

*"Haya chukua.Hakikisha umeuregesha, la sivyo…"Alipoupokea wembe alimshukuru rafikiye kasha akaanza kukata kucha za vifaranga wake. Alikata kucha za vifaranga watatu vizuri lakini alipokuwa akimshughulikia wa nne, wembe ulimponyoka ukaanguka. Alijisemea kwa masikitiko, "Ole wangu mie, wembe wa mwewe nitaupata wapi?" Mwewe alipomaliza kujitayarisha alimwita kuku waende karamuni.Kuku aliyekuwa na wasiwasi alikataa kwenda huku akisingizia maumivu mwilini. Mwewe aliwachukua wanawe na kujiendea karamuni.Baada ya mwewe kuondoka, kuku alirudi nje na kuanza kuchakura chakura chini mahali alipokuwa akiwakatia vifaranga kucha. Alitafuta hadi*

*machweo bila kufuadafu. Mwenye wembe aliporejea alimwuliza,"Kulikoni ndugu kuku?"*

*"Ah, eh, wembe, wajua wembe wako u u u..."*

*"Wembe umefanya nini? Isijekuwa umeupoteza!"*

*"Kwa kweli ndio ume...potea"*

*"Aka!Hujui wewe huo wembe ni mmoja kama roho. Lazima nitwae fidia.*

*Nitawala vifaranga wako mmoja hadi uniregeshee wembe wangu."*

**5. Ngano za mtanziko**

Hadithi ambazo wahusika au mhusika hupambana na hali ambapo analazimika kufanya uteuzi mgumu yaani, kuna hali mbili au zaidi zilizo gumu. Huweza pia kuhusisha kufanya uamuzi fulani aghalabu kimaadili.

**Sifa za ngano za mtanziko**

- Huishia kwa swali ambalo mtambaji analiachia hadhira ijibu au iliwazie na kulitafutia uvumbuzi.
- Hukusudiwa kuipevusha jamii kwa kuikuza na kuendeleza uwezo wao wa kufanya uamuzi fulani.
- Huweza kuzua mijadala miongoni mwa wanajamii pamoja na kuukuza uwezo wa kushiriki kwenye majadiliano au mazungumzo ya kimjadala.

**6. Istiara**

Hadithi ambayo huwa na maana mbili; uwazi na ufiche. Ile maana wazi huificha maana ya pili ambayo kueleweka kwake huhitaji ufahamu fulani wa muktadha wa hadithi yenyewe. Wahusika na matukio yaliopo huwa kama mlinganisho wa hali nyinginezo huwa kama sitiari yaani vinasimamia watu halisi.

**7. Soga**

Ni hadithi ndogo ndogo zinazohusisha utani na ucheshi kwa kiasi Fulani kimsingi soga hutumiwa kwa akili ya kuchekesha, kukejeli au kuumbua au kufanyia dhihaka. Hata hivyo, katika ucheshi huo, mna mafunzo muhimu kwa binadamu.

**Sifa za soga**

- Wahusika huwa ni wa kubuni.
- Wahusika hupewa majina ya watu wanaopatikana katika jamii.

- Huwa na ukweli fulani unaowaumiza na unaowahusu wanajamii.
- Ucheshi au vichekesho vinavyotumiwa huwa muhimu kama njia ya kupunguza ukali wa ukweli uliomo.
- Hujengwa kwenye tukio moja.

  Kwa mfano;

*Katika kijiji kimoja paalishi Nafula na bintiye Esikoni. Esikoni alikuwa mrembo wa kupindukia na kila mvulana alitafuta mbinu ya kumtongoza, kwani ilikuwa muhali kumpata. Nafula alikuwa amemwonya mara kadhaa dhidi ya kucheza na wavulana. Siku ya Jumapili Adela ambaye alikuwa jirani wao aliamua kwenda kuazima kisu, kwa bahati nzuri, alikutana na Nafula akienda kanisani, akamweleza " Nafula nimetumwa nije uniazime kisu." Nafula akamweleza "Nenda umwambie Esikoni akupe." Adela akaenda mbio, kufika tu akamweleza Esikoni "Leo umeambiwa na Mamako unipe…" Esikoni akashangaa na kusagaa, akamwuliza Adela " Nikupe nini?" Adela bila kupoteza wakati akamwita Nafula kwa sauti kwani hakuwa ameenda mbali. " Nafula! Nafula-eee! amekataa!" naye Nafula akamjibu " Esikoni! Esikoni! mpeeee…"*

**Umuhimu wa soga katika jamii**

- Kukejeli matendo ya binadamu ambayo huwa na matokeo mabaya au yasiyofaa katika jamii.
- Huwaelekeza wanajamii kwenye mambo au tabia inayofaa au inachukuliwa kama msingi mzuri kwa matendo ya binadamu.
- Huwasilisha mafunzo fulani kuhusu matendo na tabia ya binadamu.
- Ni msingi wa burudani hata kutokana na utani na ucheshi wake.
- Huonyesha utani uliopo katika jamii.

**8. Mbazi/vigano**

Ni hadithi ambazo huwa za kimafumbo na mafunzo, hutolewa kwa kutumia kielelezo hasa wakati wa maongezi, zina wadhifa wa kama methali.

**Sifa za mbazi**

- Hutolewa kama kielelezo.
- Kusudi ni kumkanya, kuwelekeza, kuadhibu na hata kumfunza anayesikiliza.
- Hadhira hujifunza kutokana na masaibu yaliyowafika wahusika wa hadithi hiyo.
- Mifano kutoka bibiliani.

**Kwa mfano**

*Kulikuwa na mpanzi aliyetawanya mbegu, nyingine zikaanguka miibani na nyingine kwenye mawe na nyingine kwenye udongo wenye rotuba. Zilizoanguka kwenye mawe zililiwa na ndege, zilizoanguka miibani zikamea lakini zikabanwa na magugu na zilizoanguka kwenye udongo wenye rotuba zikamea zikazaa.*

**9. Ngano za kichimbakazi/ udhubahi**

Ni hadithi ambazo aghalabu hujifunza kwa matendo ya mhusika ambaye hukumbana na matatizo ya kila aina ambayo uhusisha matendo ya kimaumbile lakini mwishoe huishi maisha ya raha mfano katka bibilia Yohana kisa cha Nelson Mandela.

**Sifa**

Maajabu, uchawi, uganga, itikadi huchukua sehemu kubwa sana kisa maarufu za sinderela.

**10. Mchapo au kidahizo**

Huwa ni kisa kifupi kinachomhusu mtu au tukio fulani. Aghalabu wahusika wanaopatikana kitaka mchapo huwa na maana ya ziada.

**Pasta na mhumini**

*Siku moja Mritu alimwendea pasta amwombee ili apate bwana, pasta akamjuza awe akienda kanisani jioni kuomba na anapoomba asikize sauti ya "mungu" toka juu. Siku moja pasta alijificha darini akamsikiza Mritu akiomba ndiposa pasta akamjibu akiwa amebadili sauti yake "Toka nje na baada ya dakika kumi urejee utampata bwana wako ameketi humu kanisani" Mritu alitoka nje naye pasta akashuka toka kwa darini na kuketi pembeni. Mritu aliporejea alipigwa na butwaa kuona mungu amempa pasta.*

**B) NGANO ZA KIHISTORIA**

1. **Mighani/Migani**

Huzungumzia watu ambao ni mashujaa katika jamii.Walitenda matendo ya kishujaa, hutokana na watu waliowahi kuishi.

**Sifa za mighani.**

- Huzungumzia matukio ya kihistoria na wahusika waliowahi kuishi au wanaoaminiwa waliishi.
- Matendo ya wahusika hupewa sifa ambazo zinapita uwezo wa kawaida wa binadamu.
- Chuku hutumiwa katika utambaji wake.
- Huwa na ukweli wa kihistoria.
- Wanajamii wanaamini matendo ya mighani ni ya kweli.
- Kila jamii ina mighani yake.
- Aghalabu majagina huwa na siri ya nguvu na uwezo wao.
- Hatima ya wahusika huwa ni kifo kisicho cha kawaida.
- Majagina mara nyingi huwindwa na maadui zao.

**Umuhimu wa mighani**

- Ni njia moja ya kupitisha au kuitunza historian ya jamii
- Ni njia ya kutukuza matendo ya kishujaa
- Hutumiwa kukuza ujasiri na ukakamavu wa kijamii
- Huburudisha
- Huelimisha wanajamii kuhusu maisha
- Hufunza utamaduni
- Hukuza lugha
- Hufunza maadili ya jamii

**2. Visasili.**

Neno visasili huwa ni ufupisho wa visa vya asili. Ni sawa na visa viini. Hii hadithi hueleza chanzo cha mambo, yaani jinsi kitu au watu walivyopata kuwepo.

Sifa.

- Masimulizi ya kuelezea asili ya vitu, watu au matukio mbalimbali.
- Yaweza kuwa hadithi ya sasa au ya kale.
- Wahusika huwa binadamu au wanyama.
- Visa asili vinafungamana na imani ya kidini ya jamii, hasa hadithi zinazohusu asili ya watu; yaani jinsi kundi fulani la watu lilivyoanza.
- Kila jamii ina kisa asili chake na inakiamini.

**Umuhimu wa visasili**

- Hueleza utaratibu wa kutekeleza desturi kwa mfano, jinsi ya kutoa kafara
- Hueleza chanzo au asili ya tabia au hata watu fulani.

- Huhalalisha baadhi ya mila kwa mfano utoaji wa mahari.
- Husaidia katika kukitisha mizizi tabia fulani ya watu na vitu vinavyowazunguka.
- Huhimiza maadili ya jamii na imani zake.

**3. Shajara**

Hutumiwa kuelezea maelezo ya matukio au matendo ya mtu au watu fulani kwa mujibu wa kutoka kwake.

Shajara hueleza jinsi matukio hayo yanavyotokea kila siku .

Huwa ni hifadhi ya matukio kwa kutegemea siku hadi siku.

**4. Tarihi**

Ni hadithi fupi zinazosimulia matukio muhimu ya kihistoria. Matukio yanaweza kuwa ya huzuni au ya furaha. Lengo lake ni kuikumbusha jamii mambo yaliyotukia. Inawezekana matukio yanayosimuliwa yakawa ya kweli yaani yaliwahi kutokea.

**5. Kumbukumbu**

Ni neno linalotumiwa kuelezea maelezo au hadithi za matukio yanayohusishwa na jamii au mtu fulani. Kwa kiasi kikubwa, huwa pana mwelekeo mkubwa wa kuyaangalia maisha ya mtu huo au jamii hiyo yaani wasifu.

## UTANZU WA MAIGIZO

### Utangulizi

Maigizo/drama huwa mazungumzo yanayoambatana na matendo. Wahusika huigiza maneno, matendo na tabia ya watu fulani. Nia huwa ni kuburudisha na kupitisha ujumbe fulani. Maigizo hupatikana katika tanzu nyingine za fasihi simulizi ya kiafrika kama vile katika hadithi, mtambaji huambatana na matendo. Uigizaji pia hupatikana katika ushairi simulizi kama vile ngonjera, majigambo, tendi na mazungumzo kama vile soga, ulumbi na malumbano ya utani.

### Vipera Vya Maigizo

- michezo jukwaani
- Michezo ya watoto
- Vichekesho
- Matambiko
- Ngomezi

- Miviga

**Sifa za maigizo**

- Hutolewa mbele ya hadhira.
- Uigizaji huhitaji mandhari maalum ya utendaji.
- Hufungamana na shughuli za jamii kama vile mtambaji wa hadithi na sherehe za miviga kama jando, harusi na matanga.
- Sharti kuwe na tendo la kuigiza ambalo lina matendo ya watu na viumbe wengine kwa nia ya kuelimisha, kukashifu, kusifu na kuburudisha.
- Waigizaji wanavaa maleba yanayooana na hali wanayoigiza.
- Maigizo huigiza hali ya maisha ya jamii; kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kwa nia ya kuonyesha mafanikio, udhaifu na migogoro katika nyanja za maisha.
- Huwa na muundo mahususi na mtiririko wa matukio tangia mwanzo ukuzaji wa migogoro, kilele na usuluhishaji.
- Maigizo yaweza kuandamana na ngoma, pamoja na uimbaji au ukariri wa tungo za kishairi.

**Umuhimu wa maigizo**

- Huburudisha watazamaji na waigizaji wenyewe. Burudani hii mara nyingine hupumbaza.
- Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii kama vile upashaji tohara, matambiko, majigambo, ngoma, miviga na michezo ya watoto hudumishwa kupitia maigizo.
- Ni kitambulisho cha jamii; kila jamii ina Sanaa ya maigizo ya jamii husika. Miviga na sherehe za arusi na mazishi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.
- Hukuza umoja na ushirikiano wa watu wanapojumuika kushiriki katika maigizo. Hao hujitambulisha kama jamii moja.
- Ni nyenzo za kupitisha maarifa na amali za jamii kupitia michezo ya jukwaani.
- Husawiri mtazamo wa jamii kuhusu masuala mbalimbali kama vile woga, wizi na usaliti.
- Hukuza ubunifu madhalan watoto wanaposhiriki michezo ya watoto, hujifunza kubuni michezo wakiwa wachanga na pia Sanaa ya uigizaji.
- Hukuza kipawa cha uongozi katika michezo, huweza kujifunza stadi za uongozi
- Ni njia ya kuimarisha urafiki. Kwa vile mizaha na utani katika malumbano hukuza urafiki na uhusiano bora

- Huongoza jamii kupambana na na mazingira wanamojipata. Kutegemea imani ya wanajamii,matambiko yanaweza kuondoa matatizo katika jamii kama vile njaa, ugonjwa na ukame kwa kuomba Mungu
- Maigizo huelimisha kupitia maudhui na hulka za waigizaji na kushauri nafsi zao, kuiga au kukashifu hulka hizo.

1. **Malumbano ya utani/mchongoano**

Ni kufanyiana dhihaka ili kuchekesha watu. Wanajamii wanaweza kutaniana kwa namna ifuatayo:

Utani wa mababu/mabibi na wajukuu.

Utani wa marafiki.

Utani wa ukoo /makabila.

Utani wa rika moja.

**Sifa za malumbano ya utani**

Malumbano ya utani hufanywa na watu wawili au makundi mawili ya watu wanapokutana hata hivyo, kila utani una msingi na mpaka wake.

Watu wenye uhusiano mzuri ndio hutaniana, watani hufanya mizaha ambayo inadhibitishwa na masharti yanayotawala uhusiano wao. Baadhi ya makabila hutaniana mazishini.

Malumbano ya utani inaweza kuwa kati ya makabila, marafiki, wajukuu na mababu, wajukuuu na mabibi, bwana na bi harusi. Katika malumbano ya utani, mbinu ya chuku hutumiwa kwa kiasi kikubwa, mbinu hii hunuiwa kusisitiza sifa fulani au kukejeli sifa fulani wazi. Malumbano ya utani yanaweza kuwa hata na masimango.

Huchukua njia ya ushindani, kila mmoja akijaribu kumpiku mwenzake.Wakati mwingine watu hutania wasiokuweko, utani wa aina hii huandamana na uigizaji wa kuchekesha.

**Umuhimu wa malumbano ya utani**

a) Hutoa maadili kwa hivyo mila na desturi za jamii huwapa baadhi ya watu katika jamii jukumu la kutaniana na wengine kwa sababu maalum.
b) Malumbano hupunguza urasmi miongoni mwa wanajamii, hivyo huhimiza kujieleza kwa urasmi bila kuficha.

c) Huimarisha urafiki, ni watu walio na uhusiano mwema tu wanaoweza kutaniana.
d) Hukuza utangamano miongoni mwa watu na makabila mbali mbali hasa wanapokuja pamoja kutaniana.
e) Hutambulisha jamii kwa kutaja baadhi ya sifa zake katika utani k.m unaweza kumtania mtu mchoyo, hivyo kumtaka ajirekebishe.
f) Hukosoa na kukashifu tabia hasi baadhi ya malumbano ya utani hudhihaki ulafi, uchoyo, wivu na tabia nyingine mbaya.
g) Huburudisha, ucheshi katika malumbano ya utani huburudisha na kuchangamsha.
h) Huelimisha, kupitia malumbano ya utani, watu hupata maarifa ya kukabiliana na hali mbalimbali maishani.

Mfano wa utani

**Mtu A**: *Wasee wasee unacheki huyu msee kwao ni wengi hadi wakipika chapo wanatoa photocopy*

**Mtu B***: Wasee wasee unacheki huyu msee amezeeka hadi ako na phone number ya Abraham wa bibilia.*

**2. Ulumbi**

Huu ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee, ni utangulizi wa lugha kwa mvuto na ufasaha. Ulumbi huwezesha mtu kulieleza jambo la kawaida kwa namna ambavyo linaonekana kuwa geni kabisa na kuwashawishi watu kulikubali au kulipenda.

**Kuna aina mbili za ulumbi**

Ulumbi rasmi
Ulumbi usio rasmi
Ulumbi rasmi unaweza patikana katika miktadha ifuatayo;

a) Kortini, ambapo mawakili hutoa hoja zao kuwatetea wanaowawakilisha.
b) Kanisani au msikitini, kanisani ambapo wahubiri wanatoa sala.
c) Mijadala ya kisiasa ambapo wanasiasa wenye vipawa vya ulumbi huvitumia kuwapiku wanasiasa wenzao na kuwashawishi raia kuwapigia kura.
d) Katika sherehe za arusi au mazishi k.m katika kutoa taabili; maelezo yanayotolewa kuhusu aliyeaga.
e) Katika kuapiza na katika kufukuza pepo.
f) Katika utoaji wa risala.

Ulumbi usio rasmi unaweza kupatikana hali zote zisizo rasmi. K.m vile mazungumzo ya kupitisha wakati; kuapiza, kulaani, kushauri, baina ya wanafunzi n.k

**Sifa za ulumbi**

1. Mlumbi hutumia lugha kwa njia ya kuvutia na kushawishi hadhira yake
2. Ulumbi hubainika katika miktadha ya kutoa hotuba au katika hali ambapo mtu anahitajika kutetea msimamo wake katika vikao au hata katika mijadala rasmi
3. Hukuza ukakamavu wa kuzungumza hadharani, mlumbi hupenda kuzungumza na hupenda kujisikia akizungumza mbele ya watu.
4. Hutumia vipengele anuwai vya lugha k.v sitiari, maswali ya balagha, methali, nahau, taswira na pia viziada lugha kama vile toni ili kuishawishi hadhira au kutilia mkazo wazo fulani na kutetea misimamo yao, hutumia lugha kutegemea muktadha na hadhira yake.
5. Katika baadhi ya jamii, walumbi walitumika kuzungumza kwa niaba ya viongozi kama maehifu, wanaoomba posa au kwa niaba ya ukoo au mwanajamii aliyedhulumiwa. Walumbi wengi aghalabu huwa na vipawa vya uongozi na huinukia kuwa viongozi wa jamii zao.
6. Ulumbi husisitizwa sana katika matabaka ya juu kama kitambulisho cha tabaka hilo, baadhi ya jamii, watu katika tabaka tawala walifunzwa kutumia msamiati wenye haiba, matumizi ya ishara, toni na sauti zifaazo, hili lilinuiwa na kuimarisha stadi za ulumbi.
7. Walumbi hutumia chuku kwa kiasi kikubwa hata hivyo, lazima wadumishe adabu.

**Umuhimu Wa Ulumbi**

1. Hukuza uwezo wa kujieleza hadharani, kadri mtu anavyozungumza hadharani, ndivyo anavyojiboresha kama mlumbi
2. Ni nyenzo ya kukuza ujuzi na ufasaha wa lugha, jinsi mtu anavyoitumia lugha kwa ugwiji, ndivyo anavyokuza umairi wake wa kuisarifu lugha.
3. Ni msingi wa kuteua viongozi, uwezo wa mtu kuwashawishi wanajamii kukubaliana na mtazamo wake humfanya kutambuliwa kama mwenye uwezo wa kuongoza jamii. Walumbi wana uwezo mkubwa wa kuishawishi hadhira.
4. Huhifadhi utamaduni wa jamii, ulumbi ni sanaa jaadia, imekuwepo katika jamii kwa muda mrefu, ikipokezwa vizazi na vizazi.
5. Ni nyenzo ya kuburudisha wanajamii na kuwaelimisha bila kuwachosha, walumbi huweza kupitisha maarifa mbali mbali kwa wanajamii kwa njia yenye mvuto.

6. Hukuza uzalendo, vijana wanaposikiza walumbi wakitongoa lugha, huionea fahari lugha yao na kujitambulisha zaidi na jamii zao.
7. Huweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu au ulio na athari kubwa au ambao una makali na usio rahisi kueleza.
8. Ni kitambulisho cha utabaka, katika baadhi ya jamiii ulumbi ulihusishwa zaidi na tabaka tawala au watu wenye vyeo vya juu na heshima katika jamii zao. Katika jamii hizi ulumbi ni kigezo cha kuainisha matabaka.
9. Ulumbi ni msingi wa kuheshimiwa katika jamii, walumbi huheshimiwa kwa sababu ya matumizi ya lugha yenye ubingwa na ustadi katika kuyafafanua maswala ya jamii.

**3. Hotuba**

Ni maelezo au taarifa itolewayo mbele ya hadhira kuhusu mada fulani, kwa kawaida hotuba ni mazungumzo rasmi kama vile:

1. Hafla za kisiasa (hotuba za wanasiasa)
2. Kanisani au msikitini (mahubiri)
3. Sherehe za kitamaduni k.v vikao vya posa.
4. Kortini kabla jaji hajatoa hukumu, anaweza kutanguliza hotuba.
5. Kwenye mazishi (taabili) taadhiri na risala za rambirambi.
6. Katika harusi mawaidha yanayotolewa kwa maarusi huchukua muundo wa hotuba
7. Katika tamasha za muziki na ukariri wa mashairi au mashindano ya utoaji hotuba.

**Sifa za hotuba**

1. Kwa kawaida, hotuba hutolewa na watu maalumu au walioteuliwa kuzungumza k.v viongozi au wawakilishi wao na watu wengine wenye hadhi katika jamii. Hata hivyo, baadhi ya hotuba hutolewa katika miktadha isiyo rasmi, katika makazi ya watu hotuba za mawaidha (waadhi) nasaha huweza kutolewa wakati wa chajio au baada ya chajio
2. Watu wanaoteuliwa kutoa hotuba aghalabu huwa na umilisi mkubwa wa lugha, walumbi ni watoaji hotuba na wana stadi za kutoa hotuba zao hadharani.
3. Hotuba hutolewa kwa nafsi ya kwanza.
4. Mtoaji hotuba anaweza kutumia viziada-lugha kama vile ishara za uso na mikono ama miondoko ili kufanya hotuba ivutie hadhira, maswali ya balagha pia hutumika
5. Hotuba huteuliwa mada mahususi wala haizungumzii jambo lolote lile.

**Umuhimu wa hotuba**

1. Huadilisha na kuasa, hotuba zinazotolewa jandoni au arusi kwa kawaida hunuiwa kutoa nasaha
2. Huelimisha, hotuba za jandoni kwa mfano huwapa vijana maarifa ya kukabiliana na maisha.
3. Huimarisha ukakamavu wa kuzungumza hadharani, kadri watu wanavyotoa hotuba ndivyo wanavyoimarisha umilisi wao wa lugha na ujasiri wa kuzungumza hadharani.
4. Hukuza ufasaha na umilisi wa lugha
5. Hupalilia kipawa cha uongozi, kwa kawaida mahatibu huteuliwa kadri mtu anavyochukua jukumu la kuhutubu katika hafla mbalimbali, ndivyo anavyojitayarisha kuchukua nyadhifa kubwa zaidi za viongozi.

**4. Mawaidha**

Haya ni mazungumzo yanayotolewa yanayompa mtu ushauri au nasaha kuhusu jambo fulani, mawaidha hutoa mwongozo na maelekezo ya kukabiliana na changamoto katika maisha na jinsi ya kuhusiana na wanajamii.

**Sifa za mawaidha**

1. Mawaidha hutolewa katika miktadha mbalimbali; rasmi kama vile jandoni, katika arusi, kwenye maisha darasani na kanisani. Hata hivyo, mawaidha yanaweza kutolewa katika miktadha isiyo rasmi kama vile mzazi anaweza kumpa mwanawe mawaidha nyumbani wakati wa chajio.
2. Katika jamii nyingi, wazee na watu walio na vyeo vikubwa na waliochukuliwa kuwa na hekima ndio waliowapa vijana mawaidha. Hata hivyo, vijana pia wanaweza kutoa mawaidha kwa vijana wenzao wanaohitaji ushauri au pia vijana wanaweza kutoa mawaidha kwa wazee.
3. Hutolewa zaidi kwa wadogo, ambao wanaaminika kuwa wanahitaji kupewa mawaidha maishani. Hata hivyo, yanaweza kutolewa kwa yeyote anayehitaji
4. Mwenye kutoa mawaidha analielewa jambo analowosia kwa undani lazima awe na ujuzi wa kutosha katika mada anayozungumzia.
5. Mwenye kutoa mawaidha hutumia lugha inayoathiri hisia za wanaowosiwa inaweza kuwa na tamathali za usemi kama vile methali.

6. Mawaidha huingiliana na vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile methali hufumbata mawaidha pia utambaji ngano, miviga kama vile jando na arusi huandamana na utoaji wa mawaidha aidha yapo mashairi ya waadhi halikadhalika anayetoa mawaidha anaweza kutumia mbazi/vigano ili kusisitiza ushauri anaotoa.
7. Maudhui katika mawaidha ni mapana yaani huweza kugusia maswala kama dini, uongozi, ujasiriamali, elimu na taaluma, unyumba, mahusiano ya kijamii, malezi na afya.
8. Mawaidha yanayotolewa katika miktadha rasmi mbalimbali huwa na muundo maalum yenye sehemu tatu kuu:

i) **Utangulizi**, katika sehemu hii anayetoa mawaidha huanza kwa kauli ya kuvuta makini ya hadhira anaweza kuanza kwa kutoa kiini cha mawaidha, kwa mfano utu uzima huenda na uwajibikaji… baadaye anaelezwa anayofaa kufanya

ii) **Uwili,** mawaidha huwasilishwa na kusisitizwa kwa kutumia kauli sisitizi na tamathali za usemi kama vile methali, tashbihi, istiara hutumika kuwosia, maonyo na maelekezo hutolewa kutegemea lengo

iii) **Hitimisho**, mwasilishaji huonyesha msimamo wake kuhusiana na swala analowosia kwa kawaida anayetoa mawaidha huishirikisha hadhira kwa kutaka kujua msimamo au maoni yao kuhusu swala alilowawosia, hadhira inaweza kutaja changamoto zinazohusiana na wosia unaotolewa.

9. Anayetoa mawaidha hutumumia mambo mengi kupitisha mawaidha hayo k.m miondoko ya viungo au ishara, kubadilisha kasi ya kuzungumza na pia kudondoa sehemu za watu maarufu.

**Majukumu ya mawaidha**

1. Jukumu la mawaidha ni kuelekeza, mawaidha hutoa mwongozo wa jinsi ya kukabiliana na matatizo au jinsi ya kutenda jambo fulani.
2. Huelimisha, mawaidha huwapa wanajamii maarifa ya kuendesha maisha, huwajuza wanajamii kuhusu majukumu ya kijamii na matarajio ya jamiii zao kwao.
3. Huadilisha wanaopewa mawaidha hujifunza maadili kama vile usafi, unyenyekevu, utulivu na kusamehe.
4. Hutambulisha jamii, kila jamii huwa na aina yake ya mawaidha kulingana na thamani zake pia mawaidha hutolewa kwa namna mbalimbali kutegemea jamii.
5. Husaidia kuondoa ujinga katika jamii, huadilisha waliopotoka na kufanya mabaya.

6. Husaidia kuwapa ukakamavu wasio nao na kuwaongezea wengine ujasiri na stadi za kimaisha.
7. Huwaandaa watu kushiriki ipasavyo katika shughuli za kitamaduni, kijamii na kadhalika.

**Mfano wa mawaidha**

*1. Owa , sandame hadaa, moyo ukahadaiwa*
*Owa, anaye kufaa, mke mwenye kusifiwa*
*Owa, upate kuzaa, kama ulivyozaliwa*
*Owa, ukijaaliwa, mupendane na mkeyo*
*2. Owa, aliye na kheri, muandamane kwa dini*
*Owa, yai la johari, litiye nuru nyumbani*
*Owa, mdomo mzuri, ukupandie lisani*
*Owa ungiye nyumani, mupendne na mkeyo*
*3. Owa, moyo wa imani, wazumbua majuja*
*Owa, susiowe duni, anayeitwa kioja*
*Owa, mtenda ya dini, ndiye mke mwenye haja*
*Owa, utungiwe koja, mupendanena mkeyo.*
*4. Owa, usiowe tambara, linukiyalo vibaya*
*Owa, mwanamke jura, umjunze yenye ndiya*
*Owa, usiowe sura, kutakakuzangaliya*
*Owa, mzuritabiya, mupendane na mkeyo*
*5 Owa, akukubaliye, akuizao siowe*
*Owa, upendanenaye, zamani sizo ujuwe*
*Owa, akuridhiyaye, mujikubali wenyewe*
*Owa, mukae mutuwe, mupendane na mkeyo*
*6 Owa, utukuze cheo, na jina lipate kuwa*
*Owa, upate mkeo, aambiwe meolewa*
*Owa, kama waowao, moyo usiliye ngowa*
*Owa, ujue kuhuwa, mupendane na mkeyo.*

**ZOEZI**

**1.a) Eleza sifa za mawaidha zinazojitokeza**

*Inaandamana na miviga; arusi au ndoa*

*Maudhui ya ndoa yanaonekana wazi*

*Inatolewa kwa wadogo; wale ambao bado hawajaoa*

**b). Utungo huu unaweza kutolewa katika muktadha upi?**

*Unaweza kutolewa kwa mtu anayetarajia kuoa*

**c.)Eleza mawaidha yanayotolewa kuhusiana na ndoa.**

*Mtu anafaa amwoe mke ambaye wanapendana naye.*

*Oa mwanamke ambaye anaheshimu dini*

*Oa mwanamke mwenye tabia njema*.

**2.a) Taja miktadha mitano ya kutoa hotuba**

*Katika mikutano ya kisiasa. Katika sherehe za kibinafsi*

*Katika mikutano shuleni.katika kusoma bajeti.*

*Viranja wakiongea kwa wanajunzi.*

**b) Eleza majukumu manne ya mawaidha.**

*Mawaidha huelimisha wanajamii*

*Pia husaidia kuondoa ujinga katika jamii*

*Huwaandaa watu kushiriki katika shughuli za kitamaduni*.

*Husaidia kuwapa watu ukakamavu katika  wasauyayo*

5. **Soga.**
   Rejelea soga katika hadithi

   Soga ni mazungumzo yanayonuiwa kupitisha wakati

6. **Maapizo**
   Maapizo ni maoni maalum ya kumtaka mungu, miungu na mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani na mwovu. Hivyo maapizo ni dua yaa laana au maombi mabaya kutoka kwa mtu anayehisi ametendewa wovu au amesalitiwa na mwingine.

   **Sifa za maapizo**

1. Maapizo yalitolewa na watu walioenda kinyume na matarajio ya jamii zao mifano ya watu hawa ni wabakaji, wezi, wauaji na waliowatusi wazazi, wazee au ukoo.Wazazi pia huweza kutoa maapizo kwa wana wao ili kuwaonya dhidi ya hulka mbaya kama vile utumiaji wa vileo.
2. Katika baadhi ya jamii za kiafrika, maapizo yalitolewa kabla ya ulaji viapo.mlaji kiapo anaweza kusema *ambaye amefanya tendo hili chuma hiki kimwingie kwenye mboni ya jicho,asiuone mwangaza wa jua tena*
3. Maapizo yanaweza kutolewa moja kwa moja na yule aliyeathirika, mtu anapopoteza kitu chake anaweza kuapiza ili kumtisha aliyeiba k.m *aliyeiba mbuzi wangu apepenuke na huo mchanga, zizi lake asiweze kulala mbuzi hata mmoja*
4. Kidini, Mungu, miungu au mizimu huweza kutoa maapizo kuhusu mustakabali wa mhusika fulani aidha maapizo ya kidini yanaweza kutolewa kama laana baada ya mhusika kukaidi amri za Mungu au miungu, maapizo ya aina hii huathiri mhusika na jamii yake.
5. Maapizo huaminika kuwa yataleta maangamizi kwa jamii, hivyo wanajamii hushauriwa kuyaepuka kwa kutenda mema.
6. Maapizo hutumia fasaha k.m ulumbi watoaji maapizo katika ulaji wa aghalabu huwa walumbi.
7. Maapizo hutumia lugha kali inayonuiwa kujaza woga ili kuonya dhidi ya uovu.

**Umuhimu wa maapizo**

1. Kimsingi, maapizo hutumiwa kama nyenzo ya kawaonya wanajamii dhidi ya matendo hasi
2. Hutambulisha jamii, kila jamii ina namna yake ya kuapiza, na mitindo tofauti ya kutoa maapizo.
3. Hukuza umoja katika jamii, kuweka na kaida au miiko sawa huwafanya watu kujihisi kuwa kitu kimoja.
4. Huadilisha, wanajamii hujifunza kutenda mema ili kuepuka laana.

**Mfano wa maapizo**

*Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,*

*Nami ndiye nilompa uhai mwana unoringia,*

*Anakufanya upite ukinitemea mate,*

*Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,*

*Mzimu na waone uchungu wangu,*

*Radhi zao wasiwahi kukupa,*

*Laana wakumiminie,*

*Uje kulizwa mara mia na wanaa,*

*Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,*

*Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,*

*Wakaza mwanao wakuuguze katika utu uzima wako!*

**MASWALI**

1. **Msemaji ni nani katika utungo huu?**
*Mzazi –mkwe*

**2. Fafanua sifa tatu za anayeelekezewa maapizo haya**

*Mwenye majivuno, anaringa kupitia mwana wa msemaji*

*Mchoyo, anamnyima msemaji chakula hata wakati wa kuwa na wajukuu wake.*

*Mwenye dharau, msemaji anasema kuwa anayerejelewa anapita akimtemea mate.*

**3. Andika mifano ya maapizo katika miktadha ifuatayo.**

**a) Dini-** *kwa dharau uliomwonyesha mtumishi wa jalali na asikujalie mema uishipo duniani humu*

b) **Familia**-*yule atakayepuuza amri zangu kama kicwa cha familia hii, asiweze kukuza familia yake mwenyewe.*

c**) Kijiji** *–aliyeiba matunda shambani mwangu, na matunda hayo yawe mwisho kuyala, atambae njaa mpaka atakapokabiliana na ziraili wake.*

d) **Darasani**-*aliyeniibia kalamu zangu na asipite mtihani wake wa mwisho wa mwaka*.

**4. Eleza majukumu ya maapizo yanayojitokeza katika tungo**.

*Unaadilisha msemaji anakashifu tabia hasi zilizo kwa mkazamwana wake.*

7. **Ngomezi**

- Ngomezi ni fasihi ya ngoma.

- Midundo na mapigo fulani ya ngoma ubainisha maana na ujumbe maalum kutengemea jamii.

**Sifa za ngomezi**

- Ujumbe huwa umefichika ile hali ya midundo na mapigo ya ngoma.
- Mapigo na midundo hii hufuata toni na wizani (ridhumu) kwa mujibu wa lugha ya wahusika au jamii husika.
- Ujumbe huweza kueleweka na kutafsiriwa na wanajamii au hadhira iliyonuiwa. Hulenga hadhira teule.
- Kila utaratibu wa ngoma hubainisha suala tofauti na ula mwingine Kutegemea mapigo huweza kutofautisha baina ya habari za kutangaza hatari ya vita, harusi, au kifo cha kiongozi.
- Huweza kuwasilisha ujmbe wa dharura kwa njia ya haraka na ambayo si ghali ikilinganishwa na njia zingine.
- Ngomezi huongozwa na watu teule katika jamii ili kuhakikisha kuwa hakuna kutuma ujumbe unapotosha au kuwasilishwa visivyo.
- Ngomezi vilevile hutolewa wakati maalum mfano vita au vifo kitokeapo.

**Udhaifu wa ngomezi**

- Si kila mtu katika jamii atapata kutafsiri ujumbe vyema.
- Ngoma pia husikika kwa idadi ndogo tu ya watu wanaoishi pengine katika kijiji kimoja.
- Mapigo na midundo yanaweza kuhitilifiana na hivyo kuwasilisha ujumbe amboa haukukusudiwa.
- Utanzu huu haujachunguzwa kwa kina na huenda ukapotea bila kuacha kumbukumbu ridhishi endapo utafiti hautaendelezwa.
- Hubagua wageni wa jamii husika na vilevile wasio na uwezo wa kusikia. Sio rahisi kutia mpaka baina ya habari moja na nyingine.

## USHAIRI SIMULIZI

### Utangulizi

Ushairi simulizi ni utanzu unaojumuisha tungo zote zenye mapigo ya kimuziki, mawazo, hisia na hoja katika utanzu huu huwasilishwa kwa njia ya mdomo kutumia lugha ya mkato yenye mpangilio maalumu wa maneno katika mishororo. Ushairi simulizi huimbwa, hughaniwa au hukaririwa ni muhimu kutaja hapa kuwa ushairi simulizi hutofautiana na mashairi ambayo huandikwa kwa lengo la

kuwasilisha mbele ya hadhiri katika mashindano ya tamasha za muziki au yanayowasilishwa katika hasia maalumu.

**Sifa Za Ushairi Simulizi**

1. Ushairi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo mbele ya hadhira kwa kukaririwa, kughanwa au kuimbwa. Nyimbo kwa mfano huimbiwa watu hata hivyo, baadhi ya mashairi huimbwa na watu bila kuhusisha hadhira nyimbo za kazi mara nyingi hazina hadhira.
2. Hubuniwa papo hapo na kuwasilishwa kwa hadhira au tungo za awali huwasilishwa kutoka kwa kumbukumbu za mwasilishaji.
3. Tungo za mashari simulizi hutolewa zikiambatana na ala za muziki, uimbaji wa nyimbo huambatana na ala kama njuga na marimba aidha anayejigamba huweza kutumia ala kama vile mkuki anapojigamba.
4. Ushairi simulizi ni sehemu ya utamaduni wa jamii na hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, nyimbo za jandoni (nyiso) na tendi, kwa mfano hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
5. Ushairi simulizi hutumia lugha yenye mvuto mkubwa, yenye mapigo yaliyopangwa kwa muwala na urari.
6. Utungo wa ushairi simulizi huweza kuwasilishwa na mtu mmoja kama ilivyo katika majigambo au kundi la watu kama vile nyimbo nyingi na ngonjera.
7. Ushairi simulizi hubadilika kulingana na anayeuwasilisha, hadhira na wakati.Wimbo mmoja unaweza kuimbwa kwa mahadhi mbalimbali kulingana na mwimbaji, mwasilishaji anaweza kubadilisha wimbo au shairi wakati wa kuimba, kukariri au kughani kutegemea hadhira yake.
8. Hadhira huweza kushiriki katika uwasilishaji wa mashairi simulizi, mwimbaji, kwa mfano, anaweza kuishirikisha hadhira yake katika uimbaji kwa kupiga makofi.
9. Uwasilishaji wa mashairi simulizi, kwa kawaida huandamana na uigizaji. Mwimbaji kwa mfano huambatanisha maneno yake na vitendo kama vile ishara za uso, ishara za mkono, miondoko mbalimbali na upigaji makofi.
10. Ushairi simulizi hufungamana na shughuli au muktadha maalumu mathalani nyimbo hufungamana na shughuli tofauti tofauti kama vile:

i) **Hodiya**-nyimbo za kazi.
ii) **Kimai**-nyimbo za uvuvi na shuguli za majini.
iii) **Mbolezi**-nyimbo za kuomboleza/matanga.
iv) **Wawe**-nyimbo za kilimo.

11. Ushairi simulizi una miundo mbalimbali, unaweza kuwa na beti zilizo na kibwagizo kila ubeti unaweza kuwa na idadi tofauti tofauti za mishororo, kama vile 2,3,4,5,6,7 na zaidi.
12. Ushairi simulizi unaweza kuwa na urari wa vina na mizani au ukakosa kuwa nao, kilicho muhimu zaidi ni mapigo ya muziki yanayofanya utungo huo uweze kuimbika.
13. Ushairi simulizi, kama tanzu nyingine za fasihi simulizi hutumia lugha ya kitamathali, kunaweza kuwa na misemo, nahau, methali, ishara, taswira, jazanda na istiara.

**Uainishaji wa ushairi simulizi**

Mashairi simulizi yanaweza kuainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali kam vile.

**1. Maudhui**

**a)** Mapenzi-hupitisha jumbe za mapenzi.

**b)** Kutuliza-kuna nyimbo za bembea au bembelezi zinazowatuliza watoto.

**c)** Kuomboleza-mbolezi huimbwa wakati wa msiba.

**d)** Kusifu-sifa huimbwa kujisifu mashujaa au waliofaidi umma na kustahili kutambuliwa.

**e)** Siasa-nyimbo za siasa huwasilisha jumbe za kisiasa.

**2. Muktadha au mahali pa uwasilishaji**

a) Nyiso-nyimbo za jandoni.

b) Mbolezi-zinazoimbwa kwenye mazishi au kwenye maombolezi.

c) Nyimbo za harusi.

d) Nyimbo za matambikoni ambazo hutolewa wakati wa kutoa kafara au sadaka kwa mizimu, labda baada ya janga.

e) Nyimbo za kazi.

3. **Mtindo wa uwasilishaji**

a) Maghani hutolewa kwa kalima bila kuimbwa.

b) Nyimbo huwasilishwa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka.

c) Shairi utungo unaokaririwa.

d) Tendi au Rara husimuliwa kwa mapigo ya kishairi.

e) Ngonjera huwasilishwa kwa kujibizana.

4. **Mwasilishaji**

a) Majigambo huwasilishwa na anayejigamba

b) Kwaya uimbaji wa watu wengi

**Umuhimu Wa Ushairi Simulizi**

Ushairi simulizi kama kipengele cha fasihi simulizi una umuhimu wa kijumla licha ya kuwa kuna vitanzu mbalimbali vinavyotekeleza majukumu tofauti. Majukumu ya ushairi simulizi hutofautiana kutoka jamii hadi jamii, hata hivyo kuna majukumu ya kijumla kama vile

a) Ushairi simulizi hutumiwa kupitisha maarifa au mafunzo ya jamii fulani nyimbo za jandoni, za harusi na dini hutumiwa kupitisha mafunzo maalumu.

b)Ni nyenzo ya kuhifadhi na kupitisha utamaduni na historia ya jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa mfano, tendi zinazosifu mashujaa huendeleza historia ya jamii hiyo kwa kuonyesha matukio kama vile nyimbo za jandoni (nyiso) husawiri utamaduni wa jamii kuhusu jando na kuuhifadhi.

c) Hukashifu tabia hasi kwa nia ya kuhimiza urekebishaji wa tabia hizo nyiso kwa mfano, hukashifu woga, hivyo vijana waoga huhimizwa kujirekebisha. Maghani na nyimbo za kisiasa hukashifu tawala dhalimu.

d) Ni nyenzo kuu ya kukuza umoja na uzalendo miongoni mwa wanajamii kupitia kwa nyimbo zinazosifu mashujaa wa vita, huhimiza vijana kuzionea fahari jamii zao na kujitoa mhanga kuzitumikia aidha wanajamii wanapojumuika pamoja kuimba au kughani katika hafla fulani, hujihisi kuwa kitu kimoja, hivyo uzalendo hujengeka.

e)Ni nyenzo ya kutakakasa hisia kupitia kwa mashairi au nyimbo, watu hutoa hisia za moyoni na kutakaza nyoyo zao mfano mwafaka ni nyimbo na mashairi ya mapenzi ambayo kwayo mtu humtolea mpenzi wake hisia. *Rara* pia hutumiwa kutekeleza jukumu hili.

f) Huelimisha, hukosoa na kurekebisha jamii nyimbo hutoa maadili ya kuonya na kuelimisha wanajamii nyimbo au mashairi ya sifa, tendi hata mbolezi huonyesha matendo mazuri ya anayeimbiwa na kukashifu wanaoenda kinyume na matakwa ya jamii.

g) Husawiri mfumo wa jamii fulani kisiasa, kiuchumi na kijamii baadhi ya nyimbo huonyesha shughuli za kiuchumi za jamii kama vile ufugaji. Hodiya (nyimbo za kazi) huonyesha shughuli mbalimbali kama vile uwindaji, kilimona uvuvi. Majigambo pia husawiri mifumo ya jamii kisiasa na kijamii.

h) Huonyesha falsafa na imani za jamii husika kuhusu masuala fulani. Mbolezi huonyesha imani za jamii kuhusiana na kifo. Majigambo husawiri falsafa ya jamii kuhusu ushujaa.

i) Ni nyenzo kuu ya kuhamasisha wanajamii. Nyimbo za kisiasa na kizalendo zimetumiwa na tawala kama nyenzo ya kueneza propaganda za kisiasa.

j) Hukuza ubunifu anayekariri, huimba au kughani mashairi huhitajika kubuni mbinu zifaazo za uwasilishaji. Kwa kufanya hivi, uwezo wake wa kubuni hukuzwa.

k) Hukuza usanii wa lugha wanaotunga na kuimba mashairi huhitajika kubuni mbinu zifaazo za uwasilishaji kwa kufanya hivi, uwezo wake wa kubuni hukuzwa.

l) Husaidia wanajamii kukabiliana na hali ngumu na kuwahimiza wasikate tama kwa mfano mbolezi husawiri na kusawiri kifo kama faradhi kwamba humfika yeyote, hivyo hisia za mwemeo hupungua aidha nyimbo huhimiza waliokwenda vitani au wanaofanya kazi wasikate tamaa.

m) Ushairi simulizi hustarehesha na kufurahisha wanajamii tungo za ushairi simulizi huvutia hisia, huburudisha na kusisimua mwili na akili.

**Vipera vya Ushairi Simulizi**

Ushairi simulizi una vipera vitatu:

- Nyimbo
- Maghani
- Ngonjera

Nyimbo ni tungo za kishairi zenye mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti, muwala na mapigo ya kimuziki na huwasilishwa kwa kuimbwa, nyimbo hutambuliwa kwa sifa tatu;

i) Huwepo kwa hadhira inayotumbuizwa
ii) Muziki unaoimbwa kwa sauti
iii) Matumizi ya ala

**Sifa za nyimbo**

a) Sifa bainifu ya nyimbo ni kwamba hutolewa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti.
b) Nyimbo hutumia lugha ya mkato yenye mpangilio maalumu wa silabi, mishororo na beti zenye mapigo ya kimuziki.
c) Nyimbo hutumia lugha nzito yenye kuibua taswira na hisia nzito kama za mapenzi, huzuni na furaha.
d) Nyimbo zinapoimbwa, maana nyingi huandamana na ala za muziki kama vile ngoma, baragumu, msewe na zumari.
e) Katika jamii za kiafrika, nyimbo hufungamana na muktadha fulani kuna nyimbo za kazi harusi jando na unyago kuzaliwa kwa mtoto, kumpa mtoto jina, ibada na matambiko.
f) Baadhi ya vifungu katika nyimbo hurudiwarundiwa vifungu hivi huitwa vibwagizo, viitikio au mikarara ya nyimbo.
g) Nyimbo nyingi huandamana na ucheshaji wa viungo kama vile mabega kupiga makofi na mapigo ya miguu.
h) Kimsingi, nyimbo ziliimbwa na makundi ya watu kwa hadhira hai. Hata hivyo, kuna nyimbo zinazoimbwa na mtu mmoja kwa hadhira yake au hata bila hadhira.

**Umuhimu wa nyimbo**

a) Nyimbo hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyozibuni mathalan nyimbo katika jamii ya wakulima  zitasheheni msamiati unaohusu shughuli za kilimo kama vile kuvuna, kupanda na kupalilia.
b) Nyimbo humwezesha binadamu kutakasa hisia zake kupitia kwa nyimbo, binadamu hutoa hisia za moyoni kama vile kujutia kosa alilofanya, mapenzi ama huzuni. Mbolezi humsaidia aliyehathiriwa kutoa hisia za huzuni. Nyimbo za mapenzi kama vile chombezi, humwezesha mpenzi kumfichulia mwenzake hisia za moyoni.
c) Ni mbinu mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii rekodi za matukio muhimu katika jamii huweza kuhifadhiwa kwa nyimbo na kupitishwa kwa vizazi.
d) Nyimbo hutumbuiza hutumiwa kama burudani, kufurahisha, kustarehesha na kusisimua.

e) Hupitisha amali na mambo ambayo jamii inayothamini, amali hizo hurekodiwa katika nyimbo mbalimbali kama vile za kazi na kurithishwa vizazi vya jamii hiyo. Mawaidha na thamani za jamii hukaririwa katika nyimbo kama nyenzo za kuzirithisha.
f) Nyimbo hutumiwa kuhamasisha watu na kuchochea hisia za kuchangamkia jambo fulani. Nyimbo za kisiasa, kwa mfano huweza kuchochea hisia za kuungana pamoja kutetea haki au kuunga mkono jambo fulani.
g) Nyimbo huakisi ukwasi wa tamaduni za jamii umbuji (ufasaha wa kujieleza) na ujamii (mvuto na uzuri wa kazi ya sanaa) wa jamii hujitokeza katika nyimbo huteuzi wa maneno,ishara na ujumbe katika nyimbo huonyesha ukwasi wa jamii hiyo kifani.
h) Hukuza ubunifu miongoni mwa wanajamii, uimbaji ni kipawa na nyimbo hupalilia kipawa hiki.

**Aina mbalimbali za nyimbo**

**Bembelezi /bembea/bembe/pembezeji**

Hizi ni nyimbo zinazowafanya watoto walale au watulie wanapolia, zinapoimbwa.

**Sifa**

1. Bembea huimbwa kwa utaatibu kwa sauti na mahadhi ya chini.
2. Huimbwa na wazazi au walezi wa watoto kuwaliwaza na kuwabembeleza watoto walale.
3. Huwa fupi.
4. Bembea hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kutokana na thamani za jamii hiyo.
5. Huimbwa kwa kurudiarudia maneno au kibwagizo wakati mwingine hata nyimbo mzima huimbwa kwa kurudiwarudiwa.
6. Hutumia lugha shawishi na wakati mwingine hutolewa ahadi za kumnunulia mtoto zawadi.
7. Aghalabu zinapoimbwa, mtoto huwa amebebwa kwa mbeleko na mwimbaji kutoa mapigo ya kumpapasa.

**Umuhimu**

1. Hutumbuiza na kuongoa watoto, bembea hupumbaza na kumfanya mtoto anyamaze au alale anapolia
2. Hutumiwa kama sifa kumsifu mtoto mtulivu, husifu pia somo ya mtoto huyo au wazazi wake.

3. Husawiri mfumo wa kiuchumi wa jamii husika, ikiwa baba ni msasi, mtoto atarajiwa kuwa baba ni msasi jasiri au baba yake yuko karibu kutoka usasini.
4. Huonyesha au kusawiri uhusiano katika jamii kupitia bembea, mlezi huweza kuibua migogoro iliyomo kati yake na wazazi wake au wazazi wa mtoto, hivyo kuonyesha uhusiano kati ya waajiri na wajiriwa.
5. Hutakasa hisia ambazo mwimbaji huweza kuwa nazo
6. Humwelimisha mtoto, hata katika umri huu mchanga, kuhusu mambo na shughuli mbalimbali katika jamii na umuhimu wake au thamani yake katika jamii.
7. Husawiri falsafa au mtazamo wa jamii kuhusu jinsia na matarajio ya jamii kwa jinsia Fulani katika bembea, mlezi anaweza kutaja kuwa machozi ni ya kike iwapo anamtuliza mtoto mwanaume, majukumu ya mtoto wa kiume kwa jamii pia huweza kutajwa mlezi huweza kumtajia mtoto wa kike kuwa anatarajiwa kuwa mlezi mwema.
8. Huwaonya watoto dhidi ya tabia hasi. watoto huonywa dhidi ya kulia onyo kwani kulia hukumbusha mtu mambo mabaya.

   **Mfano**

   *Ewe malaika wangu*

   *Uloshuka toka mbinguni*

   *Mbingu kapasua kwa hei*

   *Siku nipokukopoa*

   *Ulinitia furaha iliyopasua kifua*

   *Tabasamu kipajini pako*

   *Ilinitia tumaini, ikanisahaulisha zingizi*

   *Ikayeyusha madhila, ya utasa wa miaka kumi*

   *Ikapeperusha mbali cheka la ukwenza.*

   *Sasa napolia, wanitonesha jeraha*

   *Waniregesha misri, kwa vitimbi vya firauni*

   *Kwa vitisho vya muhebi*

   *Talaka huahidiwa, hadi mbingu.*

*Lipofungua milango ya heri,*

*Silie mwana silie, walimwengu watakusuta.*

*Tangu hapo tanabahi*

*Vidume humu mwenu*

*Kulia hari kuumbiwa*

*Machozi na kekevu ni za kike fahamu*

*Jogoo halii, daima huwika*

*Nikikuona kigugumika hivi wanitia hangaiko*

*Tumaini kuzima*

*Udhaifu kiandama, moyo kitia hamaniko*

*Atanipigania nani*

*Watesi king'anga'ania chake kujitwalia?*

ZOEZI

**1(i) Je, mtoto huyu ni wa kike au kiume?**

**ii) Thibitisha**

2. **Mwimbaji ni nani au ana uhusiano gani na anayeimbiwa**?
**ii) Thibitisha.**

3. **Andika sifa tatu za jamii ya mwimbaji**
5. **Andika mbinu za lugha zilizotumiwa**
6. **Andika majukumu sita ya wimbo wa aina hii.**
*Hutumbuiza watoto na kuwaongoa*

*Hutumika kumsifu mtoto mtulivu*

*Husawiri mfumo wa kiuchumi wa jamii husika*

*Husawiri uhusiano katika jamii kupitia migogoro*

*Hutakasa hisia ambazo mwimbaji huweza kuwa nazo*

*Huwaonya watoto dhidi ya tabia hasi.*

**Mbolezi /nyimbo za matanga/tahalili**

Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa wakati mtu amefariki au wakati wa maafa ama katika halfa za kuadhibisha makumbusho.

**Sifa**

1. Mbolezi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kutegemea imani ya jamii kuhusu kifo na pia kulingana na aliyekufa.
2. Huimbwa kwa njia ya kuwafariji waliofiwa
3. Husifu aliyekufa kwa kawaida mbolezi hutoa sifa chanya au nzuri za aliyekufa watu mashuhuri katika jamii huweza kutungiwa mbolezi zao mahususi zinazowasifu na kutuja michango yao kwa jamii.
4. Hufungamana na muktadha maalum, mbolezi huimbwa tu katika matanga au wakati wa kuomboleza jambo fulani.
5. Huimbwa kwa toni ya huzuni na pengine uchungu ili kuibua hisia za ndani za mwombolezaji.
6. Huimbwa kwa mwendo wa utaratibu.
7. Huonyesha imani ya jamii husika kuhusu kifo.

**Majukumu**

1 Husawiri msimamo wa jamii kuhusu kifo wapo wanaoamini kuwa kifo husababishwa na maovu au pepo fulani na watakao kashifu kifo, watu wengine hutambua kifo kama mlango wa kuingia katika uzima wa milele (kidini)

2. Kuwaliwaza waliofiwa, na kuwasaidia kukabiliana na uchungu au uzito wa kumpoteza mpendwa wao.

3. Hutoa wasifu wa aliyekufa

4. Ni njia ya kutakasa moyo na hisia za aliyefiwa, aliyefiwa huweza kutumia mbolezi kutoa hisia zake za huzuni kwa njia hii, anaweza kupunguza uzito wa kumpoteza mwenzake.

**Mfano**

*"Kama kesho itapambauka*

*Jua la kinjano kuchomoza*

*Kuangazia siku mpya*

*Siku isio tumaini*

*Siku bila mimi mama mtu.*

*Kumbuka ewe kipenzi*

*Usiache chozi kufurika*

*Kuyeyusha makini yako inuka, mwanangu inuka*

*Silie daima, yote yatatengenea''*

*Mpenzi mama ulolala usingizi usio na mzindushi*

*Nalikumbuka vyema hili ni beti uloniandikia*

*Kitandani ukiwa, ukiuguza donda.*

*Donda walokusababisha walimwengu mahasidi*

*Ela nataka ujue, kamwe yote si shwari kama uliponambia*

*Hayawezi kuwa shwari kwa mlezi kikembe*

*Hayawezi tengea kwa yatima alozungukwa*

*Na waja wenye tama kila kitu kurithi,*

*Hayawezi kuwa shwari kumtazama mwezio,*

*Ulotwambia tumwite baba na kumstahi,*

*Ati ni amri ya muumba*

*Akitoka na muhebi, pumbao apata yeye*

*Wafurahia ulochuma wewe.*

*Najitahidi mpenzi mama*

*Ukakamavu kujipa*

*Machozi kuyafuta*

*Ela hino kumbuka*

*Kuondoka kwako huko*

*Hatukukutarajia japo hukuisha kunikumbusha*

*Ziraili liingia ja mwewe*

*Na kukwiba mithili ya kifaranga*

*Mama yake akitazama.*

**MASWALI**

**1a) Andika sifa za mbolezi zinazojitokeza**

*Huimbwa kwa toni ya huzuni na uchungu kwani anayeimba ana huzuni kwani amempoteza mama.*

*Inadhihirisha imani ya jamii inatajwa kuwa ziraili alimwiba mama*

B) Andika mbinu zilizotumiwa

*Tashbihi-ziraili liingia ja mwewe*

*Inksari-walokusababishia*.

**Nyiso**

Nyiso n nyimbo zinazoimbwa jandoni(wavulana ) na unyagoni (kwa wasichana ) kila jamii hata hivyo ina desturi zake zinazozingatiwa kama kigezo cha kuvusha vijana kutoka utotoni na kuingia utu uzima.

**SIFA**

1. Zilitoa sifa kwa waliotiwa jandoni (waliopashwa tohara) wazazi na wasimamizi wao.
2. Ziliimbwa kuwapa wavulana ujasiri wa kukabili kisu cha ngariba
3. Zinatoa mafunzo kwa wavulana kuhusu majukumu yao mapya baada ya kutiwa jandoni.
4. Katika baadhi ya jamii, nyiso huimbwa usiku wa kuamkia siku ya kupasha tohara
5. Maudhui katika nyiso hutofautiana kutoka jamii hadi nyingine.
6. Maudhui yanaweza kuwa ya kuonya dhidi ya kutoa siri, kuwaandaa kwa uchungu watakaohisi au kukejeli woga.

**Majukumu**

1. Hutumika kuwaondoa kihisia wanaotarajia wanaotahiriwa kuwapa ari ya kuwapa kisu cha ngariba

2. Huwajuza wanaotahiriwa kuhusu majukumu mapya na matarajio ya jamii yao kwao, huwafahamisha kuwa wamevuka na ni muhimu kuwaandaa kiakili kwa majukumu ya utu uzima
3. Huonyesha furaha ya vijana wanaotoka katika utoto na kuingia utu uzima.
4. Huhimiza ujasiri na kukebehi woga.
5. Huhimiza uzalendo na kuonea fahari utamaduni wa jamii, wanaohiriki jandoni hujitambulisha na jamii zao zaidi na hivyo uzalendo huimarika.
6. Nyiso hutoa nasaha kwa vijana, huwafahamisha kuhusu matarajio ya uchungu, matarajio ya utu uzima husa dhidi ya woga na umuhimu wa kuhifadhi siri watakazopewa.
7. Huburudisha waliohudhuria shughuli hii.
8. Huleta umoja miongoni mwa wanajamii, vijana waliotahiriwa wakati mmoja hujitambulisha kama ndugu.

**Mfano**

*Ewe kiii*

*Ulozowea kujificha*

*Nyuma ya mama kujikinga, dhidi ya milio*

*Ya radii ilo juu mbinguni*

*Jua kesho ni siku ya siku*

*Siku ya kujua mbichi na mbivu*

*Kutofautisha jogoo na vipora*

*Ngaribu taposhika, chake kijembe*

*Ndipo utakapojua bayani*

*Ukoo wetu si wa kunguru*

*Ikiwa u tayari*

*Kisu kukidhihaki*

*Si thubutu kamwe, wanjani kuingia*

*Ije kuniabisha miye, amiyo na akraba nzima.*

**Nyimbo za kisiasa**

Hizi ni nyimbo ambazo huimbwa katika shuguli au miktadha ya kisiasa.nyimbo za kisiasa huwa na maudhui mapana kama vile mapambano, propaganda, kuzindua, kuhamasisha, kukejeli, kuburudisha, kuhimiza au kutia ari.

**Sifa**

1. Huwa na maudhui mapana kama vile mapambano, propaganda n.k
2. Huimbwa katika shughuli au miktadha ya kisiasa.
3. Huonyesha hali ya mwenye nguvu kumwonea mnyonge.
4. Huburudisha hutumbuiza na kustarehesha watu katika shughuli za kisiasa au za kitaifa.
5. Hutumiwa kuwatuliza na kuliwaza wahasiriwa wa migogoro ya kisiasa.

**Jukumu**

1. Hukuza umoja wa kisisa miongoni mwa washiriki .wakati wa kupigania uhuru, nyimbo hizi zilitumiwa kama nyenzo za kuwaunganisha watu.
2. Huzindua na kuhamasisha watu, huwapa watu k.m wafanyi kazi, ari ya kupigania haki zao. Nyimbo za kisiasa huwatanabahisha watu kuhusu haki zao na kuwahimiza kupigana dhidi ya unyanyasaji.
3. Husawiri mfumo wa kisiasa na kijamii wa jamii husika na maoni ya wananchi kuhusu mfumo huo. Je, wanaupenda au wanaupinga?
4. Husawiri migogoro iliyopo katika jamii, je ni ya unyanyasaji, uongozi mbaya, unyonyaji, ubinafsi, usawa na uhuru?
5. Hutumiwa kueneza propaganda za kisiasa, baadhi ya nyimbo za kisiasa huimbwa ili kusawiri uzuri wa utawala fulani.k.m KANU yajenga nchi, ni wimbo wa kisiasa ulionuia kuwavutia watu kukipenda chama hiki cha kisiasa.
6. Huimiza uzalendo na mshikamano wa kitaifa, nyimbo za taifa ni mfano wa nyimbo za kisiasa zinazohimiza raia kuionea fahari nchi yake na kuishi kwa undugu.
7. Huweza kutumiwa kama rekodi ya matukio ya kihistoria katika jamii Fulani, baadhi ya nyimbo za kisiasa huzungumzia mapambano dhidi ya ukoloni na historia ya mapambano hayo.
8. Hutumiwa kukashifu uongozi mbaya.
9. Hutumiwa kama sifo kuwasifia viongozi waadilifu na mashujaa wengine wa kisiasa kama vile Harry thuku,Dedan kimathi, Arap moi, Jaramogi Odinga, Kenyatta wa nchini Kenya
10. Huburudisha, hutumbuiza na kustarehesha watu katika shughuli za kisiasa au za kitaifa.

11. Hutumiwa kuwaliwaza na kupoza waasiriwa wa migogoro ya kisiasa.

**Mfano**

*Mabeberu watu wabaya*

*Walimfunga kombozi*

*Nia yao ikiwa moja*

*Kudidimiza jamii yetu*

*Katika lindi la istiimari*

*Ela hawakufua dafu*

*Mabarobaro waliingia msituni*

*Bunduki wakashika*

*Kupigana, kupigania 'wiyathi'*

*Beberu lipoona*

*Vita vimechacha*

*Tama iliwatoka*

*Wakasalimu amri*

*Uhuru wakatoa*

*Hawakutoa kwa hiari*

*Hilo usisahau*

*Wazalendo walipigana*

*Kwa jino au ukucha*

*Uhuru tukapata*

*Kombozi akashika sukani*

**Nyimbo za sifa/sifo**

Nyimbo za sifa pia huitwa sifo.ni nyimbo ambazo hutoa sifa za mtu fulani, sifo husifu michango na mafanikio ya watu katika jamii ni muhimu kutaja kuwa nyiso, mbolezi na nyimbo za arusi hutumiwa kama sifo.

**Sifa**

1. Sifo husifu na kutukuza watu ambao wamefanya jambo fulani k.m husifu maarusi, waliohitimu jandoni, viongozi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii, mbolezi na walioshinda mashindano ya michezo au wa kumiliki kitu, kipawa au hali fulani.
2. Sifo hutumia sitiari kwa usanifu mkubwa, huwalinganisha wanaosifiwa na wanyama ili kuonyesha sifa fulani k.m kiongozi anaweza kufananishwa na simba ili kuonyesha ujasiri
3. Sifo hutumiwa katika miktadha mbalimbali ya kijamii kama vile miviga.
4. Huimbwa kwenye jando kuwasiu mashujaa na kuwapongeza kwa kuingia katika utu uzima
5. Huimbwa kwenye mazishi kama taabili/taabini kuwasifu na kuwakumbusha waliokufa.
6. Huimbwa kwenye arusi kuwasifu maarusi.
7. Huimbwa katika sherehe za kutawazwa kwa viongozi au wafalme.
8. Kuna sifo za kidini zinazomsifu Mungu au mitume kwa mfano kasida ya mzia zinamsifu mtume mohammed.
9. Sifo pia huweza kuimbwa na mtu au watu binasfi wakijisifu –majigambo au vivugo.
10. Sifo huasi au kuonyesha thamani ya jamii zinazothamini ujasiri wa kivita, nyingine nasaba tukufu, ufugaji wa mifugo wengi, kilimo au arusi.
11. Sifo hupiga chuku sifa za anayesifiwa.

**Majukumu**

1. Sifo husifu matendo ya viongozi au watu mashujaa katika jamii
2. Hutangaza mafanikio au mchango wa mtu au watu wanaosifiwa kwa jamii, anayeimba sifo hutaja mambo ambayo anayesifiwa alitenda au ametenda.
3. Hukuza uzalendo, sifo huwahimiza vijana kuiga matendo mazuri ya wanaosifiwa, kwa njia hii, watu hujifunza kuionea fahari jamii na kuwa tayari kuitolea mchango wao.

4. Kuweka kumbukumbu au rekodi ya matukio ya kihistoria, wimbo unaomsifu shujaa wa vita, k.m huonyesha vita alivyopigana, alipigana na nani na lini na mbona
5. Huonyesha msimamo na mitazamo ya jamii fulani kuhusu maswala mbalimbali, wimbo unaosifu uzalendo wa mtu fulani, vilevile unaweza kuonyesha chuki kwa usaliti.
6. Hutambua mchango wa watu mbalimbali kwa jamii, sifo hutaja majina ya wanaosifiwa kwa nia ya kutambua na kutambulisha juhudi zao
7. Huburudisha, sifo nyingi hutumbuiza, hutuliza na hupumbaza akili.

**Nyimbo za kazi/hodiya**

Nyimbo za kazi pia huitwa hodiya, ni nyimbo zinazoimbwa na watu wanapofanya kazi huwa kama kihamasishaji kwa wanaoifanya kazi fulani au zinaonyesha mazingira yao ya kazi, hofu zao shida zao, matumaini na ndoto zao.

**Sifa**

1. Maneno ya nyimbo hizi huwa ni ya kuhimiza.
2. Urefu wake hutegemea kazi na vifungu fulani vinaweza kurudiwarudiwa.
3. Mdudo hutegemea kazi inayofanywa, iwapo kazi itafanywa kwa utaratibu mdundo utafuata hali hiyo.
4. Huimbwa wakati watu wanapofanya kazi kila aina ya kazi ina hodiya yake, kwa mfano; wawe /vave ni nyimbo za wakulima. Kimai ni nyimbo zinazohusishwa na ubaharia.
5. Huimbwa na kundi la wafanyakazi au mtu mmoja wakati anapofanya kazi yake binafsi
6. Nyimbo hazihusishi ngoma kwa kuwa watu wote walishiriki kazi.

**Majukumu**

1. Huhimiza watu kutia bidii na kuendeleza kazi bila kufa moyo.
2. Hukashifu uvivu na utegemezi, baadhi ya nyimbo za kazi hukashifu wasiopenda kazi
3. Hurahisisha kazi kwa kupunguza fikra za uchovu, watu wanapofanya kazi wakiimba kazi huonekana kuwa nyepesi na muda kupita kwa kasi.
4. Husawiri imani, mitazamo na thamani za jamii husika kuhusu kazi jamii inathamini kazi gani? Uzembe na bidii kazini huchukuliwaje? Kazi inapewa nafasi gani?
5. Huonyesha changamoto ambayo wafanyakazi hukabiliana nayo katika kazi zao, je, wanahofia nini kazini? Wana matumaini gani katika kazi zao?

6. Hujenga ushirikiano, watu wanapoimba wanapofanya kazi pamoja hujenga ushirikiano; pia huhimizwa katika baadhi ya nyimbo za kazi.

**Mfano**

*Viongozi walisema*

*Turudi mashambani*

*Makonde kushughulikia*

*Mimea kupalilia*

*Tutie ghera ndugu*

*Tujifunge masembo*

*Udongo tutifue*

*Samadi tutie*

*Magugu tung'oe*

*Kilimo tuimarishe*

*Pasiwe wa kutuvuta*

*Misri kuturudisha*

*Kwa pato la kufutia chozi*

*Ukame tatwandama*

*Mashamba tukiachilia*

*Mmomonyoko kuyatoa*

*Tutabaki mikunguni*

*Kutegemea wahisani*.

**Nyimbo za mapenzi**

Nyimbo hizi zinaimbwa kueleza hisia za mapenzi, zinasimamia maoni ya jamii kuhusu mapenzi mtu anaweza kumsifu mpenzi au kusikitika kwa kuachwa na mpenzi, nyimbo hizi huwa na maudhui ya mapenzi.

**Sifa**

1. Huelezwa kwa maneno matamu yenye hisia nzito.

2. Zinaweza kuwa sifa, yaani zikaimbwa kumsifu mpenzif fulani.
3. Huthibitisha mapenzi.
4. Huwa na maudhui mbalimbali kulingana na lengo la mwimbaji k.m

i) Kuonyesha kusalitiwa au wivu.
ii) Kuomba uchumba.
iii) Kumsifu mpenzi-husifu umbo au hulka yake.
iv) Kutambua uhusiano mzuri na mwenziwe na kumbembeleza mpenzi.

**Majukumu**

1. Kusifu tabia au umbo la mpenzi, yaani hutaja tabia chanya na umbo zuri la mpenzi.
2. Kutakasa hisia za anayeimba, mwenye mapenzi huweza kutumia nyimbo kutoa hisia zake za huzuni, furaha au kupumbazika kwa kufanya hivi anaweza kupunguza uzito wa hisia alizonazo.
3. Huburudisha, nyimbo za mapenzi huburudisha anayezisikiza.
4. Hukuza ubunifu, nyimbo za mapenzi hubuniwa kwa ubingwa wa hali ya juu ili kuibua hisia za mapenzi, huzuni au huruma.
5. Ni nyenzo ya kupitisha maarifa au elimu, nyimbo za arusi hutumiwa kutoa mawaidha ya unyumba kwa maarusi wapya aidha matarajio ya jamii na majukumu yao mapya kama bibi na bwana hupitishwa kwa nyimbo.

**Mfano**

*Tina analia tina analia*

*Chozi lausaliti undani wake*

*Undani ambao ameuficha kwa miaka na mikaka*

*Undani ambao japo anachelea kutangaza asije*

*Akaonekana apendaye chongo*

*Itabidi kuuto kuumwaga mtama*

*Na kiini chozi hili ni kwamba imewadia*

*Imewadia siku kanisani kwenda,*

*Kujitia pingu pingu za aushi*

**MASWALI**

Jibu maswali yafuatayo ukirejelea wimbo huu

1. **Ainisha utungo huu kimaudhui**.
   *Ukatili-bibi arusi anapoenda kufanya arusi, bwana arusi haonekani*

   *Mapenzi*-mwanamke huyu anaonekana kuwa alimpenda sana mchumba wake.

   Usaliti-mchumba wa mwanamke huyu, tina anamsaliti kwa kukosa kuja arusini

2. **kwa mujibu wa wimbo huu, jadili kwa mifano nafasi ya mwanaume katika jamii**
   *Msaliti-mchumba wa tina anamsaliti kwa kukosa kkufika pale katika arusi ili amwone* ***tina***

   *Katili-pia anamwacha tina pale bila yakumwambia kuwa hangependa kumwoa*.

9. **Toa mifano ya tamathali za usemi zilizotumika**
   *Uradidi-tina analia, tina analia*

   *Methali-apendaye chongo…(huita kengeza )*

   *Nahau- kumwaga mtama*.

5. **Fafanua umuhimu wa aina ya tungo hii katika jamii yako**.
   *Huthibitisha mapenzi baina ya watu Fulani*

   *Hutakaja hisia za anayeimba, baadaye anapunguza uzito wa hisia hizo*

   *Huburudisha wale wanaosikiliza*

   *Hukuza ubunifu kwa wanaobuni nyimbo hizo na kuziimba*.

**Nyimbo za watoto/chekechea**

Nyimbo za watoto pia huitwa nyimbo za chekechea

Sifa

1. Huimbwa na watoto wakati wa kucheza ili kuifanya michezo ipendeze,au wanapofanya shughuli zao za kitoto.
2. Huwa na matumizi ya takriri kwa kiasi kikubwa
3. Ni maarufu katika shule za malezi kama vile chekechea
4. Watoto hufunzwa  na kuimba nyimbo hizi
5. Maudhui yake hutegemea aina ya mchezo na jamii husika
6. Lugha yake ni sahili au nyepesi

7. Aghalabu huwa fupi
8. Huandamana na miondoko kwa kiasi kikubwa

**Umuhimu**

1. Hutumiwa kama burudani, ni nyenzo muhimu ya kujipumbaza na kupitisha wakati
2. Hukuza ubinifu miongoni mwa watoto hujifunza nyimbo zinazooana na michezo yao
3. Hukashifu tabia hasi, watoto hutumia nyimbo hizi kuwakashifu walio na tabia hasi k.v uchoyo.
4. Hukuza utangamano, watoto wanapokuja pamoja kucheza na kuimba, hawajali tofauti zao za kinasaba na huwa kama watu wa jamii moja.
5. Hutambulisha jamii, kila jamii ina nyimbo za watoto ambazo hufungamana na utamaduni pamoja na thamani za jamii hiyo.
6. Hukuza kumbukumbu za watoto, kwa sababu ya kukariri vifungu mara nyingi.

**MFANO**

*Kitoto kivivu aia aia*

*Kikienda skuli aia aia*

*Saa tatu hazijafika aia aia*

*Ndicho hicho chalia njaa aia aia*

*Ticha' naona njaa aia aia*

*Malimu hadiriki kuandika lolote aia aia*

*Kitoto machozi yatoka aia aia*

*Hadi ruhusa kipewe aia aia*

*Kitazame kilo ndani ya chupa aia aia*

*Ndipo kitulie aia aia*

**MASWALI**

1. Andika maadili yanayojitokeza katika wimbo
   *Bidii –inakashifu uvivu*

   *Tabia njemma- inakashifu tabia ya kulia onyo na kusumbua*

   *Masomo-watto wanahimizwa kwenda shuleni*

2. Taja mbinu za lugha zilizotumiwa
   *Uradidi- aia aia*
   *Utohozi -ticha*
3. Andika miktadha mitatu ambayo nyimbo za watoto hupatikana
   *Watoto wanapocheza*

   *Watoto wanapopewa elimu*.

**Jadiya/jadiia**

Ni nyimbo za kitamaduni ambazo huimbwa na kupokezwa kwa mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine, kila jamii ina jadia zipokezwazo kwa vizazi vyake kimaudhui, nyimbo hizi husimulia mambo mengi hasa yaliyotukia katika historia ya jamii kama vile matendo ya shujaa fulani, mateso, njaa na ucheshi.

**Kongozi**

Ni nyimbo za mwaka, huimbwa wakati wa kukaribisha mwaka mpya.

**Nyimbo za dini**

Huimbwa katika shughuli za kidini

**Kimai**

Uhusisha shughuli za kibaharini

**Nyimbo za vita**

Huimbwa na askari wakati wa vita

**Nyimbo za usasi**

Huimbwa na wasasi wanapokwenda au kutoka usasini

Husifu mtu fulani kwa mchango wake katika jamii

**Nyimbo za kuzaliwa kwa mtoto**

Huonyesha au kuathimisha kuzaliwa kwa mtoto.

**Maghani**

Ni ushairi ambao hutolewa kwa kalmia (nusu kuimba nusu kuongea kama afanyavyo padre) badala ya kuimbwa tofauti kati ya maghani na nyimbo ni kuwa

maghani hayaimbwi, hata hivyo kimaudhui maghani ni sawa na nyimbo kama za kazi, maombolezi au siasa; kama ilivyo katika nyimbo.

**Sifa**

a) Ni fungu za kishairi, yaani yana sifa za kishairi za kuwa na mapigo ya kimuziki na maneno mateule yenye muwala (mtiririko) mzuri wa mawazo

b) Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanayotambwa

c) Hutungwa papo hapo na kusemwa au kutongolewa mbele ya hadhira.

d) Hutungwa kwa ufundi mkubwa

e) Hutolewa na mtu mmoja au kundi la watu

**Umuhimu**

a) Kuchochea wanotaka kuwa shujaa

b) Kutoa sifa nzuri za kuigwa au kutumiwa kukosewa

c) Kuelezea usuli wa mtu, asili au nasaba ya mtu kitu jambo au familia.

d) Kudhihirisha uhodari wa kutenda

**Aina za maghani**

Aina mbili kuu

a) Maghani ya kawaida

b) Maghani simulizi

1. Maghani ya kawaida

Tungo za kishairi ambazo hutongolewa kuhusu maswala ya kawaida, njaa, mapenzi, masikitiko, kazi, majonzi, dini hughaniwa tu.

**Rara**

Ni hadithi fupi nyepesi za kishairi ambazo husisimua

**Sifa**

- Huweza kuandamana na ala za muziki.
- Nyingi zilihusu koo tukufu/zilizotajika.
- Hutolea kwa ...ya huzuni /kitanzia.

- Masuala hufumbua na kudokezwa tu.
- Lugha hujaa utendaji wa matukio.
- Hushughulikia maswala ya kawaida na ibuka kwa mtindo usio rasmi.
- Huwa na ucheshi wenye kinaya.

4. **Maghani simulizi**

   Maghani ya kihadithi yanayosimulia sifa za mtu, kitu, mnyama, historia au tukio fulani.

   Hutolewa na kuambatana na muziki pamoja na ala k.m zeze, marimba, njuga. Mtambaji wa maghani huitwa yeli/manju. Kwa kawaida, yeye huwa bingwa wa kupiga ala aina fulani ya muziki.

1. **maghani ya kawaida**

   Ni ya aina tatu.

a) Sifo

   Ni mashairi ya sifa yaghaniwayo kumsifu mtu fulani kutokana na matendo yake ya kishujaa.

   **Sifa**

a) Husifu watu, wanyama, mimea na hata vitu visivyo hai.
b) Hutoa sifa chanya na hasi sifa hasi hukashifu vitendo vibaya.
c) Hutegemeana na kuingiliana na tanzu nyingine za fasihi simulizi, hutumiwa katika k.m mazishi kusifu aliyekufa kwa matendo yake ya kipekee pia huweza kutumiwa katika arusi na tohara kusifu wanaohusika katika shughuli hizo.

   **Aina za sifo**

a) Majigambo /vivugo

   Tungo za kujisifu, kujitapa au kujigamba anayejigamba huwa mwanasanaa (mshairi) anayeelewa kwa undani analozungumzia.

   **Sifa**

i. Hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe.
ii. Hutungwa kwa usanii mkubwa, anayejigamba hutumia sitiari, ishara, takriri na tashbihi.
iii. Anayejigamba hujitumia kivugo kufuatia tukio mahususi katika maisha yake, anaweza kuongea kuhusu siku za jandoni, ndoa au kuoa, kutoka vitani, michezo, kesi au jambo kali.
iv. Kwa kawaida hutungwa na kughanwa na wanawake.

v. Huwa na matumizi ya chuku kwa kiasi kikubwa, anayejigamba hujisifu kupita kiasi kwa kutaja mafanikio au mchango wake. Anaweza kuahidi kuleta mafanikio makubwa kuliko yale tayari ameletea jamii.
vi. Hutolewa kwa nafsi ya kwanza maadam anayejigamba ni mshairi mwenyewe.
vii. Anyejigamba huweza kubeba baadhi ya vifaa vyake vya kazi au vinavyoonyesha jambo analojisifia. Aidha anaweza kuvaa maleba yanayooana na kazi au jambo ambalo anajisifia
viii. Kwa kawaida, hutungwa papo hapo hata hiyo mengine huandikwa ili kughanwa baadaye katika hafla fulani k.v arusi.
ix. Anayejisifu hutaja usuli wake wa kinasaba, katika baadhi ya jamii anayejigamba huhitajika kutaja na kusifu nasaba au ukoo wake, upande wa baba na mama kwa majina yake halisi.
x. Wanaojigamba nao huwa walumbi au washauri wanaofahamu wanalolitunga.
xi. Maudhui makuu ni ushujaa.

**Umuhimu**

a) Hukuza ubunifu –kadri mtu anavyotunga na kughani majigambo ndivyo anavyoimarisha uwezo wa kubuni mitindo mipya ya utunzi na uwasilishaji.
b) Hukuza ufasaha wa lugha watunzi wengine wa majigambo huwa walumbi.
c) Ni nyenzo ya burudani, huangua waliohudhuria sherehe ambapo yanatolewa.
d) Hudumisha utu na utambulisha mwanamume katika familia, kwa sababu ya uchokozi uliokuwa katika jamii, ilikwa muhimu kwa wanaume katika familia kuwa jasiri, wakakamavu na mashujaa ili kutetea jamii zao. Kupitia kwa majigambo wanaume walidhihirisha nafasi zao katika jamii.
e) Nyenzo ya kufanya watu waheshimiwe, hudumisha ari ya kuwafanya wanaume kutaka kuwa mashujaa mtu alipofanya kitendo cha ushujaa, alijigamba na kuheshimiwa na kila mtu alitaka kufanya jambo la kishujaa ili ajigambe na kuheshimiwa

**b) Tondozi**

Ni tungo ambazo hughanwa kumsifu mtu, mnyama au kitu k.m milima, kijiji, nchi au kitu chochote ambacho huweza kusifiwa.

Tondozi za watu husifu watu mashuhuri, wapenzi, marafki, watani, wake, waume, watoto au adui zao.Wanyama na vitu ambavyo hutungiwa tondozi aghalabu ni mifugo, wanyama wa porini na miti mikubwa, vitu na wanyama hawa hupewa sifa kistiara, zikikusudiwa binadamu.

**Mfano**

*Kipungu kipungu*

*Nani kama yeye*

*Hashindiki kwa nia*

*Hashindiki kwa shabaha*

*Hulenga mbinguni*

*Hutulia gera kufikia peo*

*Peo zisofikika kwa wanaokata tamaa*

*Kipungu, kipung'u, hachi tufani za sanaa*

I. **Kwa kutoa mifano katika utungo huu, thibitisha kuwa utungo huo ni aina ya sifo.**
*Utungo huu unasifu kipungu, ambaye ni ndeg. Inatoa sifa chanya kuhusu kipungu; hashindiki hulenga mbinguni na kufikia peo;hakati tamaa*

II. **Kipungu anapewa sifa gani?**
*Asiyekata tamaa*
*Asiyeshindika*
*Mwenye bidii*

**(c) Pembezi/Pembezeji**

Ni aina ya tondozi inayotolewa kusifu watu fulani pekee, kwa kawaida, husifu watu wenye kujipambanua kwa matendo yao ya kishujaa na kujitolea kwao, hutungiwa watu kama:

- Watawala /viongozi.
- Walezi wazuri.
- Mashujaa wa vita.
- Waganga mashahuri.
- Wapenzi waliopigania pendo lao.

**UTANZU WA SEMI**

**Utangulizi**

Semi ni kauli fupi za kisanaa zenye maana na mafunzo yaliyofichika. Semi hutoa mafunzo kwa njia ya kufumba, mafunzo katika semi hutokana na imani ya jamii ambayo imezibuni mifano ya semi ni methali, vitendawili, misemo, nahau,

misimu, lakabu, mafumbo, chemshabongo na vitanza ndimi. Semi pia huitwa tungo fupi au tungo bainifu.

**Sifa za semi**

a) Semi hufumba ujumbe wake kwa mfano maana ya ndani ya nahau "piga kalamu' ni'futa kazi' ilhali maana ya juu ni 'kuchapa au kugonga kalamu methali pia huwa na maana iliyofumbwa aidha vitendawili hufumba jibu.
b) Hutumia picha (taswira) na ishara kupitisha ujumbe wake, mtu anaposema 'kwetu ni jehanamu; ile picha ya jehanamu inajichora akilini mwa msikilizaji, jehanamu hapa inamanisha mahali pabaya penye mateso mengi
c) Maana ya semi hupatikana katika jamii iliyozibuni, methali "mgaaga na upwa hali wali mkavu" kwa mfano itaeleweka na jamii za pwani.Vile vile katika tashbihi weupe au weusi, hulinganishwa na vitu mbalimbali kutegemea jamii na mazingira yake.mathalani, watasema –eupe kama maziwa au theluji-eusi kama mpingo, lami au makaa kutegemea vifaa vinavyopatikana katika jamii husika.
d) Huwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache mfano ni methali 'juhudi si pato'ambayo imefupisha ujumbe mrefu kuwa mtu huweza kufanya bidii sana na akakosa kufanikiwa, Semi huwasilisha ujumbe kwa njia ya mkato tofauti na hadithi ambazo ni masimulizi marefu.
e) Semi ni tanzu tegemezi, hii ina maana kwamba semi hutokea kuambatana au kutegemea tanzu nyingine kwa mfano methali hutolewa katika muktadha wa mazungumzo ya kutoa mawaidha au mwishoni mwa hadithi kama funzo la hadhi lakabu, misimu, misemo na nahau pia hupatikana katika utanzu wa mazungumzo.

**Umuhimu wa semi**

a) Semi huelimisha, vitendawili, methali, mafumbo na nahau zote hutoa mafunzo ya aina Fulani; methali "mwenda pole hajikwai "hutoa maarifa ya kufanya mambo bila pupa.
b) Hukuza uwezo wa kufikiria, vitendawili, methali na mafumbo humhitaji mtu kufikiria ili kupata ujumbe uliofumbwa.
c) Hutambulisha jamii na wanajamii, kila jamii huwa na semi mahususi zinazohusu shughuli zake, misimu kwa mfano hutumiwa na kundi fulani katika jamii.Methali *mkulima ni mmoja walaji ni wengi* inatambulisha jamii inayohusika katika kilimo, kitendawili kimoja kinaweza kuwa na majibu tofauti kutegemea jamii na mazingira yake.

d) Hukuza utangamano, wakati wa kutegeana vitendawili; kwa mfano watu huja pamoja aidha misimu hujenga uhusiano wa karibu miongoni mwa watu wanaoitumia, lakabu nazo hutumiwa na watu walio na uhusiano wa karibu.
e) Huburudisha, baada ya shughuli za kazi watu hujumuika pamoja katika vikao vya kujiburudisha ambapo hutegeana vitendawili na hushiriki katika vitanza ndimi ili kutuliza bongo na kusisimka.
f) Huhifadhi utamaduni, semi hufumbata desturi za jamii zinapopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, utamaduni huo hufunzwa na kuhifadhiwa.
g) Husawiri mitazamo ya jamii kuhusu masuala Fulani, je, jamii inachukia nini? Inahimiza nini? Kupitia kwa methali *bidii ya mja haiondoi kudura* tunafahamishwa kwamba jamii hii inaamini kuwa binadamu yumo chini ya uwezo wa Mungu nahau, lakabu, vitendawili na mafumbo pia hufumbata tajiriba ya jamii.
h) Hututasfidia lugha, nahau, misemo, misimu na lakabu hutumiwa badala ya msamiati mkali /wenye aibu, badala ya kusema 'kuzaa'tunasema 'kujifungua'
i) Hukuza lugha, semi huyapa maneno maana mpya au maana ya ziada. Misimu huweza kukubaliwa na kuwa nahau rasmi za lugha kwa njia hii msamiati wa lugha hupanuliwa.

**Vipera vya semi**

**Methali**

Methali ni semi fupifupi za kimapokeo zenye kueleza fikira, maarifa, hekima na mafunzo yanayotokana na uzoefu wa jamii mahususi. Methali hutumia taswira na mafumbo, chukulia kwa mfano, *fimbo ya mbali haiui nyoka,* utungo huu ni mfupi na unatumia neno 'fimbo kama fumbo la 'suluhisho'

Methali ni tanzu tegemezi kama ilivyotajwa kutumika kwake hutegemea tanzu nyingine. Methali hutokea katika mazungumzo mazito kama vile kutoa mawaidha au kama kielelezo na kifupisho cha hadithi si utanzu unaoweza kujisimamia kama tanzu nyingine kama vile hadhithi, ushairi au mazungumzo.

**Sifa**

✔ Methali ni kauli fupi ambazo hutolewa kwa mtindo wa kishairi kinyume na jinsi kauli za kawaida zinavyowasilishwa.
✔ Methali zina sifa za kishairi, huwa na vipande vyenye mizani inayolingana na kwamba ni mshororo mmoja.

- ✔ Maudhui katika methali huchotwa katika jamii zinamozaliwa, maudhui hutokana na tajriba na mambo yanayoathiri jamii.
- ✔ Huwa na muundo maalumu wenye sehemu mbili, kwa mfano. *Aliye juu, mngoje chini* sehemu ya kwanza hudokeza wazo na ya pili hulikamilisha kwa kukubali au kukataa.
- ✔ Hujengwa kwa tamathali nyingine za usemi na mbinu za lugha kama vile kinaya, taswira na takriri, methali *kukopa arusi kulipa matanga* imejengwa kwa sitiari.
- ✔ Methali hueleweka na jamii iliyozibuni kwani hubuniwa kutokana na mazingira ya jamii husika.
- ✔ Methali zina sifa ya utegemezi na huingiliana na tanzu nyingine za fasihi.
- ✔ Hutumiwa mwishoni mwa ngano kufupisha maadili ya ngano hiyo.
- ✔ Hutumiwa kubuni lakabu, mtu ambaye huwasaliti marafiki anaweza kuitwa 'kikulacho' kutokana na methali 'kikulacho ki nguoni mwako'
- ✔ Hutumiwa katika tanzu za kimaandishi kama vile riwaya na tamthilia ili kuongeza ladha katika usimulizi.
- ✔ Hutumiwa katika mazungumzo ya kawaida na ulumbi kuleta mvuto.
- ✔ Hutumiwa katika nyimbo na  mashairi
- ✔ Hutumika katika hotuba rasmi au hata mahakamani mshtakiwa, mlalamishi na mahakimu wanaweza kutoa maoni yao kutumia methali.
- ✔ Hutumika katika kutoa mawaidha
- ✔ Methali huelezea ukweli ambao unakubalika na jamii ambao imebuniwa
- ✔ Tofauti na vitendawili ,methali hazina muktadha maalumu wa kutolewa .hazitengewi vikao vya kutolewa
- ✔ methali ni mali ya jamii, kama tanzu nyingine za faihi simulizi hakuna anayeweza kudai kumiliki methali
- ✔ methali huambatana na mazingira ya jamii iliyozizaa, hulka, itikadi, tamaduni na tajriba zake busara fulani huwasilishwa kutegemea mazingira ya jamii kwa mfano.

  *Ulingo wa kwake haulindi manda*
  *Kamba ya mbali haifungi kuni*
  *Fimbo ya mbali haiui nyoka*
- ✔ methali zina matumizi mapana.methali moja huweza kuwa na majukumu mbalimbali kama vile kuonya, kuelekeza na kufunza.
- ✔ Methali huwa na maana ya ndani na nje, maana ya nje hutokana na maana halisi ya maneno yaliyoiunda. Vilevile, methali hupewa maana ya ndani yenye fumbo lililofumbwa na maneno yanaoiunda.

**Majukumu**

a) *Huelimisha,* methali hutumiwa kupitisha maarifa ya kijamii kwa wanajami. *Abebwaye hujikaza* huonyesha kuwa unapopata usaidizi nawe pia jikaze kutia bidii, usingoje tu usaidizi.
*b) Huadilisha.* methali hufunza maadili kama uvumilivu kwa mfano '*mstahimilivu hula mbivu'*
c) *Husawiri mitazamo na falsafa za jamii.* Fulani kuhusu masuala mbaliimbali. Je, jamii inapenda nini? Inachukia nini? Methali *ucha mungu si kilemba cheupe* hudhihirisha kuwa jamii huchukia unafiki.
d) *Hutambulisha jamii,* kila jamii ina methali zake maalum zinazoitambulisha.
e) *Huongeza ladha katika mazungumzo na maandili,* mazungumzo na maandishi yenye matumizi mazuri ya methali huvutia.
f) *Hubudisha,* katika jamii nyingine, methali hutengewa vipindi vya kutolewa na makundi yanayoshindana, hii ni njia mojawapo ya kutuliza bongo.
g) *Hurithisha utamaduni wa jamii,* methali ni zao la utamaduni husika na hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine hivyo utamaduni huweza kurithiwa.
h) *Hufariji,* methali huwatuliza na kuwaliwaza watu wanapokabiliana na matukio au hali zinazohuzunisha, kwa mfano hakuna refu lisilo na ncha.
i) *Hukuza uwezo wa kufikiri,* mtu huhitajika afikiri kwa makini na kuoanisha msamiati uliotumika kwa hali ya maisha ili kupata maana.
j) *Hukuza ushirikiano na mshikamano wa jamii.* Katika jamii ambazo methali hutengewa vikao, watu hujumuika pamoja hivyo kukuza ushirikiano na mshikamano.

**Uainishaji wa methali**

1. **Muktadha**
Ile kuelewa methali, ni muhimu kujua mazingira, tamaduni na hali zilizozizaa methali hizo methali ambazo zimezaliwa katika muktadha au mazingira sawa huweza kuwekwa katika kundi moja.
2. **Maudhui**
Maudhui na fani ndiyo hutawala methali, maudhui katika methali ni mengi na mapana kama zilivyo jamii na shughuli zao, methali ambazo huwa na maudhui sawa huwekwa katika kundi moja, baadhi ya maudhui yanayojitokeza katika methali za Kiswahili ni ya

**a) Malezi**

i. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe

ii. Samaki mkunje angali mbichi
iii. Asiyefunzwa na mamake hufunzwa na ulimwengu.

**b) Kazi**

i) Kazi mbi si mchezo mwema.

ii) Mchagua jembe si mkulima.

iii) Kazi ya bakuli husiri.

v) Kazi isiyo faidi kutenda si ada.

**II. Ushirikiano**

i) Kidole kimoja hakivunji chawa.
ii) Jifya moja haliinjiki chungu.
(iii) Umoja ni nguvu utengano udhaifu.

**3. Mtindo au fani**

Mbali na maudhui, methali hutawaliwa na fani pia. Fani katika methali hudhihirika katika muundo, tamathali za semi na taswira inayoibuliwa, methali ambazo huundwa kwa kutumia fani sawa huweza kuwekwa katika kundi moja. Methali zifuatazo zimeundwa kwa kutumia kweli kinzani

a) Simba mwenda pole ndiye mla nyama.
b) Kuinamako ndiko kuinukako.

**4. Jukumu**

Methali huweza kuanishwa kulingana na majukumu yake. Je, methali inasifu, inakashifu, inahimiza, inaonya ama inafariji? Methali zifuatazo hutumiwa kuonya:

a) Mwenye pupa hadiriki kula tamu.
b) Asiyeangalia huishia ningalijua.
c) Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.

**5. Maana**

a) Methali zote zenye maana sawa huweza kuwekwa katika kundi moja, kwa mfano.

I. Damu ni nzito kuliko maji
i. Meno ya mbwa hayaumani
ii. Mtoto wa nyoka ni nyoka
iii. Mwana wa mhunzi asiposana, huvukuta.

b) Methali zenye maana zinazokinzana pia zinaweza kuainishwa pamoja, kwa mfano. Mvumilivu hula mbivu. Ngoja ngoja huumiza matumbo. Mtu pweke ni uvundo. Nahodha wengi chombo huenda mrama.

**Fani katika methali**

1. **Sitiari**

   Sitiari ni mbinu ya kulinganisha kitu na kingine bila kutummia maneno ya kulinganisha, methali zinazoundwa kwa sitiari ni pamoja na:

a. ***Mgeni ni kuku mweupe***, hapo mgeni anafananishwa moja kwa moja na kuku mweupe kuonyesha mgeni hutambulika haraka akiwa kundini.

b. ***Ahadi ni deni,*** ahadi inafananishwa na deni kuonyesha kuwa ni sharti mtu kutimiza ahadi.

2. **Takriri**

   Takriri ni mbinu ya kurudiarudia maneno au sauti kwa nia ya kusisitiza methali zenye takriri ni kama vile;

***i)*** ***Ngoja ngoja huumiza matumbo.***

***ii)*** ***Haba na haba hujaza kibaba.***

3. **Tashbihi.**

   Tashbihi ni tamathali ya usemi na inayo linganisha vitu kwa kutumia maneno ya kulinganisha kwa mfano:

i. Kawaida ni *kama* sheria.

ii. Jambo usilolijua ni *kama* usiku wa kiza.

4. **Tanakali za sauti**

   Hizi ni miigo ya sauti zinazotolewa na kitu au zinazotokea tendo linapotendeka methali zinazotumia tanakali za sauti ni kama vile

i. Chururu si ndo ndo ndo!

5. **Taswira**

   Taswira ni picha zinazojengeka akilini mwa mtu baada ya kusoma, kutazama au kusikia maelezo fulani. Taswira hizi hutokana na tajriba pamoja na mazingira ya mtu ifuatayo ni mifano ya methali zinazotumia taswira.

i. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.

ii. Mpanda farasi wawili hupasuka msamba.

**Kweli kinzani**

Katika kweli kinzani, maana ya maneno hukinzana kijuujuu (husikika kuwa haiwezekani) lakini ikichunguzwa kwa undani kuna ukweli fulani uliofichika, ifuatayo ni mifano ya methali zinazotumia ukinzani.

a. Wagombanao ndio wapatanao.

b. Ukipigao ndio ukufunzao.

6. **Chuku**

Chuku ni mbinu ya kuongezea sifa kitu zaidi ya kilivyo, mifano ya methali zinazotumia mbinu hii ni:

a. Usipoziba ufa utajenga ukuta.
b. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.

7. **Taashira au ishara**

Katika taashira, kitu kimoja huashiria kingine. Mifano ya methali zenye taashira.

i. Kimya kingi kina mshindo mkuu.
ii. Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.

8. **Dhihaka stihizai au kejeli**

Hii ni mbinu ya kufanya mzaha au kudharau tabia au mienendo isiyofaa, kwa mfano.

i. Hawi musa kwa kuchukua fimbo.
ii. Ucha mungu si kilemba cheupe.

9. **Tashihisi au uhuishaji**

Tashihisi ni mbinu ya kukipa kitu sifa za kibinadamu au kitu kisicho hai kupewa sifa za kitu kilicho hai

**mfano**

i) Adhabu ya kaburi aijuaye ni maiti.
ii) Siri ya mtungi aijuaye kata.

10. **Balagha**

Maswali yasiyo hitaji majibu maswali haya humchochea mtu kufikiri.

i. Pilipili usiyoila yakuwashiani?
ii. Mavi usoyala wayaingiani kuku?

Methali hizi zimeundwa kwa mbinu ya swali ambalo linamhitaji mwenye kuambiwa kufikiria.

11. **Tanakuzi**

Hii ni mbinu inayotumia maneno au kauli zinazopingana, katika tanakuzi sehemu moja ya methali huwa na maana inayopingwa na sehemu ya pili.

i) Tamaa mbele mauti nyuma.
ii) Mpanda ngazi hushuka.
iii) Pole pole ya kobe humfikisha mbali.

12. **Kinaya**

Kinaya ni kinyume cha matarajio au cha hali ilivyo kwa mfano.

i) Kigumba kwa nguruwe kwa mwanadamu ki uchungu.
ii) Kikiharibika cha fundi kikiongoka cha bwana swedi.

**Muundo wa methali**

Methali kwa kawaida huwa na muundo na wenye sehemu mbili sehemu ya kwanza hudokeza wazo nayo ya pili hulikamilisha mfano.

i) Baada ya shida, mkasa.
ii) Debe shinda, haliachi kutika.
iii) Dawa ya moto, ni moto.

**Uchambuzi wa methali**

Maswali yafuatayo husaidia kuchambua au kuhakiki methali

a) Methali imerejelea vifaa gani au inahusu nini? K.m Wanyama, binadamu ama vifaa vya nyumbani?
b) Methali imebuniwa kwa kutumia tamathali gani na mbinu gani za kifasihi? k.m uradidi , kinaya, balagha n.k
c) Methali inaibua taswira gani? Methali ‘simba mwenda pole ndiye mla nyama ‘inaibua taswira ya utulivu makini na subira, kwamba ukitaka kufanikiwa ni sharti uwe na subira.
d) Methali inakupa wazo gani kuhusu jamii? Methali *mtu pweke ni uvundo* inaonyesha kuwa jamii husika inachukia utengano.
e) Je, kuna methali nyingine inayokaribiana kimaana au inayopingana na hii?
f) Je, methali imejikita katika mazingira ama muktadha gani? Kwa mfano.
i) Jogoo wa shamba hawiki mjini (mashambani /mjini)
ii) Mgaagaa na upwa hali wali mkavu (pwani)
iii) Ucha mungu si kilemba cheupe (dini)
g) Je, dhamira ya methali yenyewe ni gani? Inanuia kuonya, kushawishi, kufahamisha au kusifu? Kwa mfano ‘mali bila daftari hupotea bila habari’ inaelimisha; *uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti* ina kejeli ilhali ‘hakuna refu lisilokuwa na ncha” inaliwaza.

**Vitendawili**

Kitendawili ni kauli yenye fumbo ambalo hutolewa kwa hadhira hai ili ilifumbue jibu la kitendawili ndilo fumbo lenyewe.

**Sifa**

a) Kwa kawaida, vitendawili ni semi fupifupi zinazotumia lugha ya mkato.kwa mfano ’pa’funika ‘pa’funika (jibu; nyayo wakati wa kutembea )

b) Vitendawili hutolewa kwa hadhira ili vifumbuliwe hivyo, hadhira yake ni hai na tendi.
c) Hutumia lugha ya picha au taswira na vina ukwasi wa tamathali za semi.
d) Vitendawili huhitaji watu au makundi mawili ili kukamilisha uwasilishaji wavyo mtu wa kwanza hutega na mwenzake hutegua.
e) Vitendawili huwa na muundo au fumyula maalumu ya uwasilishaji kwa mfano
   Mtegaji: kitendawili
   Mteguaji: tega!
   Mtegaji: nyumba yangu haina mlango
   Mteguaji: yai
f) Vitendawili huwasilisha kwa mtindo wa majibizano kati ya mtegaji na mteguaji mteguaji akishindwa kutegua, huhitajika kutoa mji ndipo kupewa jibu na mtegaji
g) Kitendawili ni fumbo au swali liilofichika ambalo huhitaji jibu.
h) Fumbo au jibu la kitendawili hufahamika tu na jamii ambamo kitendawili hicho kimezaliwa, kitendawili kinaweza kuwa na majibu mawili kutegemea mazingira ya jamii kwa mfano, vitendawili vifuatavyo huweza kuwa na jibu zaidi ya moja.
i) Wanangu wawili husabihiana majibu tui na maziwa; unga na majivu.
iii) Mwarabu kasimama kwa mguu mmoja majibu uyoga; mwavuli.
j) Vitendaili ni sanaa ambayo kwa kiasi kikubwa hutegemea uwezo wa mtu kutambua na kuhusisha au kulinganisha vitu katika mazingira yake, kwa mfano ili kufumbua fumbo la kitendawili mbili mbili hadi pwani, lazima mtu aweze kuhusiaha vitu viwili ambavyo daima hufanya jambo pamoja (jibu macho ) macho hutazama pamoja, hulala pamoja na hulia pamoja.
k) Vitendawili huingiliana na tanzu na vipera vingine vya fasihi simuliza kwa mfano ngano za mtanziko hutumia vitendawili, hasa katika fomyula ya ufunguzi wa ngano. Aidha vitendawili hutangulia vikao vya kusimulia hadithi au hutegwa baada ya vikao hivyo.
l) Vitendawili hubadilika kutegemea wakati au kipindi cha kihistoria na maendeleo ya jamii, kitendawili kimoja kinaweza kuundwa au kutolewa kwa maneno tofauti kulingana na kipindi cha wakati kinapotumiwa kwa mfano.
   Mwarabu wangu nimemtupa biwini (machicha ya nazi)
   Mzungu katupwa jalalani (machicha ya nazi) maneno tofauti (mwarabu na mzungu) katika vitendawili hivi viwili ambavyo vina jibu moja yanaonyesha viliathiriwa na nyakati tofauti za kihistoria.
m) Vitendawili ni sanaa inayotendwa kwa hivyo hujisimamia yenyewe tofauti na methali ambazo kwa kawaida ni sanaa tegemezi. Hutegewa vikao maalumu na kutolewa.

n) Kimaudhui, vitendawili hushughulikia masuala katika nyanja zote za maisha ya binadamu na mzingira yake. Maudhui haya hutofautiana katika jamii mbalimbali ingawa baadhi yao huingiliwa
o) Vitendawili vinaweza kuwa sahili (rahisi) na vingine changamano

Vitendawili ni semi maarufu sana miongoni mwa watoto, katika jamii nyingine watoto na watu wazima hushiriki.Miongoni mwa wakamba, kwa mfano watu wazima walishindana kutegua vitendawili hata kuliko watoto.

**Umuhimu**

a) Vitendawili huelimisha, vitendawili hujumuisha masuala mengi katika mazingira ya jamii.
b) Hali hii inavifanya kuwa na uwezo mkubwa wa kuelimisha watu kuhusu mazingira yao aidha mtu akikosa jibu haadhibiwi zaidi ya kutoa mji.
c) Huburudisha.vitendawili huwapumbaza na kuwapumzisha wanaoshiriki katika utegaji ua utegauaji wavyo.
d) Hufundisha kaida na maadili ya jamii, vitendawili huwa na utaratibu fulani unaofuatwa na ambao washiriki wanapaswa kuuheshimu na kuuzingatia, hii ni njia moja ya kuadilisha kwa kuwa kila jambo maishani lina kaida zake zinazoheshimiwa.
e) Hukuza ubunifu na stadi ya kufikiri haraka, mteguaji wa kitendawili sharti afikiri na kuoanisha yaliyotajwa na mazingira yake ili kupata jawabu.Vitendawili hukuza ari ya kufikiria na kudadisi mazingira.
f) Vitendawili hudhihaki na kukejeli watu, hali au tabia hasi katika jamii.hukashifu matendo hasi na kusifu yale chanya
g) Husawiri mitazamo na itikadi ya jamii kuhusu hulka fulani, kwa mfano *nyumbani kwetu kuna papai lililoiva sana lakini nashindwa kulichuma* (jibu: kaka au dada) inaonyesha kuwa ndoa kati ya dada na kaka hairuhusiwi.
h) Hukuza uwezo wa kukumbuka vitendawili hutumiwa kama chemshabongo ya kujaribu uwezo wa mtu kukumbuka na kuhusisha mambo
i) Huleta umoja na ushirikiano katika jamii, watu hujumuika wakati wa kutegeana vitendawili kwa njia hiyo utangamano huimarika.
j) Hutambulisha jamii kila jamii huwa na vitendawili vinavyoonyesha mazoea, hali, tajriba na mazingira ya jamii husika.
k) Huchochea tabia ya udadisi, uzoefu wa kutafuta kiini cha kitendawili hujenga tabia ya kutaka kufichua jambo lililofichika kwa kujaribu kupata jibu la jambo

ktika kitendawili wanajamii huimarisha ari yao kutafiti mambo ili kubaini kiini chake.

l) Vitendawili hukuza na kusambaza ujuzi wa lugha, vitendawili vina ukwasi mkubwa wa lugha na tamathali za semi kwa hivyo ni nyenzo kuu ya kukuza na kusambaza maswala ya lugha katika jamii.

**Fani katika vitendawili**

**Muundo**

Kama tulivyotaja awali, vitendawili huwa na fomyula au muundo maalamu wa uwasilishaji.

1. **Kitangulizi ambacho hutolewa na mtegaji.**
   *Mtegaji: kitendawili*

*iii)* Hadhira humpa ruhusaya kutega. *Mteguaji: tega!*
*iv)* Mtegaji hutoa kitendawili mtegaji: *Fatuma mchafu*
iv) Jibu hutolewa na mteguaji*: Mteguaji nguruwe (kosa)*

*v)* Jibu likikosekana mtegaji huomba *mji :Mtegaji :Umenoa*
*Nipe mji.*

*vi) Mteguaji hutoa mji mteguaji :Ninakupa migingo*
*vii)* Mtegaji akipewa mji hutoa jawabu sahihi*: Mtegaji! Nilienda migingo, watu wa migingo wakaniambia nikija niwasalimu.*
Jibu lake ni ufagio

**Mtindo**

Vitendawili hutolewa kwa mtindo wa majibizano, majibizano haya huwa kati ya mtegaji na mteguaji na hadhira ya wasikilizaji utaratibu ulioelezwa katika muundo huzingatiwa na mtegaji na mteguaji /hadhira.

**Lugha**

1. **Sitiari**

Aghalabu, vitendawili hutumia sitiari k.m

i. Fatuma mchafu (ufagio) hapa fatuma ni sitiari ya ufagio.
ii. Saa yetu kadiri inavyotembea ndivyo inavyopunguza nguvu (moyo) saa ni sitiari ya moyo.

iii. Jani la mgomba laniambia habari zinazotoka ulimwenguni kote ( gazeti /jarida) jani la mgomba ni sitiari ya gazeti /jarida.

**2. Tashihisi /uhuishaji**

Wakati mwingine, vitendawili hutumia mbinu inayoipa kitu kisicho hai sia za kibinadamu k.m

i. Akizungumza kila mtu hubabaika (radi) hapa radi imepewa sifa ya kuzungumza kama binadamu sauti kali ya radi huwaogofya binadamu.

ii. Amenifunika kote kwa blanketi lake jeusi (giza) giza limepewa sifa ya binadamu ya kumfunika mwingine.

iii. Daima nasaabisha mafarakano (ukewenza) ukewenza umerejelewa kwa nafsi ya kwanza.

**2. Taashira**

a. Faiza akiniona ajificha (mzee kobe) kinachoashiriwa na kujificha kwa Faiza ni kobe.

b. Chonge la nyoka huuma walio mbali (ugonjwa) chonge la nyoka linaashiria ugonjwa.

**3. Stihizai /dhihaka/kejeli**

Vitendawili vinavyobuniwa kwa dhihika hutumiwa kukashifu mienendo hasi katika jamii pia hueleza sifa ya kitu kwa njia ya dharau k.m

i. Akivaa miwani hafanyi kazi vizuri (mlevi) kitendawili hiki kinakashifu ulevi

ii. Babangu amevaa koti la chuma (mzee kobe)

iii. Upara wa mwarabu unafuka moshi (chai ya maziwa )

iv. Uzi mwembamba umefunga dume kubwa (usingizi)

4. **Kweli kinzani**

Vitendawili vya aina hii huundwa kwa hoja mbili zinazopingana k.m

i) Ajenga ingawa hana mikono (ndege) ndege hana mikono kama binadamu hata hivyo hujenga kiota.

ii) Ana meno lakini hayaumi (kichana) meno ya kichana hutumiwa kuchana wala si kuuma.

iii) Hufa ikifufuka (bahari kupwa) maji ya bahari huwa (kutoka ufukweni)na kurejea.

**5. Takriri**

Kuna vitendawili vinavyoundwa kwa tanakali za sauti .kwa mfano

i) Aliwa yuala,ala aliwa-(papa)

ii) Amezaliwa ali,amekufa ali,na amerudi ali (nywele)

iii) Mama kazaa mtoto kazao mtoto na mtoto kazaa mtoto (kuku na yai)

**6. Tanakali za sauti**

i) Chubwi'-(jiwe likianguka ndani ya maji)
ii) Prr' mpaka 'makka'- (utelezi )
iii) 'Pa'funua 'pa'funika – (nyayo wakati wa kutembea )

**7. Taswira**

Baadhi ya vitendawili vimeundwa kwa jinsi ya kuibua taswira au picha mbalimbali.k.m

i) Nimemwona bi kizee akijitwika machicha –(Mvi)
ii) Ameingia shimoni akiwa uchi, akatoka amevaa nguo-(mbegu)

**8. Utata**

Baadhi y vitendawili huweza kufasiriwa kwa njia zaidi ya moja tunasema kitendawili cha aina hii kina utata. Utata katika vitendawili husababishwa na hali kwamba jibu la kitendawili hutokana na mazingira.watu tofauti huweza kuwa na majibu tofauti kwa kitendawili hicho hicho kutegemea hali ambayo inawazunguka.

Kwa mfano

i) Inachurura inaganda (asali au gundi )
ii) Gari la kila mtu (miguu au jeneza au kifo )

9. Vitendawili vinavyohusiana na methali

a. Ukichukua mama chukua mtoto –(sagio /jiwe dogo la kusagia linalopitishwa juu ya jiwe kubwa ) methali: ukivuta sagio uchukue kabisa na jiwe dogo la kusagia
b. Mzee amekufa na vyombo vimevunjikavunjika (kifo cha kiongozi husababisha matatizo ) methali :mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba

**Mfano**

a) Ndege wengi baharini (nyota ngani )
i) Taswira
ii) Istiari

b) Natembea shambani – (wembe wa kunyolea ukiwa kichwani
i) Taswira
ii) Tashihisi

c) Pambo juu ya jiwe (upara )
Taswira
Sitiari
Dhihaka /stihizai

d) Hulia huku akiunganisa (cherehani)

i) Tashihisi
ii) Taswira
e) Hukopa lakini halipi-(kifo)
i) Ukinzani
ii) Tashihisi
iii) Kinaya
f) Kisiki chetu hakikui (mbilikimo )
i. Stihizai /kejeli
ii. Sitiari
iii. Taswira

**Kufanana na kutofanan kwa methali na vitendawili**

Methali na vitendawili hufanana kwa vile.

i) Ni tungo fupi
ii) Huwa na maana fiche
iii) Hutumia lugha inayojenga taswira
iv) Huupata maana kulingana na jamii
v) Hufumbata ukweli Fulani wa kijamii
vi) Huweza kutumiwa katika shughuli rasmi kama vile katika maamuzi ya kesi na utoaji hotuba.
vii) Huweza kutekeleza majukumu sawa k.m kuonya kuburudisha au kunoa bongo.

Methali na vitendawili hutofautiana kama ifuatayo.

| **vitendawili** | **methali** |
|---|---|
| Kimuundo, huwa na fomula mahususi ya uwasilishaji | Haina fomula |
| Fumbo lake lazima lifumbuliwe pao hapo | Fumbo halifumbuliwi hapo |
| Huwa maarufu zaidi miongoni mwa watoto | Huwa maarufu miongoni mwa wazee |
| Hutolewa katika vikao maalum | Si lazima pawe na vikao maalumu |
| Huwa na hadhira tendi | Si lazima pawe na hadhira tendi |
| Huwasilishwa na mtegaji na mteguaji | Huwsilishwa na mtu moja tu |

**Misimu**

Misimu ni semi za muda ambazo hubuniwa na kutumiwa katika mazingira maalumu katika kipindi maalumu cha wakati, msimu huitwa pia *simo*. Misimu inaweza kupata mashiko katika jamii na kukubaliwa kama msamiati au semi rasmi za lugha.

**Dhima**

1. Kutambulisha makundi mbalimbali ya watu
2. Huhifadhi siri za watumiaji
3. Kuibua hisia mbalimbali
4. Hukuza lugha
5. Huhifadhi historia ya jamii.
6. Hutasfidi lugha
7. Hukuza uwezo wa kufikiri au kudadisi
8. Hukuza ushirikiano na utangamano
9. Huondoa urasmi katika mazungumzo

**Sifa**

a) Misimu ni semi au msamiati ambao huzuka na kutoweka baada ya muda Fulani.
b) Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano ya makundi fulani k.m kuna misimu ya vijana ya wafanyakazi katika vyombo vya usafiri na hata ya watoto.
c) Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano yao katika kipindi fulani cha wakati na mahali fulani
d) Ingawa misimu huzuka na kutoweka baada ya muda, baadhi ya misimu hudumu na kukubalika kama semi au msamiati sanifu wa lugha husika kwa mfano neno *chai* (kwa maana ya hongo ) lilianza kama msimu, kisha likashika na kukubalika kama msemo sanifu.
e) Msimu hupata maana yake kutoka kwa watumiaji pamoja na muktadha wa mahali na wakati, kwa mfano neno *sare* ni msimu uliopata maana katika sekta ya usafiri wa matatu likimaanisha kubebwa bila malipo.

**Uainishaji wa misimu**

Misimu hutofautiana kwa kutegemea

a) *Wahusika* – kuna misimu ya vijana, mabaharia au wanafunzi neno *beste* hutumiwa na vijana kumaanisha rafiki
b) *Matilaba* – kuna misimu ya kuendesha biashara neno ‘*kungara* ‘linamaanisha kuvaa nguo inayopendeza na ‘sare’ lina kubebwa kwenye matatu bila kulipa nauli.

c) *Vifaa*- kuna misimu ya vyakula, pesa na vyombo vingine .maneno '*nyaki'* ni nyama na '*ashu*' ni shilingi kumi.
d) *Mahal*i- kila eneo huibua misimu yake.gari la uchukuzi kwa uma nchini Kenya ni 'matatu na nchini Tanzania ni 'daladala '
e) *Wakati au kipindi* - misimu hubadilika kulingana na wakati au kipindi kwa mfano, wakati wa uchaguzi wa 2002 nchini Kenya kulizuka neon *unbwogable* lililomaanisha wasioshindwa na lika toweka katika muktadha baadaye.

**Lakabu**

Lakabu ni jina la msimbo au jina la kupanga ambalo mtu hujibandika ama hubandikwa kutokana na sifa zake za kimaumbile kitabaka, tabia au kimatendo. Aghalabu lakabu huwa neno moja au fungu la maneno lililo na maana fiche au ya kisitiari sifa zinazodokezwa katika lakabu zinaweza kuwa za kusifu, kudhalilisha au kukosoa.

**Sifa**

a) Lakabu si jina la mtu ni jina tu la kupangwa.
b) Lakabu aghalau huwa neno au fugu la maneno lililo na maana iliyofumbwa.
c) Lakabu huoana na sifa za mhusika inaweza kusifu kukejeli au kufanyia tashtiti tabia hasi ya mhusika lakabu *baba wa taifa* moja kwa moja inaashiria sifa nzuri za mhusika na kumsifu kwa upande mwingine lakabu kama *kangumu* inaashiria tabia ya uchoyo.
d) Lakabu hupatikana katika tanzu na vipera vingine nya fasihi simulizi kama vile sifo, malumbano ya utani na majigambo (vivugo) ambapo wahusika hujipa majina ya kupanga ya kujitapa.
e) Lakabu huundwa kwa lugha ya picha au taswira na sitiari kwa mfano, lakabu 'nyayo' ya Raisi mstaafu inatumia sitiari inamfananisha na nyayo za mtu hivyo kutupa taswira ya kujipata kufuata falsafa ya mtu mwingine.
f) Ingawa lakabu si jina halisi la mtu, huweza kudumu na kufanya jina halisi la mtu kusahaulika kwa mfano Sonko.

**Umuhimu/dhima**

a) Kusifiwa kwa matendo chanya ya mhusika.
b) Hukashifu au kukejeli matendo mabaya ya mhusika.
c) Ni kitambulisho cha mhusika husawiri tabia au hali ya mtu fulani ka maneno machache.

d) Hutumiwa kama ishara ya hesima katika jamii ambamo kumtaja mkazamwana kwa jina lake ni mwiko, baba mkwe huibua lakabu ya kumrejelea mkazamwanawe.
e) Hutumiwa na baadhi ya wahusika kuficha utambulisho wao baadhi ya waandishi hujibandika majina ya uandishi ili kuficha majina yao halisi.
f) Hutumiwa na wahusika kujigamba na kujinaki katika majigambo, anayejigamba hujipa lakabu ili kujinaki na kuonyesh ubingwa wake.
g) Hutumiwa kuhifadhi siri wakati mwingine watu humpa mtu fulani lakabu ili wanapomrejelea isijulikane ni nani.
h) Hukuza uhusiano bora hasa miongoni mwa watani katika kutaniana watu huweza kubandikana majina.
i) Hutumiwa kuondoa urasmi katika mahusiano ya kijamii.

**Vitanza ndimi**

Vitanza ndimi ni kauli au sentensi zenye maneno ambayo yana mfuatano wa sauti zinazotatanisha kimatamshi.Vitanza ndimi huundwa kwa maneno yenye sauti zinazokaribiana sana kimatamshi kimsingi, katika jamii nyingi za kiafrika watu hufurahia kucheza na maneno kama njia ya burudani. Watoto kwa mfano, wana mazoea ya kucheza na maneno na sauti katika michezo na nyimbo zao

**Sifa**

a) Kimsingi, vitanza ndimi ni mchezo wa maneno na sauti.
b) Huundwa kwa maneno ambayo yana sauti zinazokaribiana kimatamshi maneno haya huweza kuwa na maana nyingi au yenye kukabiriana kimaana.
c) Ukinzani wa maneno kisauti na kimaana huyafanya matamshi ya maneno kuutatiza ulimi.

**Mifano ya vitanza ndimi**

i) Wataita wataita wataita taita.
ii) Waite wale wana wa liwali wale wali wa liwali.
iii) Cha mkufuu mwanafuu ha, akila hu, cha mwanafuu hu, akila ha.

**Dhima**

a) Vitanza ndimi hukuza matamshi bora mtu anapotamka kwa haraka na kwa usahihi, hutia makali stadi zake za kimatamshi. Kupitia hali hii uzoefu wa kutamka vyema hujengwa.
b) Hukuza uwezo wa kufikiri kwa haraka, baadhi ya vitanza ndimi hutatanisha kuwaza haraka ili kuteua neno sahihi la kutamka.
c) Kuburudisha, kimsingi vitanza ndimi vilinuiwa kuibua ucheshi na kuchangamsha hadhira.
d) Hukuza ubunifu, anayebuni vitanza ndimi anahitaji kuwa na ujuzi mpana wa lugha na ubunifu ili kuteua maneno yanayokaribiana kimatamshi na kimaana.
e) Hukuza lugha, vitanza ndimi vilivyobuniwa katika vipindi mbalimbali huhifadhiwa na kupitishwa kwa vizazi vijavyo kama malighafi katika kipera cha vitanza ndimi.
f) Huhifadhi utamaduni na kuurithisha, maarifa ya kipera cha vitanza ndimi yasingehifadhiwa na kurithishwa kama vipera vingine vya fasihi simulizi, tusingevisoma leo.
g) Ni kitambulisho cha jamii, vitanza ndimi huakisi mazoea ya jamii husika kila jamii ina vitanza ndimi vyake mahususi.
h) Hujenga uhusiano bora wa kirafiki, ucheshi unaoibuliwa na vitanza ndimi hujenga uhusiano bora miongoni mwa washiriki.

**Mafumbo na chemshabonga**

Mafumbo ni kauli zenye maana iliyojificha, mafumbo hutumia lugha fiche au ya kiistiari pamoja na tamathali nyingine za usemi. Humtaka anayeambiwa kudadisi mazingira yake na kufikiria ili kupata maana, mafumbo huchemsha bongo za wale wanaoshiriki katika kuyafumbua ingawa vitendawili ni aina za fumbo tunadai kwamba mafumbo kwa kawaida ni semi ndefu kuliko vitendawili.

Kuna mafumbo yaitwayo chemshabongo, chemshabongo ni maswali ambayo humtaka mtu kutumia akili na ujuzi kuyajibu. Maswali mengi ya aina hii ni ya kimapokeo, mengine hubuniwa na msemaji ili kukidhi mahitaji ya hadhira mahususi. Baadhi ya chemshabongo kwa hakika ni hesabu tu nyingine hutolewa kwa mraba unahitaji kujazwa

Mfano

Nina kilo moja ya mchanga na kilo moja ya pamba kipi kizito zaidi, mchanga au pamba?

Jibu: vyote vina uzito sawa kwa vile uzito wavyo ni sawa (kilo moja)

**Sifa**

a) Ni semi zinazofumba jambo.
b) Huhitaji mtu kuwaza ili aweze kubuni fumbo lenyewe.
c) Shughuli, maumbile au vitu vilivyo katika mazingira ya jamii kama vile mifugo, njia za usafiri na nyenzo za biashara vinaweza kufumbiwa.
d) Baadhi ya mafumbo hufananisha kitu kilichotajwa katika fumbo na mazingira halisi.
e) Baadhi ya mafumbo huwa marefu na mengine huwa mafupi.
f) Mafumbo huhitaji mantiki ili kuyatmbua. Mfano nina chui mbuzi na majani ya kuliwa na mbuzi je nitafanya aje ili nivuke ngambo ile …

**Dhima /umuhimu**

a) Hukuza uwezo na wepesi wa kufikiri ili kufumbua fumbo ni lazima mtu afikiri kwa makini na wakati mwingine kwa upesi.
b) Hustawisha ubunifu fumbo hufumbuliwa kwa kuoanisha yaliyomo katika fumbo, tajiriba na mazingira hivyo mtu hutumia kiwango fulani cha ubunifu ili kupata maana aidha shughuli ya kufumbua huhitaji watu kuwa wabunifu.
c) Hukuza maarifa ya kukabiliana na changamoto na kutumia mantiki kusuluhisha mambo.

**Nahau**

Nahau ni fungu la maneno ya kawaida lenye maana ambayo haitokani moja kwa moja na maana za maneno yaliyoziunda, nahau **piga kalamu** si kuchapa kalamu bali ni 'kufuta mtu kazi'

Mifano mingine ni.

Piga maji- Lewa.

Kujitia hamnazo – Kujifanya hujui.

Kukata kamba- Kufa.

Kunja jamvi- Maliza shughuli.

Kwenda nguu- Kukata tama.

Piga vijembe- Kusema kwa mafumbo.

Kumwaga unga- Kuachishwa kazi.

Ndege mbaya-  Bahati mbaya.

Kupata jiko- Kuoa.

Shingo upande- Bila kutaka.

**Sifa za nahau**

a) Nahau huundwa kwa lugha ya mkato iliyo na ujumbe mzito wa mafumbo k.m kidudu  mtu-mfitini.
b) Nahau mbili au zaidi zinaweza kuwa na maana moja k.m jamvi la wageni/bao la mkahawani –kahaba.
c) Nahau moja inaweza kuwa na maana zaidi ya moja k.m kushika mguu-kuomba radhi /kutoa shukrani kupiga mbio.
d) Maneno katika nahau hupoteza sifa zake za kawaida na kuchukua maana nyingine iliyo tofauti kabisa .k.m kula chumvi –kuwa mzee.
e) Nahau huundwa kwa maneno mawili au zaidi kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa-danganya.
f) Bega kwa bega pamoja.
g) Nahau huweza kuundwa kwa mitindo mbalimbali au kwa maneno ya kategoria mbambali k.m

i. Kitenzi na nomino –piga chuku, andika meza
ii. Kitenzi na kitezi-kufa kupona,pata shika
iii. Kitenzi na kielezi –jikaza kisabuni, kufa kikondoo
iv. Noino na nomino-askari kanzu, domo kaya
v. Nomino na kitenzi-mguu haumshiki, damu kumkauka.
vi. Nomino na vivumishi –nyoat njema, ndege mbaya

**Dhima ya nahahu**

a) Nahau hukuza lugha, nahau huyapa maneno maana tofauti na maana ya kawaida kwa njia hii hupanua msamiati wa lugha.
b) Nahau huipa lugha, badala ya kutumia maneno yaliyozoeleka, nahau hutumiwa kukoleza ladha ya lugha.
c) Nahau pia hutumiwa kupunguza ukali wa jambo linalorejelewa k.m jicho la nje-uasherati.
d) Nahau huweza kutumika pia kuhifadhi siri ili wanatengwa wasielewe, si watu wote wanaoelewa maana ya nahau zote.

**Misemo**

Misemo ni semi ambazo zinabeba ukweli wa kijumla, hutumika kueleza mambo mbalimbali yanayokubali ukweli huo. Misemo hutumiwa kutoa ujumbe kwa muhtasari mfano zaidi.

i. *Binadamu ni udongo* –kumaanisha binadamu aliumbwa kwa udongo na hufa na kurudi udongoni.
ii. *Mwili haujengwi kwa mbao*-mtu lazima ale ili apate kujenga mwili au kunenepa hauwezi kujengwa kwa mbao.
iii. *Umaskini si kilema*-kumaanisha kuwa mambo hubadilika ukizaliwa katika umaskini si lazima uishi na ufe ukiwa maskini.
iv. *Lila na fila havitangamani* –ubaya na wema hayaendi pamoja.
v. *Ndio kwanza mkoka ualike maua* –kumaanisha ndio mambo yamezidi kushika kasi.
vi. *Mgomba haupandwi changaraweni ukamea* –jambo njema halifanywi mahali pabaya likapendeza.

Baadhi ya misemo hutumiwa kama methali kwa mfano, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

**UKUSANYAJI NA UHIFADHI WA FASIHI SIMULIZI**

**Utangulizi.**

Sifa za fasihi simulizi ni kwamba huzaliwa hukua, huishi na huweza kufa. Kadiri jamii inavyobadilika, fasihi simulizi inabadilika na kuathiiriwa na maendeleo ya binadamu kisayansi, kijamii na kiteknolojia.Vipera vipya vya fasihi simulizi huzaliwa kutokana na athari za utandawazi, hukuzwa na kupewa uhai katika mazingira mapya aidha vipera vya zamani k.m matambiko na ngomezi huweza kufa au kupewa sura mpya. Hivyo kuna umuhimu wa kuhifadhi tanzu za fasihi simulizi ili zisipotee lakini kabla ya kuzihifadhi ni lazima kwanza zikusanywe ukusanyaji wa data ya fasihi simulizi hufanywa ili kuendeleza na kutekeleza malengo muhimu yanayokusudiwa na anayekusanya.

Mkusanyaji apaswa kufuata hatua zifuatazo;

a) Kujiadaa – hapa mtu anatakiwa kuzingatia

- Mada ya utafiti –anatafiti kuhusu nini?
- Mawanda ya utafiti – Kama ni kitendawili anatafiti fani? Aina?
- Walengwa – jamii ipi? Wenye umri gani?
- Kipindi cha utafiti – utaanza na kutarajia kumaliza lini?

- Kuomba kibali cha utafiti kutoka kwa taasisi husika k.v wizara ya elimu
- Mbinu za ukusanyaji na kuhifadhi data, je atatumia: Hojaji au mahojiano je, vifaa hivi vi tayari?
- Gharama ya utafiti –je, atatumia kiasi gani cha pesa? Nani atafadhili utafiti?

b) Utafiti na ukusanyaji wa data –mtafiti anaweza kukusanya data kupitia hojaji, mahojiano, kushiriki au kutazama.
c) Rekodi ya data –kuna njia mbalimbali za kurekodi data basi vifaa hivi sharti viwen tayari kabla ya utafiti.
d) Kuchunguza upana wa data/maelezo yaliyotolewa na walengwa na kuyanakili ili kuyachunganua baadaye.
e) Uchanganuzi na kufasiri wa data –huchanganuliwa kulingana na vigezo vya uchanganuzi alivyoweka na kulingana na mada yake. Matokeo hutumiwa kutoa hitimisho na mapendekezo kuhusu mada ya utafiti.

**Ukusanyaji wa kazi za fasihi simulizi**

Kwa vile sifa za fasihi simulizi hutegemea jamii Fulani, sio vyema kulinganisha fasihi ya jamii moja na sanaa ya jamii nyingine.

Ni vyema mkusanyaji kuchunguza ili aelewe umbo, thamani na dhima ya fasihi hiyo. Njia mbalimbali za kukusanya fasihi simulizi ni:

1. **Kusikiliza**
   Mkusanyaji anaweza kusikiliza wasanii katika jamii fulani wakitamba, kusimulia au kuimba tungo zao
2. **Kushiriki**
   Mkusanyaji aweza kujiunga na jamii kwa kushiriki katika ngoma, soga na masimulizi ya hadithi na tanzu nyingine hapa anayekusanya data ya fasihi simulizi haulizi bali hujirekodia anachokibaini katika ushirika huo.

**Umuhimu wa kushiriki**

a) Mtafiti huja karibu zaidi na jamii na hupata habari za kuaminika moja kwa moja
b) Ni njia bora ya kukusanya habari kwa watu wasiojua kusoma na kuandika ama wanaona vigumu kujieleza moja kwa moja.
c) Ni rahisi kwa mtafiti kuuliza maswali kuhusu kipera kinachowasilishwa mathalani anaweza kuuliza kuhusu kipidi ambamo wimbo fulani uliimbwa au hadhira mahususi ambayo ilitambiwa aina fulani ya ngano.

d) Mtafiti huweza kunakili anayosikia au kuona, hivyo kuhifadhi sifa za kiimbo, toni na ishara.
e) Mtafiti hupata taathira na hisia halisi ya yanayowasilishwa kwani anakabiliana wazi na watendaji halisi huelewa zaidi.
f) Mtafiti huweza kuthibitisha aliyokusanya kwa hojaji au mahojiano kwa kuyahakiki
g) Kusiriki hukuza utangamano kati ya mtafiti na wanajamii.ni rahisi kwa mtafiti kupata majibu ya masuala anayotafiti kwa kushiriki na kutangamana na wanajamii.

**Udhaifu wa kushiriki**

a) Huchukua muda mrefu kulingana na njia nyinginezo kama vile hojaji au mahojiano.
b) Mtafiti huweza kutekwa na yaliomo akasahau kurekodi.
c) Ugeni wa mtafiti huweza kuleta wasiwasi miongoni mwa washiriki wakakosa kufanya kama kawaida.
d) Uchanganuzi wa data ikusanywayo kwa njia hii ni ngumu, lakini rahisi kwa mtafiti kuacha maswala muhimu. Ni njia ghali ya utafiti kwani inamhitaji mtafiti kusafiri mbali ili kushiriki katika utendaji pia vifaa vya kuhifadhia data yenyewe kama vile kanda za video huwa ghali na nguvu za umeme huenda zikakosa.

3. **Kurekodi**

Mkusanyaji anaweza kusikilizana na wasanii na kuwarekodi katika vinasa sauti, kanda za video filamu au kuwapiga picha .

4. **Kutazama**

Mkusanyaji anaweza kushuhudia kwa macho fasihi fulani ikiendelezwa hapo atashuhudia mwenyewe bila kushiriki baadaye anaweza kuandika ili kuhifadhi.Mbinu hii hutumika zaidi katika utafiti wa maigizo.

**Umuhimu wa utazamaji**

a) Ni rahisi kwa mtafiti kurekodi kwani hashiriki utendaji
b) Mafiti hupata habari za kutegemewa zaidi hasa anapotumia kinasasauti kurekodi moja kwa moja.
c) Mtafiti anaweza kukaa mahali asipoonekana na kushuhudia utendaji halisi hivyo utendaji hautaathiriwa k.m kuwa na wasiwasi kwa ugeni wa mtafiti.

**Udhaifu wa utazamaji**

Wanajamii wanaweza kumshuku mtafiti kuwa anawapeleleza hivyo kusitisha uwasilishaji wao.

5. **Kutumia hojaji**
Ni fomu yenye maswali yaliyochapishwa ili kukusanya habari fulani huandaliwa na mkusanyaji wa data na kutumwa au kupelekwa kwa mhojiwa au atakayejaza hojaji ni za aina mbili.

a) **Hojaji funge**
Humfunga mhojiwa kwa majibu fulani tu kila swali huwa na orodha ya majibu na mhojiwa huhitajika kuweka alama tu kwa lile analoona kuwa jibu sahihi

b) **Hojaji wazi/huru**
Aina hii ya hojaji huwa na maswali ambayo yanahitaji majibu ya maelezo mhojiwa hutoa maoni yake.

**Sifa za hojaji**

a) Hojaji huwa na maswali yanayojibiwa na kikundi lengwa mtafiti anaweza kulenga watambaji ngano au walumbi
b) Huweza kutumiwa moja kwa moja na mkusanyaji kwa anyehojiwa hivyo mtafiti humwelekeza mhojiwa namna ya kujibu.
c) Hojji huweza kutumwa kwa mhojiwa bila kuwepo kwa mtafiti. Mhojiwa husoma na kujaza hojaji bila mwongozo wa mtafiti (aina hii ndiyo iliyozoeleka zaidi )

**Umuhimu wa hojaji**
a) Huwa na gharama ya chini zaidi.
b) Mtafiti huweza kusikia iidadi kubwa ya watoaji habarikwa kipindi kifupi kwani huweza kutumiwa kwa posta.
c) Huweza kutumika katika mahojiano kama mwongozo.
d) Humpa mhojiwa muda wa kuwaza na kuchunguza.
e) Kwa kawaida , hojaji hazina athari za mtafiti kwani aghalabu mtafiti hayupo zinapojazwa .Huweza kubadilishwa kulingana na kiwango cha wajazaji au wahojiwa.

**Udhaifu wa hojaji**

a) Maswali yenye utata husababisha fasiri mbalimbali zifanyazo mategemeo yasitegemeke.
b) Huenda watu wakakosa kuijaza hojaji kwa kikamilifu kwa sababu mbalimbali kama vile kuhofia lawama au wakakataa kujaza kabisa.
c) Hojaji ndefu huenda baadhi ya watu wakakataa kuijaza.

d) Hojaji wazi huwa ngumu sana kwa mtafiti kuchanganua data, uchanganuzi huchukua muda mrefu.
e) Huenda wahojiwa wasijaze mambo ya kweli, si rahisi kwa mtafiti kuthibitisha kama habari zilizojazwa ni kweli.
f) Wahojiwa wanaweza kuchelewa kutuma hojaji zao, hasa zinazotumwa kwa posta.
g) Baadhi ya wazee, japo wana habari za kutegemewa, hawajui kusoma na kuandika hivyo hawawezi kujaza hojaji isipokuwa waanaposaidiwa na watafiti.
h) Kwa vile mtafiti hakabiliani na mhojiwa ana kwa ana, hawezi kupata sifa za uwasilishaji wa vipera vya fasihi simulizi kama vile toni na kidatu.

**6. Mahojiano**

Mkusanyaji hakabiliana ana kwa ana na watu anaonuia kupata maarifa kutoka kwao. Mkusanyaji atakuwa ameandaa maswali atakayouliza katika kikao rasmi mkusanyaji pia anaweza kushiriki mahojiano yasiyo rasmi bila kunakili majibu papo hapo, maelezo huweza kuhifadhiwa katika kanda ya kunasa sauti.

**Umuhimu wa mahojiano**

a) Kwa vile mtafiti anatazama ana kwa ana na mhojiwa ni rahisi kupata habari za kina na kutegemeka.
b) Mbinu za uwasilishaji k.m toni, ishara za uso na kiimbo hubainika kwa mtafiti hivyo kuimarisha uelewa wake.
c) Mtafiti anaweza kumfafanulia mhojiwa maswali na kumwezesha kupata data ya kuaminika zaidi.
d) Kwa vile mtafiti anamhoji mlengwa moja kwa moja anaweza kurekodi majibu ya mhojiwa moja kwa moja au kuyaandika, si rahisi kupotea.
e) Mtafiti huweza kubadilisha mtindo wa kuhoji kulingana na kiwango cha elimu cha mhojiwa, ili kupata majibu bora zaidi.

**Udhaifu wa mahojiano**.

a) Mahojiano yanahitaji stadi za mawasiliano za kiwango cha juu ikiwa mtafiti hana hizi stadi huenda akaathiri majibu ya mhojiwa.
b) Urasmi unaotokana na vikao vya mahojiano huenda ukatatiza mawasiliano kati ya mhoji na mhojiwa.
c) Ukosefu wa muda wa kutosha wa mahojiano, mahojiano huchukua muda mrefu na huenda mtafiti akakosa kupata muda kumhoji huenda asimwamini mtafiti ahisi kuwa anapelelezwa na kukataa kutoa habari.
d) Kiwango cha elimu cha mtafiti huenda kikawahajisha na kuwatia wahojiwa hisia za unyonge na kuwafanya kutoa habari za zisizotegemewa.

e) Wahojiwa wengine huenda wakampa mtafiti habari za uongo ili kumfurahisha.
f) Matatizo ya kutafsiri, ikiwa data imeandikwa kwa lugha tofauti huenda yakaathiri mahojiano.
g) Mahojiano ni njia ghali ya kutafiti kutokana na gharama ya usafiri kwenda nyanjani.

**Vifaa vya kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi**.

Ukusanyaji wa fasihi simulizi huhitaji vifaa vya kuhifadhi ujumbe; vifaa hivi ni pamoja na

i) **Kalamu na karatasi (maandishi)**

Mkusanyaji wa data ya fasihi simulizi anaweza kutazama au kushiriki na baadaye akaandika aliyoyashuhudia aidha anaweza kuandika wakati maelezo, masimuulizi au sanaa yenyewe inapoendelezwa iwapo anatazama. Hata hivyo vifaa hivi vya kukusanya fasihi simulizi vina udhaifu.

**Umuhimu wa maandishi**.

a. Data kama vile hadithi, huhifadhiwa kama ilivyotambwa hivyo si rahisi kusahauliwa mashairi na ngano nyingi zimeandikwa vitabuni.
b. Huweza kufikia vizazi vingi kwani maandishi hudumu.
c. Si ghali kama baadhi ya mbinu nyinginezo k.m video
d. Si rahisi kufisidiwa au kupotea, hasa zikiandikwa katika vitabu hadithi, methali na vitendawili vingi vimehifadhiwa hivi.

**Udhaifu wa maandishi**

a) Kuna mambo k.m kiimbo, toni, ishara, hisia na mapigo ya mziki ambayo hayawezi kuandikwa kama yalivyowasilishwa na fanani, hivyo hupotea.
b) Aidha, kwa vile maandishi si hai, hayawezi kutenda wala kusema ule uhai hasilia wa fasihi simulizi hufifishwa na kupotezwa na maandishi
c) Baadhi ya watafiti huenda wakandika yale ambayo wanahitaji kwa wakati mahususi na kupuuza mengine k.m ikiwa mada yake ni ‘wahusika katika ngano za kimapokeo’ huenda akajihusisha na wahusika na kupuuza vipengele vingine k.m fanani haya huipunja fasihi simulizi
d) Kuandika fasihi simulizi huifanya kukosa ile taathira asilia kwani kunaipokonya hadhira yake ile fursa ya kushirikiana ana kwa ana na fanani, mtu hawezi kuuliza jambo

e) Kuandika fasihi simulizi huidhibiti na kupunguza hadhira yake na kuathiri vibaya usambazaji wake fasihi inapoandikwa inawafikia wale tu wanajua kusoma

**iii) Vinasasauti /tepurekoda**

Vinasasauti hupata sauti,toni na mahadhi ya tungo za fashi simulizi.Vinaweza kutumiwa katika mahojiano au mtu anaposhiriki au kutazama fasihi simulizi ikiigizwa ingawa ni bora kuliko kalamu na karatasi, pia haiwezi kurekodi matendo na miondoko ya wasanii.

**Umuhimu wa vinasasauti**

a. Sauti ya mhojiwa /fanani huweza kuhifadhiwa.
b. Sifa ya uhai wa fasihi simulizi huhifadhiwa kwani kinasasauti hunasa sifa kama vile za kidatu,toni na kiimbo cha mtambaji.
c. Mkusanyaji wa fasihi simulizi anaweza kurudia kusikiliza uwasilishaji au mahojiano iwapo hakuelewa .sifa hii haipatikani katika maandishi.

**Udhaifu wa vinasasauti /tepurekodi**.

a) Kinasasauti huhitaji nguvu za umeme au betri hivyo hakiwezi kutumiwa katika sehemu zisizo na huduma hizi aidha nguvu za umeme zikikosekana kabla ya utafiti kukamilka utafiti utaathirika. Mtafiti atalazimika kuanza utafiti wake.
b) Kinasasauti hakiwezi kumnasa mtambaji wala uigizaji wake, watu wanaotumia kazi iliyorekodiwa basi hukosa ile taathira ambayo inaibuliwa na kukabiliana ana kwa ana na mtambaji.

**iv)** Baadhi ya wahojiwa au mfanani wasitambe ikiwa wanajua kuwa wanarekodiwa, mtafiti anaweza kupata data ya kutegemewa kama alivyotarajia kuipata.

**v) Kamera**

Kamera huweza kunasa picha zinazoonyesha kipengele kimoja tu bila kuonyesha misogeo au miondoko wala sauti hata hivyo, kamera huweza kuonyesha maleba .

**vi) Video**

Video zinaweza kuchukua picha na pia kunasa sauti na miondoko ni njia nzuri ya kukusanya fasihi simulizi isipokuwa ni ghali.

**vii) Sinema au filamu**

Filamu pia huonyesha picha za miondoko na sauti kama video kama ilivyo katika video, filamu huwa ghali

**Umuhimu**

a) Filamu na video hunasa picha na sauti ,hivyo kuhifahi uigizaji, ishara na kiimbo
b) Uhalisi wa mandhari ambamo kazi ya kifasihi inajikita huonekana na watumizi wa kazi iliyohifadhiwa kwa filamu au video
c) Huipa fasihi simulizi uhai na taathira zaidi kuliko kazi zilizohifadhiwa kwa maandisi, kamera na kinasasauti

**Udhaifu wa filamu na video**

a) Ni njia ghali ya kuhifadhi data
b) Data hii huweza kufisidiwa, hivyo kutofaidi waliolegwa

njia nyingine za kisasa ambazo hutumiwa kuhifadhia na kuendeleza fasihi simulizi ni;

i. Diski za kompyuta: mdaki, diski mweko (hard disk), kadi simaki (memory card) kadiwia/mkamimo(flash disk)
ii. Magazeti k.m hadithi huandikwa mara nyingine gazetini.
iii. Michezo ya kuigiza inayopeperushwa moja kwa moja kupitia runinga na redio na mashirika ya uigizaji
iv. Tamasha za muziki zinazofanywa shuleni kila mwaka.

**Umuhimu wa kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi**.

a) Fasihi simulizi ni hifadhi ya mitazamo ya kitamaduni ya jamii, ukusanyaji utampa mwanafunzi wa fasihi simulizi fursa ya kuingiliana na jamii iliyozaa fasihi husika ili kuweza kuielewa nyema.
b) Ukusanyaji humpa mwanafunzi wa fasihi simulizi nafasi ya kushuhudia na kuathiriwa moja kwa moja na utendaji wa fasihi simulizi hivyo mwanafunzi huona vipengele hai vya fasihi simulizi k.m uigizaji na hivyo kuielewa kwa kina.
c) Husaidia kurekodi na kuhifadhi tamaduni za jamii na kuzipitisha kwa vizazi vijavyo.
d) Ukusanyaji huiendeleza fasihi simulizi, kwa kurekodi vipera kama ngano, hekiya, historia na mtazamo wa kijumla wa jamii kuhusu maisha huhifadhiwa na kupitishwa
e) Husaidia kuziba pengo la utafiti lililopo, tanzu nyingi za fasihi simulizi hazijafanyiwa utafiti wa kutosha ili kuzihifadhi ukusanyaji utasaidia kuziba pengo hili.
f) Hutumika kama msingi wa uchunguzi wa kiulinganishi wa fasihi simulizi za jamii mbalimbali k.m muundo wa utambaji ngano katika jamii mbalimbali.

g) Ili kuelewa ni kwa nini kwa mfano, utungo mmoja wa fasihi simulizi ukawasilishwa kwa njia tofauti katika muktadha tofauti/jambo hili huwawezesha watafiti na wasomi kuelewa sifa za tungo za fasihi.
h) Utafiti wa fasihi simulizi huwezesha mwanafunzi kupata maarifa au stadi za kufanya utafiti katika taaluma nyingine k.m sosholojia.
i) Husaidia kurekebisha mawazo potovu kuhusu fasihi simulizi k.m kujua ni tanzu gani zilizokuwa za awali kabisa. Umewawezesha wasomi kutambua kuwa tungo nyingi zilizoandikwa zilitokana na simulizi za tungo za fasihi simulizi k.m riwaya, hadithi fupi na novella.

**Matatizo yanayomkabili mkusanyaji wa fasihi simulizi**

a) Gharama ya utafiti, huenda ikawa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu huenda akakosa pesa za kusafiri au kununua vifaa.
b) Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu ujazaji wa hojaji huenda ukawafanya wengi wao kutojaza hojaji hizo.
c) Wanajamii wengine huweza kushuku kwamba mtafiti anawapeleleza na wakakatoa kutoa habari.
d) Baadhi ya mafanani au wahojiwa huenda wakadai walipwe kabla ya kutoa habari zozote.
e) Mbinu nyingine k.m hojaji huhitaji watu wanaojua kusoma na kuandika ikiwa watu wanaohojiwa hawajui kusoma na kuandika matokeo ya utafiti huenda yasiwe ya kutegemewa.
f) Vizingiti vya kidini .hutokea pale ambapo wahojiwa wanaamini kuwa matendo ya fasihi simulizi k.m matambika ni kinyume cha dini hivyo kukataa kuhojiwa.
g) Kupotea au kufisidiwa kwa vifaa vya kuhifadhia data, yote yaliyohifadhiwa kwayo pia hupotea.
h) Uchache wa wazee au wataalamu wa fasihi simulizi, fasihi simulizi ilikwa maarufu miongoni mwa wazee na hivyo kukosekana kwao hutatiza ukusanyaji
i) Vikwazo kutoka kwa watawala, huenda watawala wakakataa kutoa idhini ya kufanya utafiti baadhi ya taasisi fadhili pia huenda zikakataa kudhamini utafiti.
j) Wadhamini mara nyingi ndio huamua mambo yanayochunguza, mahali pa kuchunguziwa na mawanda au upeo wa uchunguzi la sivyo, mapendekezo hufutiliwa mbali.
k) Huenda mtafiti asiwe na muda wa kutosha kuwahoji watu wengi, basi hatapata habari za kutosha kuhusu mada husika.
l) Matatizo ya mawasiliano na uchukuzi k.m katika kuenda katika sehemu zilizo kama, bila uchukuzi au vyombo vya usafiri.

m) Matatizo ya kibinafsi, mtafiti anaweza kushindwa kuidhibiti hadhira badala ya kuwauliza maswali, mhojiwa ndio huweza kumuuliza mtafiti maswali pia kutojua lugha husika huwa tatizo

n) Ukosefu wa usalama huenda mtafiti akavamiwa aidha baadhi ya watu si karimu na huenda wakamshuku mtafiti ua kumvamia.

o) Tafsiri za data pia ni tatizo fasihi simulizi huendelezwa kwa lugha za kijamii kupata msamiati unaofaa kufasiri lugha chanzi hadi lugha pokezi ni tatizo.

**MASWALI YA UDURUSU**

1. Ainisha vipera vya fasihi za simulizi
2. Tofautisha kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi
3. Fafanua umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii ya sasa
4. Linganisha methali na vitendawili
5. Eleza namna ya kuainisha nyimbo
6. Eleza umuhimu wa mawaidha miongoni mwa vijana katika jamii
7. Eleza istilahi zifuatazo

   Ayari

   Simo

   Nyiso

   Mbolezi

   Mbazi

   Lakabu

8. Tofautisha kati ya misemo, nahau misimu huku ukitoa mifano mwafaka
9. Fafanua mambo ya kuzingatia unapoainisha methali
10. Maigizo ni nini?

20. Taja vipera vyovyote viwili vya maigizo
21. Eleza dhima zozote tano za maigizo
22. Jadili njia zinazotumiwa na kizazi cha sasa kuendeleza utanzu huu.

23. Fafanua sifa **nne** za maigizo.

24. Maghani ni nini ?

25. Fafanua aina tano za maghani

26. Eleza majukumu manne ya maghani.

27. Eleza vikwazo mbalimbali vya ukuaji wa fasihi simulizi.

28. Eleza tofauti **mbili** kati ya misimu na misemo katika fasihi simulizi.

29. Eleza maana ya ngomezi.

30. Fafanua sifa zozote tano za ngomezi.

*FOR FORM 2, 3, 4 NOTES, SMS OR WHATSAPP:* **0723981225**